# Nipashe

Jumatano Aprili 1, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580194

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

MWANGA WA JAMII


## NEC yaanika kasoro maboresho daftari la kudumu la wapigakura

UKURASA 3


Bunge 2015/2020 na alama zisizofutika

Ukurasa 14
Buriani Khalifa mwanasiasa mwenye msimamo usioyumba

Ukurasa 15

siasa
JUMATANO APRILI 1, 2020
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

Ukurasa 19
Darasa la JPM na utata wa corona uchaguzi mkuu

Corona kuamua hatima uchaguzi mkuu 2020
• Ni wa mataifa 19 imo Tanzania, Marekani, Burundi, Niger, Malawi

Na Maulid Mmbaga

PAMOJA na janga la mlipuko wa homa ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona -COVID 19, bado mwaka wa 2020, ni msimu ambao umesheheni uchaguzi wa kisiasa katika nchi mbalimbali duniani ikiwamo Tanzania na Marekani.

Viongozi wanaotarajiwa kuchaguliwa kwa Tanzania Oktoba mwaka huu ni pamoja na marais wa Zanzibar na wa Jamhuri ya Muungano, wabunge, wawakilishi na madiwani.

Mbali na suala hilo la uchaguzi, virusi vya corona vimezua taha-

INAENDELEA UK.16

Ukurasa 18
Afrika yaweka vikwazo mataifa ya Magharibi

Rais John Magufuli akipiga kura yake. PICHA: MTANDAO.

Rais Congo Brazzaville afariki dunia na corona Ukurasa 17

UKURASA 13

TISHIO CORONA

# TAHARUKI YATANDA

**MTANZANIA** wa kwanza afa kwa corona, upinzani waibana serikali, Spika ataka umoja kuikabili, Nabii atangaza kuvaa gunia siku 40 kuombea itoweke... *Endelea ukurasa 2, 8,11, 22, 23, 26*







Msongamano wa wananchi katika kituo cha mabasi ya mwendokasi cha Kimara, jijini Dar es Salaam jana, kutokana na serikali kutoa maelekezo ya vyombo hivyo, kupakia abiria wanaotosha kwenye viti 'level seat', kwa tahadhari ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona. **Picha ndogo:** Daladala likiwa limepakia abiria waliokaa kwenye viti tu, huku wengine wakisubiri usafiri kwa muda mrefu katika kituo cha Gongo la Mboto. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# ... 'Level seat' yazua kizaazaa usafiri Dar

UKURASA 2



## BAA LA CORONA

"TUSILETE siasa kwenye suala hili kuwa wakipakia abiria kulingana na idadi ya viti hawatapata faida, hili ni janga lisichukuliwe kwa urahisi." Katibu wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (Taboa), Enea Mrutu.

* **Epuka mikusanyiko ya watu**
* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana kwa kushika mikono na kukumbatiana**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## TMA YAONYA MVUA KUBWA KULETA MAAFA MIKOA 15

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


MICHEZO **KAGERE, KAHATA WAITESA SIMBA** UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA

# Serikali yatangaza kifo kimoja cha corona

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ametangaza kifo cha mgonjwa wa kwanza aliyeambukizwa virusi vya corona.

Mwalimu alitangaza kifo hicho jana na kueleza kuwa mgonjwa huyo alifariki jana alfajiri katika kituo cha matibabu ya wagonjwa wa corona kilichopo Mloganzila, jijini Dar es Salaam.

"Marehemu ni Mtanzania, mwanaume mwenye umri wa miaka 49 ambaye alikuwa akisumbuliwa na maradhi mengine," alisema.

Waziri Mwalimu alisema hadi Machi 31, jumla ya watu waliopata maambukizi nchini walikuwa 19, aliyepona ni mmoja na kifo kimoja.

Mikoa iliyotangazwa kuwa na watu wenye maambukizi ni Dar es Salaam, Arusha na visiwani Zanzibar na tayari serikali imeshachukua hatua madhubuti ikiwa ni pamoja na kufunga shule na vyuo.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Mohammed Dewji katika ukurasa wake wa Instagram aliandika, "Pumzika kwa amani mpendwa wetu Iddi. Tumesoma pamoja Arusha School, urafiki wetu tukaurithisha hadi kwa watoto wetu kuwa marafiki na sisi kuendelea kufurahia mechi za Simba pamoja. Pumzika kwa amani rafiki yangu, nasi tuko njiani.

Inna lillahi wa inna ilayhi raji'un."

Rais wa Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF), Phares Magesa, ambaye ni rafiki wa marehemu, aliandika katika ukurasa wake wa Facebook kuwa, "Nimesikitishwa sana kusikia kifo cha ghafla cha rafiki yangu Idd Mbita.

"Salamu nyingi za pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wote kwa msiba huu mkubwa, Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi, Amina."

Ugonjwa huu ambao umeenea nchi mbalimbali duniani na kuua mamia ya wananchi tayari Shirika la Afya Duniani, (WHO) limeutangaza kama janga la dunia.

Baadhi ya nchi, zimefunga mipaka yake na kutoruhusu watu kuingia au kutoka kwenye nchi husika na nyingine watu wamezuiliwa kutoka nje ili kutoruhusu maambukizi zaidi.

Miongoni mwa tahadhari ambazo zimekuwa zikitolewa kila mara ni watu kuepuka mikusanyiko, kunawa mikono kila mara kwa kutumia vitakasa mikono au sabuni za maji.



Waumini wa Kanisa la Africa Inland Church Tanzania (AICT ), mkoani Mwanza, wakifanya ibada ya maombi maalumu juzi, ya kufunga ili kuliombea taifa kulinusuru na maambukizi ya virusi ya ugonjwa wa corona, kansa, kifafa, kisukari na uonevu wa kipepo. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# ... 'Level seat' yaleta kizaazaa usafiri Dar

**Na Waandishi Wetu**

WATUMIAJI wa usafiri wa daladala katika Jiji la Dar es Salaam, jana walijikuta katika wakati mgumu baada ya kuanza utaratibu wa kupakia abiria kulingana na idadi ya viti ili kuzuia msongamano na kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona.

Hata hivyo, baadhi ya daladala zimefanya udanganyifu kwa kuwakalisha abiria chini ili wanapopita karibu na askari wa usalama barabarani wasikamatwe, jambo linaloweza kusababisha hatari ya kusambaa kwa maambukizi ya virusi hivyo.

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini (Latra), ilitoa agizo la kuwataka wasafirishaji wote kuchukua tahadhari kwa kuhakikisha hakuna abiria wanaosimama kwenye magari yao na badala yake wote wakae kwenye viti ikiwamo kunawa mikono kabla ya kupanda magari hayo.

Mabadiliko hayo yalizua taharuki jijini humo na kusababisha msongamano wa abiria kwenye vituo mbalimbali.

Nipashe katika uchunguzi wake wa hali ya usafiri kwa Jiji la Dar es Salaam, ilibaini baadhi ya makondakta na madereva wanavyokiuka agizo hilo, huku kukiwa na msongamano kwenye vituo vya abiria na utekelezaji wa agizo hilo ukifanyika asubuhi pekee.

BARABARA YA BAGAMOYO

Katika barabara ya Bagamoyo, Nipashe ilishuhudia daladala zikiwa zimebeba abiria waliokaa kwenye viti na kukataa kuchukua zaidi.

Makondakta wa daladala za njia hiyo wengi walisikika wakiambizana kati ya daladala moja na nyingine walipokutana kuchukua tahadhari ya kutozidisha abiria.

"Aisee usisimamishe abiria, kuna askari wamemwagwa barabarani leo, ukisimamisha abiria tu, unakamatwa," alisikika mmoja wa kondakta wa daladala moja inayofanya safari zake katika barabara hiyo ya Bagamoyo kutoka Bunju kwenda Kawe.

Mmoja wa kondakta wa daladala linalofanya safari zake kutoka Bunju hadi Morocco, alisema kwa sasa hawako tayari kupakia abiria kuzidi idadi ya viti vya gari kwa sababu wakikamatwa na askari wa barabarani wanatozwa faini kubwa.

Katika daladala hiyo, kondakta alikuwa akipakia abiria baada ya wengine kuteremka.

Kutokana na hali hiyo, katika barabara hiyo, abiria walionekana wengi kukwama vituoni wakihangaika kupata usafiri.

Pia, baadhi ya daladala ziliwalazimisha abiria kuchuchumaa kama wanakubali kupanda lengo likiwa ni kuwapumbaza polisi.

**BARABARA YA PUGU**

Wasafiri wengi wa eneo la Chanika barabara ya Pugu jana walionekana wakitembea kwa miguu baada ya madereva na makondakta kukataa kuwapakiza.

Daladala zinazofanya safari zake Machinga Complex, Mnazi Mmoja, Gerezani, Tabata Chang'ombe, Tabata Segerea na Temeke zilipita kwenye vituo mbalimbali kutoka Chanika na vitongoji vyake bila kusimama kuongeza abiria kama ilivyozoeleka.

Baadhi ya wananchi waliamua kutembea kutokana na kupoteza matumaini ya kupata usafiri. Zawadi Abdallah, Mkazi wa Ngwale aliiambia Nipashe akiwa eneo la Nguvu Kazi kwamba ametembea kwa lengo kufuata magari ya kugeuka nayo ili apate siti, lakini yanapita bila kusimama.

"Hapa nilipo nimechoka niko hoi kwa kutembea kila gari linalopita limejaa halina nafasi hata ya kwenda kugeuka nalo inabidi nitembee bosi wangu hatanielewa kabisa lazima niende kazini," alisema Abdallah.

BARABARA YA MOROGORO

Miongoni mwa daladala hizo ni zile zinazofanya safari zake kati ya Mbezi Mwisho hadi Makumbusho, Makumbusho hadi Kawe kupitia barabara ya Morogoro huku baadhi ya makondakta wakisema hawawezi kuacha abiria.

"Kila mtu anataka kuwahi kwenye shughuli zake, kwanini tumwache, atapata usafiri gani muda huu?" Alisikika kondakta mmoja alipokuwa akiulizwa na baadhi ya abiria.

Monica John, alisema kitendo cha baadhi ya abiria kuning'inia mlangoni ni dalili kwamba kuna tatizo la usafiri ambalo linatakiwa kupatiwa ufumbuzi, vinginevyo muda ambao mamlaka husika zitakuwa hazijaanza kazi, daladala zitaendelea kujaza abiria kama kawaida.

**BARABARA YA MANDELA**

Msafiri Shabani Kange, mkazi wa Gongolamboto, alisema tahadhari ya kujikinga na ugonjwa wa corona inachukuliwa, isipokuwa suala la daladala kubeba kulingana na viti vilivyopo limesababisha mtafaruku mkubwa.

Alisema suala hilo limeongeza tatizo la usafiri kutokana na magari yaliyopo hayatoshelezi na hivyo abiria kusongamana kwenye vituo.

Aliiomba serikali kulitazama jambo hilo ili kuepusha msongamano kwenye magari, lakini katika stendi bado upo palepale, pia aliwatolea malalamiko baadhi ya makondakta wa daladala kwa kupandisha nauli bila kufuata utaratibu.

"Kuna baadhi ya makondakta wanatumia kigezo cha shida ya usafiri kupandisha nauli, sehemu yenye umbali wa kulipa Sh. 500, wanapandisha hadi Sh. 1,000," alisema Kange.

Bakari Shabani ambaye ni kondakta wa daladala inayosafirisha abiria kutoka Gongolamboto kwenda Makumbusho, alipoulizwa kuhusu suala hilo na baadhi yao kupandisha nauli, alisema kuna changamoto kubwa katika kutekeleza kwa kuwa kupandisha abiria kwa idadi ya viti ni hasara.

Alisema sheria hiyo inachangamoto kwa kuwa inasababisha kukosa kipato kutokana na kiasi kidogo cha nauli iliyowekwa na kutoa mapato makubwa kama tozo ya magari yao.

"Suala la abiria kukaa kulingana na idadi ya viti linasababisha mkusanyiko mkubwa wa abiria jambo linalosababisha watu kuamua kugeuza na gari ili apate siti, hapo ndipo anapotozwa nauli mara mbili, lakini akipanda mwanzo wa kituo analipa kiasi kilekile kilicho zoeleka," alisema Shabani.

***Imeandikwa na Elizabeth Zaya, Hellen Mwango na Mauld Mmbaga.***

## HABARI KITAIFA

# Kasoro uboreshaji Daftari la Wapigakura zaanikwa

**Na Beatrice Moses**

KAMATI ya Uangalizi wa Uchaguzi Tanzania (Temco), imebainisha kuwapo kwa dosari kadhaa katika uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura.

Miongoni mwa kasoro hizo ni baadhi ya watu kuzuiwa kujiandikisha kwa sababu walivaa fulana zenye kola ya duara.

Dosari nyingine ni ushiriki mdogo wa vyama vya siasa, ambapo vyama vinne pekee ndiyo viliweka mawakala wachache kwenye baadhi ya maeneo, kwenye mamlaka zote 89 za Serikali ya Mtaa zilizoangaliwa na Temco.

Katika taarifa ya Awali Kuhusu Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura ya Temco iliyotolewa juzi, imebainisha kuwa ilianza kuangalia uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura Desemba 1, 2019 mpaka Februari 23, mwaka huu. Temco ilifanya kazi hiyo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa 89 katika mikoa 16 ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo iliyowasilisha na Mwenyekiti wa Mpango wa Utafiti na Elimu ya Demokrasia Tanzania (Redet), Prof. Rwekaza Mukandala na Mwenyekiti wa Temco, Dk. Rasul Minja, ushiriki wa vyama vya siasa ni muhimu kwa mafanikio na kuaminika kwa mchakato wowote wa uchaguzi.

Ilibainishwa kuwa ni vyama vinne vya siasa ambavyo viliweka mawakala kwenye vituo vya kuandikisha wapigakura, CCM iliweka mawakala kwenye vituo 262 (asilimia 43), ACT-Wazalendo kwenye vituo 56 (asilimia 9), CUF kwenye vituo 20 (asilimia 3) na Chadema kwenye vituo 30 (asilimia 5).

"Iligundulika kwa mshangao mkubwa katika baadhi ya vituo vya kuandikisha wapigakura Mbeya maofisa waandikishaji wapigakura walimrudisha mtu yeyote aliyekwenda kujiandikisha akiwa amevaa fulana yenye kola ya duara," ilielezwa katika taarifa hiyo.

Dosari nyingine ni kuwa licha ya Temco kutoa elimu ya mpigakura kwa kiasi kikubwa, wadau wengine, asasi za kiraia na vyama vya siasa, hawakushiriki sana kwenye utoaji wa elimu hiyo, hali ambayo iliipa tume mzigo mkubwa.

Uwapo wa wataalamu wa Tehama ambao unatajwa kuwa ulihakikisha kwamba mashine za BRV zinafanya kazi kwa kiwango cha juu, haukusaidia ilivyotarajiwa kwa kuwa kuna wakati walishindwa kuvifikia vituo vingi, na kusababisha ucheleweshaji au kusitishwa kwa zoezi la kuandikisha wapigakura kwa muda.

"Kuharibika mara kwa mara kwa mashine za BVR, mashine za kuchapa na kamera na kutofanya kazi kwa kompyuta ni mambo ambayo yalijitokeza kwenye vituo vichache, na hii ilisababisha kuahirishwa kwa zoezi la kuandikisha wapigakura," ilielezwa.

"Temco ilishuhudia ucheleweshaji wa vifaa vya kuandikisha wapigakura Zanzibar na mikoa ya Njombe na Ruvuma; hali hii ilisababisha zoezi liahirishwe kwa siku mbili, pia vituo vingi havikuwa na walinzi, ingawa hapakuwa na matukio ya vurugu yaliyoonyesha ulazima wa kupeleka vyombo vya usalama, shughuli kama hizi ni muhimu zifanyike pakiwa na ulinzi."

TEMCO ilipendekeza kuwa serikali inapaswa kuhakikisha kwamba michakato ya uandikishaji wapigakura ya miaka ijayo na masuala ya uchaguzi mengine yanafanyika pakiwa na ulinzi, walau askari mmoja kwa kila kituo.

# Spika ataka taarifa maafa ya mafuriko

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

> **"Ni maafa makubwa sana, ninaamini serikali imesikia ujumbe wa mbunge na serikali imekuwa ikiendelea kuchukua hatua mbalimbali na wakati fulani utafika tutaiomba serikali kutoa taarifa juu ya mipango inayoendelea nayo.**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ametaka serikali kujipanga kutoa taarifa rasmi bungeni kuhusu maafa yaliyotokea nchini kutokana na mvua kubwa inayoendelea kunyesha.

Kiongozi huyo wa Bunge alitoa agizo hilo jana, bungeni jijini hapa, alipojibu hoja ya Mbunge wa Rufiji (CCM), Mohamed Mchengerwa, aliyeitaka serikali kulitaarifu Bunge hatua inazochukua kuwasaidia wananchi wa Rufiji ambao sasa hawana makazi kutokana na mvua hiyo.

Mchengerwa alisema kutokana na mvua hiyo, hadi sasa wananchi wanaokadiriwa kuwa kati ya 20,000 na 50,000 hawana makazi, chakula na wanahangaika kuokoa maisha yao.

"Je, kama Bunge tunachukua hatua gani ili kuwaangalia hata hawa wananchi wanyonge ambao wako kwenye maafa ya mafuriko?" Mchengerwa alihoji.

Akijibu hoja hiyo, Spika Ndugai alitoa pole kwa wananchi wa Rufiji na Kibiti kutokana na baa hilo na kusema kuwa mafuriko ya aina hiyo yaliyotokea katika eneo hilo ni ya aina yake kulinganishwa na miaka ya nyuma.

"Ni maafa makubwa sana, ninaamini serikali imesikia ujumbe wa mbunge na serikali imekuwa ikiendelea kuchukua hatua mbalimbali na wakati fulani utafika tutaiomba serikali kutoa taarifa juu ya mipango inayoendelea nayo.

"Tunapokea ushauri wake Mheshimiwa Mbunge, na Mheshimiwa Jenista (Mhagama) ambaye ndiye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya maafa, yako chini yake, wakati utakapofika, atatupa taarifa kama Bunge kuhusu maafa haya," aliagiza.



Sheikhe Sharifu Hashimu, akiongoza ibada ya kuusalia mwili wa aliyekuwa Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Salum Shamte, nyumbani kwake Mbweni, jijini Dar es Salaam jana, kabla ya mazishi yake yaliyofanyika katika makaburi ya Kisutu jijini humo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TMA yaonya mvua kubwa mikoa 15

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imetoa tahadhari ya mvua kubwa kwa siku mbili kuanzia kesho katika mikoa 15 ikiwamo Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na mamlaka hiyo, katika siku hizo, kutakuwa na mvua kubwa katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Njombe, Iringa, Songwe, Mbeya na Rukwa.

Meneja wa Kituo Kikuu cha Utabiri wa Hali ya Hewa (TMA), Samuel Mbuya, alisema kutokana na tahadhari hiyo, athari zinazoweza kutokea kwenye maeneo hayo ni makazi na barabara mbovu kuzungukwa na maji hali itakayosababisha kukosekana kwa makazi na adha ya usafiri.

Kwa siku ya Ijumaa, alisema mvua kubwa inatarajiwa katika baadhi ya maeneo ya Jiji la Dar es Salaam, Zanzibar, Pwani, Mafia, Tanga, Manyara, Kilimanjaro, Arusha, Morogoro na kujirudia tena mikoa ya Njombe na Iringa.

Mbuya alisema kutokana na tahadhari hiyo, wakazi wa mikoa hiyo wanapaswa kuchukua hatua za kujikinga na kuendelea kufuatilia taarifa zinazotolewa na TMA.

" Ijumaa pia athari zinazoweza kutokea ni pamoja na miundombinu kuharibika na baadhi ya makazi ya watu kuzungukwa na maji. Ni vyema wananchi wa maeneo hayo wakachukua tahadhari na kuendelea kufuatilia taarifa zinazotolewa na mamlaka," alisema Mbuya.

Meneja huyo alisema TMA itaendelea kufuatilia mifumo ya hali ya hewa na kuendelea kutoa taarifa kwa wananchi ili kuchukua hatua stahiki.


DRC DANISH REFUGEE COUNCIL

## TANGAZO LA ZABUNI

SHIRIKA LA KUHUDUMIA WAKIMBIZI LA DANISHI LINATARAJIA KUINGIA MKATABA WA UNUNUZI WA V**IFAA VYA UJENZI, VIFAA VYA NYUMBANI, VIFAA VYA OFSINI, VIFAA VYA KILIMO**

KWAHIYO SHIRIKA LA DANISHI LILILOPO KIBONDO LINAWAARIKA WAZABUNI **KULETA BEI ZAO.**

NYARAKA ZA KUJAZIA BEI ZINAPATIKANA KATIKA OFISI ZA DANISHI KIBONDO KUANZIA **TAREHE 31.03.2020 HADI TAREHE 14.03.2020 SIKU ZA KAZI SAA 2:00 ASUBUHI MPAKA SAA 10:30 JIONI.** TUNAPATIKANA BARABARA YA IRC KIBONDO.

***KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA 0623529029*** au ***barua pepe*** steward.mbonalibaye@drc.ngo

**ZABUNI ZITAFUNGULIWA HADHARANI TAREHE 16.04.2020 SAA 4:00 ASUBUHI** OFISI ZA DANISHI KIBONDO NA KAMATI YA KUFUNGUA ZABUNI LA DANISHI.

**UNAWEZA KURUDISHA ZABUNI KUPITIA rfq.tza@drc.ngo AU KULETA MOJAKWA MOJA OFISINI VINGINEVYO NI BATILI.**

215684302

ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2015 Certified

***KUMB: PPR/2020 - 04/1***

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 1 APRILI 2020

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia Jumatano, **Tarehe 1 Aprili 2020.** Pamoja na kutambua bei hizo, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

(a) Bei za jumla na rejareja za mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa yaliyopokelewa nchini kupitia **bandari ya Dar es Salaam** zimepungua ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 4 Machi 2020. Kwa mwezi Aprili 2020, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa Shilingi 116/lita (sawa na asilimia 5.28), Shilingi 165/lita (sawa na asilimia 7.64) na Shilingi 193/lita (sawa na asilimia 9.14), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa Shilingi 116.02/lita (sawa na asilimia 5.58), Shilingi 164.05/lita (sawa na asilimia 8.09) na Shilingi 192.80/lita (sawa na asilimia 9.68), mtawalia.

(b) Pia, bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli, Dizeli na mafuta ya Taa yaliyoingizwa nchini kupitia **bandari ya Tanga** zimepungua ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 4 Machi 2020. Kwa mwezi Aprili 2020, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na mafuta ya Taa **kwa Mikoa ya Kaskazini** (Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara) zimepungua kwa Shilingi 86/lita (sawa na asilimia 3.89), Shilingi 56/lita (sawa na asilimia 2.65) na Shilingi 85/lita (sawa na asilimia 4.09), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na mafuta ya Taa zimepungua kwa Shilingi 85.39/lita (sawa na asilimia 4.11), Shilingi 56.11/lita (sawa na asilimia 2.81) na Shilingi 84.39/lita (sawa na asilimia 4.34), mtawalia.

(c) Kwa mwezi wa April 2020, bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli katika **Mikoa ya Kusini (yaani Mtwara, Lindi na Ruvuma)** hazita badilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 4 Machi 2020. Kwa kuwa hakuna Mafuta ya Taa yaliyopokelewa katika bandari ya Mtwara, wamiliki wa vituo vya mafuta katika mikoa tajwa wanashauriwa kununua mafuta hayo kutoka Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za Mafuta ya Taa kwa mikoa hiyo zinatokana na gharama za mafuta hayo kutokea Dar es Salaam na kusafirishwa hadi mkoa husika.

(d) Mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la ndani yanatokana na mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la dunia na gharama za usafirishaji (BPS Premium) kama inavyoonekana katika **Jedwali C na Jedwali D.**

(e) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.

(f) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

(g) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (price cap)** kama ilivyokokotolewa na kanuni (formula) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 74 la tarehe 7 Februari 2020.**

(h) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**

(i) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (Electronic Fiscal Pump Printers) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

**JEDWALI A: BEI ZA REJAREJA**

| Mji | Bei Kikomo | | |
|---|---|---|---|
| | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta Ya Taa (Shs/Lita) |
| **Dar es Salaam** | **2,087** | **1,989** | **1,923** |
| **Arusha** | **2,174** | **2,127** | **2,044** |
| Arumeru (Usa River) | 2,174 | 2,127 | 2,044 |
| Karatu | 2,192 | 2,145 | 2,062 |
| Longido | 2,185 | 2,138 | 2,055 |
| Monduli | 2,179 | 2,132 | 2,049 |
| Monduli-Makuyuni | 2,184 | 2,137 | 2,054 |
| Ngorongoro (Loliondo) | 2,259 | 2,211 | 2,128 |
| **Pwani (Kibaha)** | **2,092** | **1,994** | **1,928** |
| Bagamoyo | 2,099 | 2,000 | 1,934 |
| Bagamoyo (Miono) | 2,129 | 2,031 | 1,965 |
| Chalinze Junction | 2,102 | 2,003 | 1,937 |
| Chalinze (Msata) | 2,106 | 2,007 | 1,941 |
| Kibiti | 2,108 | 2,009 | 1,943 |
| Kisarawe | 2,095 | 1,996 | 1,930 |
| Mkuranga | 2,097 | 1,999 | 1,933 |
| Rufiji | 2,115 | 2,017 | 1,951 |
| **Dodoma** | **2,146** | **2,048** | **1,982** |
| Bahi | 2,154 | 2,055 | 1,989 |
| Chamwino | 2,142 | 2,043 | 1,977 |
| Chemba | 2,173 | 2,074 | 2,008 |
| Kondoa | 2,179 | 2,081 | 2,015 |
| Kongwa | 2,144 | 2,045 | 1,979 |
| Mpwapwa | 2,147 | 2,049 | 1,983 |
| Mtera (Makatopora) | 2,165 | 2,067 | 2,001 |
| **Geita** | **2,253** | **2,154** | **2,088** |
| Bukombe | 2,242 | 2,143 | 2,077 |
| Chato | 2,274 | 2,175 | 2,110 |
| Mbogwe | 2,291 | 2,193 | 2,127 |
| Nyang'hwale | 2,268 | 2,169 | 2,104 |
| **Iringa** | **2,152** | **2,053** | **1,987** |
| Ismani | 2,157 | 2,058 | 1,992 |
| Kilolo | 2,156 | 2,058 | 1,992 |
| Mufindi (Mafinga) | 2,162 | 2,063 | 1,997 |
| **Kagera (Bukoba)** | **2,303** | **2,205** | **2,139** |
| Biharamulo | 2,277 | 2,179 | 2,113 |
| Karagwe (Kayanga) | 2,319 | 2,221 | 2,155 |
| Kyerwa (Ruberwa) | 2,325 | 2,227 | 2,161 |
| Muleba | 2,303 | 2,205 | 2,139 |
| Ngara | 2,291 | 2,192 | 2,126 |
| Misenyi | 2,312 | 2,213 | 2,147 |
| **Katavi (Mpanda)** | 2,296 | 2,197 | 2,131 |
| Mlele (Inyonga) | 2,315 | 2,216 | 2,150 |
| Mpimbwe (Majimoto) | 2,288 | 2,190 | 2,124 |
| Tanganyika (Ikola) | 2,313 | 2,215 | 2,149 |
| **Kigoma** | **2,319** | **2,220** | **2,155** |
| Uvinza (Lugufu) | 2,331 | 2,233 | 2,167 |
| Buhigwe | 2,308 | 2,210 | 2,144 |
| Kakonko | 2,276 | 2,178 | 2,112 |
| Kasulu | 2,305 | 2,206 | 2,141 |
| Kibondo | 2,283 | 2,185 | 2,119 |

# TANGAZO

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Kilimanjaro (Moshi)** | **2,163** | **2,116** | **2,033** |
| Hai (Bomang'ombe) | 2,167 | 2,120 | 2,037 |
| Mwanga | 2,157 | 2,109 | 2,027 |
| Rombo (Mkuu) | 2,180 | 2,133 | 2,050 |
| Same | 2,150 | 2,103 | 2,020 |
| Siha (Sanya Juu) | 2,170 | 2,123 | 2,040 |
| **Lindi** | **2,280** | **2,196** | **1,982** |
| Lindi-Mtama | 2,285 | 2,201 | 2,000 |
| Kilwa Masoko | 2,304 | 2,220 | 1,957 |
| Liwale | 2,316 | 2,232 | 2,003 |
| Nachingwea | 2,300 | 2,216 | 2,011 |
| Ruangwa | 2,307 | 2,222 | 2,013 |
| **Manyara (Babati)** | **2,208** | **2,161** | **2,078** |
| Hanang (Katesh) | 2,218 | 2,171 | 2,088 |
| Kiteto (Kibaya) | 2,223 | 2,176 | 2,093 |
| Mbulu | 2,221 | 2,173 | 2,091 |
| Simanjiro (Orkasumet) | 2,240 | 2,193 | 2,110 |
| **Mara (Musoma)** | **2,266** | **2,168** | **2,102** |
| Musoma Vijijini (Busekela) | 2,307 | 2,208 | 2,142 |
| Rorya (Ingirijuu) | 2,275 | 2,177 | 2,111 |
| Rorya (Shirati) | 2,310 | 2,211 | 2,145 |
| Bunda | 2,257 | 2,159 | 2,093 |
| Bunda (Kisorya) | 2,267 | 2,168 | 2,102 |
| Butiama | 2,263 | 2,164 | 2,098 |
| Serengeti (Mugumu) | 2,312 | 2,213 | 2,147 |
| Tarime | 2,277 | 2,179 | 2,113 |
| Tarime (Kewanja/Nyamongo) | 2,282 | 2,183 | 2,117 |
| **Mbeya** | **2,195** | **2,096** | **2,030** |
| Chunya | 2,204 | 2,106 | 2,040 |
| Chunya (Makongolosi) | 2,218 | 2,120 | 2,054 |
| Kyela | 2,210 | 2,112 | 2,046 |
| Mbarali (Rujewa) | 2,179 | 2,080 | 2,014 |
| Rungwe (Tukuyu) | 2,204 | 2,105 | 2,039 |
| **Morogoro** | **2,113** | **2,014** | **1,948** |
| Mikumi | 2,128 | 2,030 | 1,964 |
| Kilombero (Ifakara) | 2,150 | 2,052 | 1,986 |
| Kilombero (Mlimba) | 2,173 | 2,074 | 2,008 |
| Kilombero (Mngeta) | 2,162 | 2,063 | 1,997 |
| Ulanga (Mahenge) | 2,161 | 2,063 | 1,997 |
| Malinyi | 2,171 | 2,073 | 2,007 |
| Kilosa | 2,131 | 2,032 | 1,966 |
| Gairo | 2,131 | 2,032 | 1,966 |
| Mvomero (Wami Sokoine) | 2,123 | 2,024 | 1,958 |
| Mvomero (Sanga Sanga) | 2,113 | 2,014 | 1,948 |
| Turiani | 2,138 | 2,039 | 1,973 |
| **Mtwara** | **2,267** | **2,182** | **1,995** |
| Nanyumbu (Mangaka) | 2,303 | 2,219 | 2,044 |
| Masasi | 2,283 | 2,199 | 2,021 |
| Newala | 2,288 | 2,203 | 2,028 |
| Tandahimba | 2,281 | 2,196 | 2,021 |
| Nanyamba | 2,281 | 2,196 | 2,021 |
| **Mwanza** | **2,238** | **2,139** | **2,073** |
| Kwimba | 2,256 | 2,157 | 2,091 |
| Magu | 2,246 | 2,147 | 2,081 |
| Misungwi | 2,232 | 2,134 | 2,068 |
| Sengerema | 2,270 | 2,172 | 2,106 |
| Ukerewe | 2,297 | 2,199 | 2,133 |
| **Njombe** | **2,180** | **2,082** | **2,016** |
| Njombe (Kidegembye) | 2,201 | 2,102 | 2,036 |
| Ludewa | 2,218 | 2,119 | 2,053 |
| Makambako | 2,172 | 2,074 | 2,008 |
| Makete | 2,211 | 2,112 | 2,046 |
| Wanging'ombe (Igwachanya) | 2,178 | 2,079 | 2,013 |
| **Rukwa (Sumbawanga)** | **2,261** | **2,162** | **2,096** |
| Sumbawanga Rural (Mtowisa) | 2,261 | 2,162 | 2,096 |
| Kalambo (Matai) | 2,268 | 2,169 | 2,103 |
| Nkasi (Namanyele) | 2,274 | 2,175 | 2,110 |
| **Ruvuma (Songea)** | **2,352** | **2,268** | **2,046** |
| Mbinga | 2,365 | 2,281 | 2,080 |
| Namtumbo | 2,343 | 2,259 | 2,076 |
| Nyasa (Mbamba Bay) | 2,390 | 2,306 | 2,090 |
| Tunduru | 2,318 | 2,233 | 2,105 |
| **Shinyanga** | **2,216** | **2,118** | **2,052** |
| Kahama | 2,230 | 2,132 | 2,066 |
| Kishapu | 2,245 | 2,146 | 2,080 |
| Ushetu (Nyamilangano) | 2,248 | 2,149 | 2,083 |
| **Simiyu (Bariadi)** | **2,258** | **2,159** | **2,093** |
| Busega (Nyashimo) | 2,251 | 2,152 | 2,086 |
| Itilima (Lagangabilili) | 2,261 | 2,162 | 2,096 |
| Maswa | 2,249 | 2,151 | 2,085 |
| Meatu (Mwanhuzi) | 2,256 | 2,158 | 2,092 |
| **Singida** | **2,178** | **2,080** | **2,014** |
| Iramba | 2,190 | 2,092 | 2,026 |
| Manyoni | 2,163 | 2,064 | 1,998 |
| Ikungi | 2,174 | 2,075 | 2,009 |
| Mkalama (Nduguti) | 2,203 | 2,104 | 2,038 |
| **Songwe (Vwawa)** | **2,204** | **2,105** | **2,039** |
| Songwe (Mkwajuni) | 2,211 | 2,112 | 2,046 |
| Ileje | 2,208 | 2,109 | 2,043 |
| Momba (Chitete) | 2,213 | 2,115 | 2,049 |
| Tunduma | 2,208 | 2,110 | 2,044 |
| **Tabora** | **2,242** | **2,143** | **2,077** |
| Igunga | 2,196 | 2,097 | 2,031 |
| Kaliua | 2,261 | 2,162 | 2,096 |
| Ulyankulu | 2,255 | 2,156 | 2,090 |
| Nzega | 2,206 | 2,108 | 2,042 |
| Sikonge | 2,254 | 2,155 | 2,089 |
| Urambo | 2,255 | 2,156 | 2,090 |
| Uyui | 2,243 | 2,144 | 2,078 |
| **Tanga** | **2,117** | **2,070** | **1,987** |
| Handeni | 2,138 | 2,091 | 2,008 |
| Kilindi | 2,153 | 2,106 | 2,023 |
| Korogwe | 2,129 | 2,082 | 1,999 |
| Lushoto | 2,139 | 2,091 | 2,009 |
| Mkinga (Maramba) | 2,124 | 2,077 | 1,994 |
| Muheza | 2,122 | 2,075 | 1,992 |
| Pangani | 2,124 | 2,077 | 1,994 |

**JEDWALI B: BEI ZA JUMLA**

| BANDARI | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta ya Taa (Shs/Lita) |
|---|---|---|---|
| **DAR ES SALAAM** | 1,961.95 | 1,863.31 | 1,798.17 |
| **TANGA** | 1,991.56 | 1,944.10 | 1,862.19 |
| **MTWARA** | 2,140.83 | 2,056.15 | - |

**JEDWALI C: SABABU ZA MABADILIKO YA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI**

| Bandari | Maelezo | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|---|
| DAR ES SALAAM | Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia | Punguzo la Dola 48.275/Tani | Punguzo la Dola 76.010/Tani | Punguzo la Dola 88.026/Tani |
| | Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (BPS premiums) | Ongezeko la Dola 12.219/Tani | Ongezeko la Dola 3.029/Tani | Ongezeko la Dola 2.810/Tani |
| TANGA | Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia | Punguzo la Dola 62.460/Tani | Punguzo la Dola 47.726/Tani | Punguzo la Dola 49.779/Tani |
| | Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (BPS premiums) | Ongezeko la Dola 5.510/Tani | Ongezeko la Dola 18.680/Tani | Ongezeko la Dola 6.500/Tani |
| MTWARA | Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia | N/A | N/A | N/A |
| | Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (BPS premiums) | N/A | N/A | N/A |

**JEDWALI D: MWEZI HUSIKA WA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA DUNIA**

| | Aina ya Mafuta | Shehena ya Mafuta Ilipokelewa Mwezi: | Mwezi husika wa Bei za Soko la Dunia zilizotumika mwezi huu: | Mwezi husika wa Bei za Soko la Dunia zilizotumika mwezi uliopita: |
|---|---|---|---|---|
| DAR ES SALAAM | Petroli | Machi 2020 | Februari 2020 | Januari 2020 |
| | Dizeli | Machi 2020 | Februari 2020 | Januari 2020 |
| | Mafuta ya Taa | Machi 2020 | Februari 2020 | Januari 2020 |
| TANGA | Petroli | Machi 2020 | Februari 2020 | Novemba 2019 |
| | Dizeli | Machi 2020 | Februari 2020 | Novemba 2019 |
| | Mafuta ya Taa | Machi 2020 | Februari 2020 | Juni 2019 |
| MTWARA | Petroli | Februari 2020 | Januari 2020 | Novemba 2019 |
| | Dizeli | Februari 2020 | Januari 2020 | Novemba 2019 |
| | Mafuta ya Taa | N/A | N/A | N/A |

**Nzinyangwa E. Mchany**
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**
**EWURA"**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Udhibiti uhalifu mpaka wa Msumbiji uwe endelevu

**KUMEKUWAPO** na matukio kadhaa ya uhalifu katika maeneo ya mpaka kati ya Tanzania na Msumbiji.

Matukio hayo yalianza takribani zaidi ya mwaka mmoja uliopita, na yameshasababisha Watanzania kadhaa kupoteza maisha, wakiwamo wanaoingia ndani ya Msumbiji kufanya shughuli za kujipatia riziki.

Hadi sasa sababu zinazosababisha kasi ya matukio hayo hazijajulikana, ingawa hali inaonyesha kuwa tatizo linatoka Msumbiji, hivyo Tanzania nayo kuathirika.

Itakumbukwa kuwa Tanzania na Msumbiji ni mataifa yenye urafiki na udugu wa muda mrefu, kiasi kwamba raia wake wamekuwa wakiishi kila upande, kutokana na kutokuwapo na vikwazo katika mipaka.

Hali hiyo imekuwa ikiwafanya raia wa nchi hizo mbili kwenda kila upande kupata mahitaji zikiwamo huduma na bidhaa na wakati mwingine wengine kwenda kufanya shughuli za kujipatia riziki upande mwingine, ukiwamo uvuvi na ujasiriamali.

Hata hivyo, kuibuka kwa kasi ya matukio ya uhalifu katika maeneo kadhaa ya mpaka wa nchi hizi mbili, yamesababisha kuzorota kwa hali ya usalama, hivyo kuwa tishio kwa upande wa Tanzania.

Moja ya athari ambazo Tanzania imezipata ni raia wake takribani tisa kuuawa ndani ya Msumbiji mwaka jana na watu wasiojulikana kwa silaha za moto, walikokuwa huko kwa shughuli za uvuvi.

Pia matukio kadhaa ya uhalifu yamekuwa yakiendelea na kusababisha kukosekana kwa usalama maeneo ya mpakani, ingawa matukio mengi yamekuwa yakiripotiwa kwa siku za karibuni kutendeka Msumbiji, ukiwamo uvamizi na uporaji wa mali, zikiwamo benki.

Mara kadhaa Jeshi la Polisi la Tanzania limekuwa likieleza kuwa linafuatilia kwa karibu kuhakikisha kuwa usalama wa Watanzania ni wa uhakika na kuahidi kuwasaka na kuwatia mbaroni wahusika.

Taarifa za kutia moyo ni kuwa Jeshi la Polisi kutangaza kuwa kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama vimeimarisha ulinzi katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji kwa lengo la kukabiliana na vitendo vya uhalifu, yakiwamo mauaji.

Hayo yalisemwa juzi mkoani Mtwara na Kamishna wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi nchini, Liberatus Sabas, alipokuwa akikagua kikosi maalumu cha kupambana na uhalifu nchini kilichowasili Mtwara kwa ajili ya kuimarisha ulinzi kwenye mkapa wa nchi hizo.

Alisema kumekuwapo na matukio ya uhalifu yanayofanywa na baadhi ya watu, yakiwamo ya mauaji kwenye maeneo ya mpaka, na kwamba Jeshi la Polisi limekuwa likichukua hatua mbalimbali ikiwamo kuwakamata wahusika na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria.

Kwamba wahalifu hao wamekuwa wakivamia kambi za jeshi, vituo vya polisi, kuchoma moto na kuchukua silaha Msumbiji kisha kuzitumia katika vitendo vya uhalifu kwenye maeneo mbalimbali ya nchi hizo.


Alisema baadhi wamekuwa wakikimbia nchini na kwenda Msumbiji kisha kuungana na wahalifu wa nchi hiyo na kufanya vitendo vya uhalifu kwenye maeneo mbalimbali katika nchi hizo mbili.

Alisema katika operesheni hiyo watahakikisha wanawasaka kwa nguvu zote wahalifu hao na kuwakamata kisha kuwafikisha katika vyombo vya sheria. Tunashauri kwamba operesheni hiyo iwe endelevu hadi matukio hayo yatakapotokomezwa kabisa, na hali ya usalama kurejea.

Ili kuwakamata wahusika wa matendo hayo, Watanzania wanaoishi maeneo ya mpakani hawanabudi kutoa ushirikiano kwa vyombo vya ulinzi na usalama vya Tanzania kwa kutoa taarifa kuhusu watu wote wanaowatilia shaka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Ufuatiliaji visiwani uanze ili kujiepusha na corona

Na Mwandishi Wetu

**MOJA** kati ya nyenzo muhimu za maisha ya binadamu ni afya bora inayompa mtu uwezo wa kufanyakazi na kuzalisha mali. Kwa hali hiyo ndiyo maana kila kijiji kinajengewa zahanati, kata zote zinakuwa na vituo vya afya, wilaya na mikoa ikijengewa hospitali na pia kukiwa na hospitali maalumu za rufani za kanda na za kitaifa.

Hatua hizo zinachukuliwa kwa sababu maisha ya binadamu yanahitaji zaidi afya bora na madhubuti ili kumwezesha kufanyakazi kwa ufanisi na hatimaye kuzalisha mali.

Taifa au jamii ya watu wasio na afya bora ni vigumu kufanyakazi kwani nguvu ndiyo inategemewa zaidi, hivyo lishe bora na huduma bora za matibabu ni kipaumbele ili kupambana na adui maradhi.

Katika uwezekezaji wa huduma za afya visiwa ni eneo ambalo linahitaji kupewa kipaumbele na umuhimu mkubwa.

Pamoja na kwamba wakati huu wa corona ndiyo muda wa kuangalia huduma za afya kwenye visiwa na kuwa makini kwani kuna uwezekano wa watu watakaoona wana matatizo hasa ya maambukizi wakaamua kukimbilia visiwani.

Lakini, pia kuna uwezekano wa wageni kukaa kwenye visiwa na kuongeza nafasi za maradhi kusambaa katika maeneo hayo, hivyo kuna haja ya kuvipa visiwa jicho la pili kuepusha uwezekano wa ugonjwa kusambaa tena ukianzia huko.

Ni vyema pia kufanya msako kwenye sehemu hizo kwa kuwa pamoja na kwamba ni maeneo ya burudani yanaweza pia kutumiwa kama maficho ya wageni ambao wanaweza kuwa na maradhi.

Ni jambo jema pia kuwahimiza wakazi wa maeneo hayo kuwa macho na wageni ambao wanaweza kuwafikishia maradhi hasa corona ambayo inaonekana kwa kiasi kikubwa inaingizwa nchini kutoka kwa wageni wanaotokea nje ya mipaka.

Aidha, pamoja na kuliona tatizo hilo la uwezekano wa wageni kukimbilia kwenye visiwa hasa vyenye maeneo ya burudani, kadhalika kuna umuhimu wa taifa kuwekeza katika sekta ya afya hasa sehemu zisizofikika kama visiwani. Ni muhimu ili huduma za afya zinazotolewa katika sehemu nyingine ziwafikie wanaokaa visiwani.

Halikadhalika ni muhimu kuwashawishi wakazi wa maeneo hayo kuona umuhimu wa kujiunga katika mpango wa mfumo wa bima ya afya ya jamii vijijini (CHF) na mpango wa Bima ya Taifa ya Afya (NHIF) na kuchangia huduma kama hizo.

> **Katika kuhamasisha wananchi kujihadhari na wageni ni vyema kuwahusisha maofisa watendaji wa kata wajumbe wa bodi za afya za zahanati, madiwani wa kamati ya afya, wajumbe wa bodi ya afya ya wilaya, wenyeviti wa serikali za vijiji, viongozi wa dini na asasi za kiraia.**

Kwa kiasi fulani ni vyema huduma hizo zikagharamiwa na wananchi na mifuko ya CHF na NHIF na wadau wengine ambao wanashirikiana na serikali katika kuboresha afya za Watanzania.

Mathalani maeneo yenye visiwa ni pamoja na wilayani Mafia sehemu kama Mibulani, Kirongwe, Dagoni, Kilindoni, Kiegeani na Jibondo.

Hata hivyo kuna visiwa vingine katika maziwa kama Victoria ambavyo pia vinahitaji kuhudumia na kusimamiwa ili wananchi watambue jinsi ya kusimamia afya zao wakati huu wa mlipuko na kubainisha iwapo kuna wageni.

Katika kuhamasisha wananchi kujihadhari na wageni ni vyema kuwahusisha maofisa watendaji wa kata wajumbe wa bodi za afya za zahanati, madiwani wa kamati ya afya, wajumbe wa bodi ya afya ya wilaya, wenyeviti wa serikali za vijiji, viongozi wa dini na asasi za kiraia.

Pamoja na hilo ni vyema kuwajengea uwezo wananchi na kuwashawishi wanavijiji kuhoji matumizi ya fedha na kuboresha ufanisi ili kuboresha hudma za afya kwa kufuatilia rasilimali za umma zinazotumiwa kwenye eneo hilo.

Wananchi ni lazima wahamasishwe kutambua umuhimu wa kujiunga na NHIF ili nayo iwe na uwezo wa kuboresha huduma ili wawe na uhakika wa kupata huduma bora ya afya kwa wakati.

HABARI KITAIFA

# Wanasiasa walivyomlilia Suleiman Khalifa wa CUF

**Na Mary Geofrey**

CHAMA cha Wananchi (CUF), kimemlilia Katibu Mkuu wake, Khalifa Suleiman Khalifa, ambaye amefariki dunia usiku wa kuamkia jana, huku kikieleza kuwa siyo rahisi kumpata kiongozi wa aina yake.

Mwenyekiti wa CUF, Prof. Ibrahim Lipumba, alitoa taarifa ya msiba huo kwa vyombo vya habari jana, na kusema kuwa Khalifa alifariki dunia wakati akipatiwa matibabu ya maradhi ya ini katika Hospitali ya Aga Khan jijini Dar es Salaam.

Alisema chama kimepata pigo kubwa ambalo siyo rahisi kuzibika huku akiwataka wanachama kuendelea kuwa watulivu wakati wakiendelea na maandalizi ya ratiba za maziko ya mpendwa wao.

"Marehemu Khalifa amefariki dunia akiwa katika Hospitali ya Aga Khan alipokuwa akipatiwa matibabu kutokana kwa matatizo ya ini.

Kwa hakika chama kimepata pigo kubwa na marehemu ameacha pengo ambalo haliwezi kuzibika kirahisi," alisema Prof. Lipumba.

Alisema CUF inatoa pole kwa familia ya Khalifa, ndugu na jamaa wote walioguswa na msiba huo mzito na kumuomba Mungu awape subira na uvumilivu katika kipindi hiki kigumu.

"Allah aiweke roho ya marehemu mahala pema peponi. Aamin. Tutafahamishana rasmi juu ya ratiba ya maziko kadri tutakavyopata taarifa kutoka kwa familia ya marehemu," alisema Prof. Lipumba.

Khalifa ambaye alikuwa ni Mbunge wa zamani wa Jimbo la Gambo, Pemba kuanzia mwaka 1995 hadi 2015.

Khalifa alitangazwa rasmi Machi 16, mwaka jana kushika nafasi ya ukatibu mkuu iliyokuwa inashikiliwa na Maalim Seif Sharif Hamad, ambaye kwa sasa ni Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo.

CHADEMA, ACT WAMLILIA

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kupitia Katibu Mkuu wake, John Mnyika, kimetuma salama za rambirambi kufuatia msiba wa katibu mkuu huyo.

Mnyika alisema walipokea taarifa hizo kwa masikitiko na kwamba ni pigo kubwa kwa familia yake, viongozi na wanachana wa chama cha CUF.

"Nilifanya naye kazi alipokuwa mbunge, wakati naingia yeye alikuwa mmoja wa wabunge wa muda mrefu akiwa anawakilisha Jimbo la Gando, Zanzibar tangu 1995. Tunatoa pole zetu za dhati kwa familia ya marehemu Khalifa kwa msiba mzito," alisema Myika.

Naye Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alituma salamu za rambirambi kwa ndugu jamaa na marafiki waliofikwa na msiba huo.

"Nachukua fursa hii pia kuipa pole familia ya ndugu Khalifa kwa kuondokewa na nguzo muhimu katika familia. ACT-Wazalendo ipo pamoja na CUF na familia ya ndugu Khalifa katika kipindi hiki kigumu," alisema Shaibu.

Wakati huo huo, aliyekuwa Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Salum Shamte (67) aliyefariki dunia juzi katika Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili (MOI), alizikwa jana jijini Dar es Salaam.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula (wa pili kushoto), akiangalia utengenezaji wa madirisha ya alminium, kwa ajili ya kuwekwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mara, alipokwenda kukagua maendeleo ya ujenzi huo, mjini Musoma jana. Kushoto ni Mhandisi wa Ujenzi wa mradi wa hospitali hiyo, Mhandisi Kazoba Wilson. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

## Chadema yataka unafuu bei maji tiba na barakoa

**Na Enock Charles**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimeiomba serikali kushirikiana na wawekezaji kuangalia uwezekano wa kupunguza bei ya maji tiba (Sanitizers) na barakoa.

Hatua hiyo, kwa mujibu wa chama hicho, itawezesha wananchi wengi wa kipato cha chini kununua kwa ajili ya kujikinga na corona.

Akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana Ofisa Habari wa Chadema Kanda ya Pwani, Lyenda Gervas, alisema kwa mujibu wa uchunguzi uliofanywa na chama hicho, katika maduka mbalimbali Jijini Dar es Salaam bei ya vifaa hivyo ni ya ghali, hivyo kuwa kikwazo kwa wananchi wa hali ya chini kununua.

"Jana (juzi) usiku nilikwenda katika duka moja la dawa hapa hapa Dar es Salaam kununua 'sanitizer' (maji tiba) chupa hii ya mililita 250 inauzwa Sh. 10,000 nikamwambia hiyo hela sina akanipa haka kadogo ukikaangalia ni kama mililita 100 au 120 inauzwa Sh. 7,500. Nani ataweza?" Alisema Lyenda.

Alisema serikali inaweza kuwekeza katika vitakasa mikono hivyo kwa kuwaondolea kodi au kuwapelekea mahitaji muhimu yanayohitajika katika utengenezwaji wa vifaa hivyo ili viuzwe kwa bei nafuu na kununuliwa na wananchi.

Akizungumzia kuhusu usafiri wa umma hasa daladala na mabasi ya mwendokasi, alisema bado katika usafiri huo watu hujazana sana na kukosekana nafasi kati ya mtu mmoja na mwingine jambo ambalo linahatarisha usalama wa kiafya kwa abiria katika usafiri huo.

# Ewura yashusha bei ya mafuta

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma ya Nishati na Maji (Ewura) imetangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli nchini zinazoanza kutumika leo.

Kwa mujibu wa taarifa ya Ewura kwa vyombo vya habari jana, bei za jumla na rejareja za mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa yaliyopokelewa nchini kupitia Bandari ya Dar es Salaam zimepungua ikilinganishwa na toleo lililopita la Machi 4, mwaka huu.

Bei za rejareja za petroli, dizeli na mafuta ya taa zimepungua kwa Sh. 116 kwa lita moja sawa na asilimia 5.28, Sh.165 kwa lita, sawa na asilimia 7.64, Sh. 192 kwa lita, sawa na asilimia 9.14.

Ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za petroli, dizeli na mafuta ya taa zimepungua kwa Sh. 116.02 kwa lita sawa na asilimia 5.58, Sh. 164.05 kwa lita, sawa na asilimia 8.09 na Sh.192.80 kwa lita sawa na asilimia 9.68.

Ewura ilisema bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa yaliyoingizwa nchini kupitia Bandari ya Tanga zimepungua ikilinganishwa na toleo lililopita.

Katika toleo la mwezi huu, bei za rejareja za petroli, dizeli na mafuta ya taa kwa mikoa ya Kaskazini Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara zimepungua kwa Sh. 86 kwa lita, sawa na asilimia 3.89, Sh. 56 kwa lita, sawa na asilimia 2.65 na Sh. 85 kwa lita, sawa na asilimia 4.09.

Bei za jumla za petroli, dizeli na mafuta ya taa zimepungua kwa Sh. 85.39 kwa lita, sawa na asilimia 4.11, Sh.56.11 kwa lita, sawa na asilimia 2.81 na Sh.84.39 kwa lita, sawa na asilimia 4.34.

Ewura ilisema kwa bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya petroli na dizeli katika mikoa ya Kusini Mtwara, Lindi na Ruvuma zenyewe hazitabadilika ikilinganishwa na toleo lililopita.

"Kwa kuwa hakuna mafuta ya taa yaliyopokelewa katika bandari za Mtwara, wamiliki wa vituo vya mafuta katika mikoa hiyo wanashauriwa kununua mafuta hayo kutoka Dar es Salaam, hivyo bei za rejareja za mafuta ya taa kwa mikoa hiyo, zitatokana na gharama za mafuta hayo kutokea Dar es Salaam na kusafirishwa hadi mkoa husika," ilisema taarifa ya Ewura.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la ndani yanatokana na mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la dunia na gharama za usafirishaji.



Mkurugenzi wa Uhusiano kwa Umma wa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), John Wanyancha (kulia), akipokea moja ya kipeperushi chenye ujumbe wa kuelimisha umma juu ya virusi vya ugonjwa wa corona kutoka kwa Zaidan Wilfred, ambaye ni ofisa kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, jijini Dar es Salaam jana, SBL imejitolea kuisaidia serikali kusambaza vipeperushi hivyo nchi nzima. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Upinzani waibana serikali corona

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

KAMBI Rasmi ya Upinzani Bungeni, imeitaka serikali kuwasilisha bungeni taarifa ya kina kuhusu hali ya mlipuko wa virusi vya corona nchini na hatua inazochukua kuwanusuru wananchi.

Vilevile, kambi hiyo imelitaka Bunge kuhakikisha asilimia 15 ya bajeti ya mwaka ujao wa fedha inaelekezwa kwenye mapambano dhidi ya virusi hivyo.

Muda mfupi baada ya kuanza kwa mkutano wa Bunge la Bajeti jijini Dodoma jana na Spika Job Ndugai kutoa taarifa yake kwa wabunge, mawaziri kivuli wawili; Halima Mdee na Mch. Peter Msigwa, walisimama na kuomba kutoa hoja bungeni.

Mdee, Waziri Kivuli wa Fedha na Mipango, ndiye alikuwa wa kwanza kupewa fursa ya kutoa hoja yake bungeni na Mbunge huyo wa Kawe (Chadema), alieleza wasiwasi wake kuhusu wananchi wanaoishi katika mazingira aliyoyaita ya uswazi kwamba wako hatarini zaidi kupata maambukizo ya virusi hivyo kirahisi.

Waziri Kivuli huyo ambaye kitaaluma ni mwanasheria, alisema Bunge limechukua hatua za kuwakinga wabunge na wafanyakazi wake dhidi ya maambukizo hayo, lakini anaona ni muhimu kukawa na hatua zaidi kwa nchi nzima kama ilivyoshauriwa na mabunge mengine duniani.

"Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninaomba hoja hii ya kutaka ufafanuzi, naomba ufafanuzi muhimu kutoka kwenye kiti chako. Katika kipindi hiki cha Bunge kitakachokuwa kinaendelea, nilidhani ni busara serikali kupitia Wizara ya Afya ije itoe taarifa ya kina humu bungeni, suala la corona Tanzania hali ikoje, 'measures' (hatua) zinazochukuliwa.

"Mheshimiwa Spika, unasema 'social distancing' (kujiweka mbali kijamii), lakini hii kule uswazi kuanzia kwenye daladala, kwenye mwendokasi ni 'crisis' (janga). Kwanini serikali isitenge hata asilimia 15 ya bajeti nzima ili corona idhibitiwe?

"Leo wabunge tunalazimika tusambazwe kwenye kumbi mbalimbali huko, lakini kwanini tusipimwe wote ili ijulikane Halima ana corona, niwekwe karantini ili wabaki watu hapa wafanye kazi?

"Kama Marekani - dunia ya kwanza inatapatapa, kama Italia - dunia ya kwanza inatapatapa, kama Uhispania - dunia ya kwanza inatapatapa, tulipatie nafasi tujadiliane, tuokoe taifa letu," alisihi.

Baada ya maelezo hayo ya Mdee, Spika Ndugai alitoa nafasi kwa Mch. Msigwa, Waziri Kivuli wa Mambo ya Nje, ambaye aliungana na Mdee kutaka itolewe taarifa ya kina bungeni kuhusu hali ya ugonjwa wa corona nchini na hatua zinazochukuliwa kuudhibiti.

"Corona ni vita ambayo sisi kama taifa ni lazima tushirikiane kwa pamoja kupambana na tatizo hili. Wabunge tunaweza kujitahidi hapa bungeni tukaweka hiyo 'social distancing', lakini mazingira ya huko nyumbani ni janga.

"Hili tulichukue kama wabunge tujadili. Hili si suala la ugonjwa tu, kimsingi kiuchumi tumeathirika vibaya kipindi hiki, kwenye utalii huko usiseme. Serikali ije ituambie mipango gani kama wananchi njia gani tutapita ili kwa pamoja tujikwamue katika tatizo hili," alisema Mbunge huyo wa Iringa Mjini (Chadema).

### SPIKA ATAKA UMOJA

Akiwajibu wabunge hao, Spika Ndugai alisema kuna haja mkutano huo wa Bunge la Bajeti kutoa fursa ya kujadiliana na kushauriana kati ya Bunge na serikali.

"Mimi naamini mahali ambako kunapokuwa na tatizo kubwa kama hili, tunapaswa kuwa wamoja na kila mmoja atasikiliza kwa umakini mkubwa kabisa na kuchukua hatua, lazima!

"Kwa hiyo, niwatie moyo wabunge wote, hapa ndio mahali pake na bahati nzuri kesho (leo) tutaanza na hotuba ya bajeti Ofisi ya Waziri Mkuu, ofisi ambayo ndiyo inaratibu mambo yote haya.

"Na corona ni jambo mtambuka, linagusa wizara zote, lakini Kamati yetu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ipo, kama una jambo unalipeleka, moja kwa moja mkalileta kwenye meza ya Spika, kwa Waziri Mkuu, sisi wabunge tuna nafasi ya kufanya hivyo.

"Natambua mifano ya uswazi na kwingine kwamba social distancing ni ndogo, lakini nasisitiza kuwa social distancing ya corona ni muhimu. Maisha ya mwanadamu lazima kuwe na social distancing. Kuna umbali ambao ukiona mtu anauvuka, hukubali.

"Tuwaelimishe wananchi wetu, hata kama ni boti anaona imejaa, aachane nayo asubiri inayofuata. Na tukumbuke hatuwezi kuchukua 'measures' za wazungu 'tuka-zipaste' hapa. Ni ngumu sana, tutaua watu wetu. Lazima tuangalie mazingira yetu ya kitanzania," alionya.

Machi 16 mwaka huu, Tanzania ilithibitisha kuwa na mgonjwa wa kwanza wa corona tangu ugonjwa huo ulipuke barani Asia mwishoni mwa mwaka jana na jana ikathibitisha kutokea kwa kifo cha kwanza cha ugonjwa huo nchini.

# Spika adokeza JPM kuzuru bungeni

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amewasilisha salamu za Rais John Magufuli kwa wabunge na kudokeza kwamba siku yoyote kiongozi huyo wa nchi atazuru bungeni.

Aliyasema hayo bungeni jijini Dodoma jana alipowasilisha taarifa yake kwa wabunge katika siku ya kwanza ya Bunge la Bajeti.

Alisema Rais Magufuli anawasalimu wabunge na yuko pamoja nao wawakilishi hao wa wananchi katika utekelezaji wa majukumu yao muhimu ya kitaifa.

"Rais yupo nasi hatua kwa hatua, na kama mnavyojua siku ya mwisho atakuja kuzungumza nasi na msishangae siku yoyote katikati hapa, siku moja tukawa naye katika mazingira haya," alisema.

Spika Ndugai pia aliliarifu Bunge kuwa Rais Magufuli ametoa kibali kwa miswada miwili kuwa sheria, ambayo ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho Mbalimbali Na. 8 wa Mwaka 2019 na Muswada wa Sheria ya Usuluhishi wa Mwaka 2020.

### RIPOTI YA CAG

Vilevile, kiongozi huyo wa Bunge alizitaka kamati za chombo hicho kushughulikia haraka hoja zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa kuwa mwaka huu ni wa kalenda ya Uchaguzi Mkuu.

Kwa kuwa hakutakuwa na mkutano mwingine wa Bunge la 11 baada ya mkutano huu kumalizika Juni 30, mwaka huu, ni vyema kamati husika zikashughulikia hoja zote za CAG ndani ya kipindi hiki cha miezi mitatu ya Bunge la Bajeti.

Kwa mujibu wa kanuni za Bunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) na ile ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) ndiyo zenye wajibu wa kushughulikia hoja zinazoibuliwa katika ripoti za CAG na ripoti ya ushughulikiaji wa hoja hizo hutolewa wakati wa mkutano wa Januari.

Spika Ndugai alizitaka mamlaka za serikali kuhakikisha zinaandaa majibu ya hoja za CAG na kuziwasilisha kwa CAG kwanza ili baadaye zishughulikiwe na kamati hizo za Bunge.

Mbunge huyo wa Kongwa pia aliwakumbusha wabunge umuhimu wa kuepuka msongamano katika kipindi hiki ambacho dunia inakabiliwa na baa la mlipuko wa virusi vya corona, akirejea hatua mbalimbali zilizochukuliwa na serikali na Bunge.

Aliwataka wabunge kuzingatia maelekezo yote yaliyotolewa na wataalamu wa afya kujinga dhidi ya ugonjwa huo, akishauri hata huduma ya chakula kwenye kantini ya Bunge iangaliwe upya ili kusiwe na mkusanyiko mkubwa wa watu katika eneo hilo.

"Social distance (kujiweka mbali kijamii) ni kitu cha kawaida katika maisha ya mwanadamu. Hata mnyama ana 'social distance'. Wewe hapo ukikutana na mkweo, mkwe wako, huwezi kuegemeana naye, kuna social distance," alisema.

# Waliolipwa fidia kupisha mradi maji waamriwa kuondoka

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

WAKAZI wa Solwa Wilaya ya Shinyanga, ambao wamejenga nyumba zao kwenye bomba la mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria, wameamriwa kuondoka eneo hilo baada ya kulipwa fidia.

Serikali imewataka kuondoka mara moja, vinginevyo itatumia nguvu kuwaondoa.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, alipokwenda kuutatua mgogoro huo kwa kuzungumza na baadhi ya wananchi, ambao waligoma kuondoka kwenye hifadhi ya bomba hilo wakati walishalipwa fidia.

Alisema wananchi kuendelea kuishi kwenye hifadhi ya bomba la mradi huo maji kutoka Ziwa Victoria ni kuhatarisha maisha yao pamoja na kuhujumu uchumi, hivyo wale ambao walishalipwa fidia wanapaswa kuondoka maeneo hayo kabla ya serikali haijatumia nguvu.

"Mimi sipendi siasa kwenye masuala ya maendeleo, yaani mtu umeshalipwa fidia na fedha umechukua ili uondoke kwenye bomba kubwa la mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria, lakini hutaki, hivyo naagiza mwondoke haraka sana kabla ya serikali kutumia nguvu," alisema Moneko.

"Mnafahamu kabisa nini kitatokea endapo serikali ikitumia nguvu...tutaharibu mali zenu kwa sababu mtambo ukija wenyewe ni kubomoa tu nyumba bila ya kujali kuna nini ndani, mwisho wa siku mnaanza kuilaumu serikali, na mimi sitaki tufike huko, hivyo maagizo yangu mwondoke haraka sana," aliongeza.

Pia aliagiza Mamlaka ya Maji ambayo inazalisha maji kutoka Ziwa Victoria na kusambaza mkoani Shinyanga (KASHWASA), kurudi kupima upya maeneo ambayo yapo kwenye hifadhi ya bomba la maji pamoja na kuwalipa fidia, ili wapishe.

Mmoja wa wakazi wanaoishi kwenye hifadhi ya bomba la mradi huo Ziwa Victoria, Kuyela Kulwa, alisema wapo tayari kuondoka kwenye maeneo yao, na kudai kuna nyumba ya serikali ambayo nayo ililipwa fidia, lakini mpaka sasa haijabomolewa, jambo ambalo linakwamisha na wao kuondoka.

Naye Jeremia Kulwa, alisema awali alipopimiwa nyumba yake aliambiwa yupo mbali na bomba hilo, lakini ameshangaa kuingizwa kwenye orodha ya waliogoma kuondoka, na kuomba akapimiwe upya na kama yupo eneo la mradi huo yupo tayari kulipwa fidia na kuondoka.

Mkurugenzi wa Kashwasa mkoani Shinyanga, Mhandisi Joshua Mgeyeka, alisema watu hao walishawalipa fidia ili kuondoka, lakini waligoma, huku wakiahidi kurudi kwenda kupima upya maeneo yote ambayo yapo kwenye bomba la mradi huo.

# Kliniki 10 za mifugo sasa kujengwa kwenye h/shauri

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

KATIKA mwaka wa fedha wa 2020/21, serikali imejipanga kujenga kliniki za mifugo 10 kwenye halmashauri mbalimbali nchini ikiwamo Singida Vijijini.

Hayo yalibainishwa jana bungeni katika majibu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika swali la Mbunge wa Singida Kaskazini(CCM), Justine Monko.

Katika swali lake, mbunge huyo alitaka kujua mpango wa serikali wa kuongeza wataalamu ama vitendea kazi kama njia mbadala ya kuwasaidia wataalamu wachache waliopo kutoa huduma bora kwa wafugaji.

"Ni lini serikali itajenga maabara za mifugo katika maeneo ya wafugaji ili wananchi waache kutibu mifugo kwa kubahatisha?" Alihoji.

Monko alisema mifugo ya wafugaji wakubwa nchini imekosa ubora wa mazao yake kutokana na maradhi yanayochangiwa na kukosekana kwa wataalamu waliobobea katika fani na kukosa maabara za mifugo.

"Je, ni lini serikali itajenga maabara za mifugo katika maeneo ya wafugaji?" Alihoji Monko.

Kwa muhibu wa majibu yaliyotolewa na Wizara ya Mifugo, serikali inaendelea na mpango wa ujenzi wa maabara za mifugo kwenye kila mkoa.

"Mpaka sasa kuna maabara za mifugo za serikali 11 kwenye kila kanda," alisema.

Aidha, wizara imeshavielekeza vituo binafsi 1,709 vya kutolea huduma ya afya ya mifugo vilivyopo kwenye halmashauri zote 185 kuhakikisha vinakuwa na maabara ndogo kwa ajili ya kutoa huduma ya uchunguzi wa awali wa magonjwa ya mifugo.

Pia inafanya juhudi za kuongeza idadi ya maofisa ugani wa mifugo kwa kuiwezesha Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA) kuongeza udahili wa wanafunzi wa ngazi ya astashahada na stashahada katika fani za uzalishaji, afya ya mifugo, nyanda za malisho na maabara.

Wizara hiyo ilibainisha kuwa wanafunzi hao wameongezeka kutoka wanafunzi 2,536 mwaka 2018/2019 hadi mwanafunzi 3,634 mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la wanafunzi 1,098.



Kaimu Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti wa Michikichi (Tari Kihinga), kilichopo mkoani Kigoma, Dk. Filson Kagimbo (kulia), akitoa maelezo kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Tari, Dk. Yohana Budeba (katikati), kuhusu uzalishaji wa miche ya michikichi unaofanywa na kituo hicho, mkoani humo juzi. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa Tari, Dk. Geofrey Mkamilo. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Afa kwa kupigwa na radi akitoka shambani

**Na Neema Hussein, KATAVI**

MTU mmoja aliyefahamika kwa jina Paulo Chundu (27), amefariki dunia baada ya kupigwa na radi akiwa anatoka shambani.

Tukio hilo lilitokea Machi 29, mwaka huu majira ya jioni katika mbuga za Kalilankulukulu Kata ya Kabungu wilayani Tanganyika mkoani Katavi.

Kamanda wa Polisi mkoni Katavi, Benjamin Kuzaga, alisema Chundu alikutwa na umauti akiwa katika mbuga hiyo akiendesha pikipiki kutokea katika Kijiji cha Ikaka akielekea nyumbani kwake.

John Laurent, baba mdogo wa Chundu, alisema alimtuma mwanawe shambani kupeleka mtu wa kufanya kazi za shambani, na kwamba alipokuwa akirudi ndipo mauti yalimkuta.

"Ni mwanangu, niliachiwa na kaka yangu alipofariki...nimekuwa naye tangu akiwa mdogo," alisema.

Magreti Michael mama mdogo wa Chundu, alisema siku hiyo hawakupata taarifa yoyote juu ya kifo chake ila walikuwa wakishangaa kwanini hajarudi nyumbani hadi usiku, na kwamba taarifa walizipata siku ya pili wakiambiwa kuwa kuna mtu amepata ajali ya pikipiki.

"Sikulala kabisa hiyo siku aliyoondoka kwenda shambani halafu hakurudi niliwaza sana, kulipokucha kuna mtu akanipigia simu akaniambia kuna mtu amepata ajali ya pikipiki," alisema na kuongeza:

"Nikamwambia mbona mi mwanangu sio bodaboda, akasema mwili wake upo hospitali, ikabidi nipige simu hospitali."

Siku chache zilizopita, liliripotiwa tukio lingine la mwanafunzi kufariki dunia kwa kupigwa na radi katika Mkoa wa Katavi.

# Upembuzi yakinifu maji Mto Ruvuma wakamilika

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

BUNGE limeelezwa kuwa serikali imekamilisha upembuzi yakinifu wa mradi wa kutoa maji katika chanzo cha maji cha Mto Ruvuma kwa ajili ya kutatua tatizo la maji kwa wakazi wa Mkoa wa Mtwara.

Hayo yalielezwa jana bungeni na katika majibu yaliyotolewa na Wizara ya Maji, katika swali la Mbunge wa Mtwara Vijijini (CCM), Hawa Ghasia.

Katika swali lake, Ghasia alisema tatizo la maji kwa Mkoa wa Mtwara limeendelea kuwa kero kubwa kwa wananchi wa mkoa huo.

"Je, mradi wa kutoa maji Mto Ruvuma hadi Mtwara Manispaa umefikia hatua gani?, Je, ni lini serikali itapeleka fedha za ukarabati wa mradi wa maji wa Mbuo Nkunwa? Je, ni nini hatuma ya mradi wa maji Makonde?" Alihoji.

Kwa mujibu wa majibu ya wizara hiyo, kwa sasa serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuajiri mtaalamu atakayefanya usanifu wa kina na kuandaa makabrasha kwa ajili ya kuanza utekelezaji katika mwaka wa fedha 2020/21.

"Mradi huu ni mkubwa ukitekelezwa utakuwa mkombozi mkubwa kwa wananchi wa Mkoa wa Mtwara," ilisema wizara hiyo.

Aidha, ilisema ukarabati wa mradi wa maji Mbuo- Nkunwa unaendelea kufanyika na mkandarasi anaendelea na kazi.

"Mpaka sasa bomba la njia kuu lenye urefu wa kilomita 3.6 limelazwa na wananchi wanaendelea kupata huduma ya maji," ilisema.

Pia ilisema mkandarasi amechimba kisima kingine kipya ili kuongeza kiasi cha maji, kazi ya kufunga miundombinu ya bomba la mtandao wa maji inaendelea.

"Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Aprili 2020, usimamizi wa mradi huu unafanywa na wataalamu wa ndani wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mtwara (Mtuwasa)," ilisema.

Kwa upande wa mradi wa Makonde, ilisema serikali imepanga kufanya ukarabati kwa awamu na awamu ya kwanza ya ukarabati inaendelea, tayari njia ya bomba kuu yenye urefu wa kilomita 17 kutoka chanzo cha maji Mitema hadi mjini Newala imekamilika.

"Kazi ya ufungaji wa pampu inaendelea ili majaribio ya mradi yafanyike kwa ajili ya mji wa Newala, aidha, katika awamu hii upo mpango wa kuongeza njia nyingine kubwa kutokea Mitema hadi eneo la Nambuga ambapo tangi lenye uwezo wa lita milioni tano litajengwa na maji yatasambazwa katika Mji wa Newala na vijiji jirani," ilisema.

Iliongeza: "Awamu ya pili itahusisha ukarabati wa mtandao wa mabomba katika eneo la Tandahimba ili kutoa huduma ya maji ya uhakika."



Spika wa Bunge, Job Ndugai, akiongoza Bunge la 11 Mkutano wa 19 kikao cha kwanza kilichoanza Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: BUNGE**

## Kituo cha afya kuwa hospitali ya halmashauri

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), imesema kuwa inakamilisha taratibu za kukipandisha hadhi Kituo cha Afya Bwisya kilichopo kwenye kisiwa cha Ukara ili kiwe na hadhi ya hospitali ya halmashauri.

Majibu hayo yalitolewa katika swali lililoulizwa la Mbunge wa Ukerewe (CCM), Joseph Mkundi, ambaye alisema kituo hicho cha afya kimekarabatiwa na kuongezewa miundombinu muhimu kufikia kiwango cha hospitali.

Alihoji ni kwanini serikali isipitishe hadhi kituo hicho na kuwa hospitali ili kuimarisha utoaji wa huduma za afya kwa wakazi wa visiwa vya Ukerewe.

Katika majibu ya ofisi hiyo, yalisema kuanzia Julai 2017 hadi Machi mwaka huu, serikali imetoa kiasi cha Sh.milioni 800 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya Bwisya na Muriti.

"Rais John Magufuli alielekeza baadhi ya kiasi cha fedha za maafa kwa ajili ya kivuko cha Ukerewe kiasi cha Sh. milioni 860 zitumike kupanua na kuboresha kituo hicho cha afua, hivyo kituo hicho kimejengwa na kukarabatiwa kwa jumla ya Sh. bilioni 1.26, serikali inakamilisha taratibu za kukipandisha hadhi ili kiwe na hadhi ya hospitali ya halmashauri.

**"Rais John Magufuli alielekeza baadhi ya kiasi cha fedha za maafa kwa ajili ya kivuko cha Ukerewe kiasi cha Sh. milioni 860 zitumike kupanua na kuboresha kituo hicho cha afua, hivyo kituo hicho kimejengwa na kukarabatiwa kwa jumla ya Sh. bilioni 1.26, serikali inakamilisha taratibu za kukipandisha hadhi ili kiwe na hadhi ya hospitali...**




Habari na Augusta Njoji

# Mbunge ahoji washirika maendeleo kutoleta fedha

MBUNGE wa Momba (Chadema), David Silinde, amehoji sababu za wahisani na washirika wa maendeleo kushindwa kuleta misaada na ahadi kwenye utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kwa wakati.

Akiuliza swali bungeni jana, Silinde alisema katika kipindi cha miaka mitatu ya fedha mfululizo iliyopita ya 2016/17, 2017/18, 2018/19 wameshindwa kuleta ahadi zao.

Katika jibu lililotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango, ilisema si kweli kuwa kuna nyakati nyingine washirika wa maendeleo wamekuwa hawatimizi ahadi zao.

Ilisema kuwa serikali imekuwa ikishirikiana na nchi wahisani pamoja na washirika wa maendeleo katika kutekeleza bajeti yake kwa kupokea fedha za bajeti ya maendeleo kupitia misaada na mikopo nafuu kwa mujibu wa makubaliano ya kimkataba.

"Kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo washirika wa maendeleo wamekuwa wakitimiza ahadi zao kwa wastani wa zaidi ya asilimia 77 kwa mtiririko," ilisema.

Ilieleza kuwa mtiririko huo ni pamoja na mwaka 2016/17 kiasi kilichopokelewa kilikuwa ni Sh. trilioni 3.351 sawa na asilimia 84 ya lengo la kipindi hicho la kupokea Sh. trilioni 3.971.

Iliongeza kuwa kipindi cha mwaka 2018/19 kiasi kilichopokelewa kilikuwa Sh. trilioni 2.082 sawa na asilimia 78 ya lengo la kipindi hicho la kupokea Sh. trilioni 2.676.

"Katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Februari 2020 fedha za misaada na mikopo nafuu zilizopokelewa kutoka kwa washirika wa maendeleo zimefikia jumla ya Sh. trilioni 1.631 sawa na asilimia 90 ya lengo la kipindi hicho," ilisema.

# Wenye mahitaji maalumu wakatiwa bima

**Na Allan Isack, ARUSHA**

WATOTO wenye mahitaji maalumu kutoka katika vituo mbalimbali vya kulelea watoto yatima jijini hapa, wamekabidhiwa kadi za bima ya afya 20, kwa lengo la kuwarahisishia upatikanaji wa huduma za afya bila malipo.

Akizungumza wakati wa kukabidhi kadi hizo, Msemaji wa Kundi la Friends of Batuli, Batuli Kisaya, alisema wamegawa kadi hizo, kwa ajili ya kuboresha mazingira ya upatikanaji wa huduma za afya kwa watoto wenye mahitaji maalumu.

Alisema kadi hizo wamezitoa kwa watoto yatima, wenye ulemavu na wale wanaotoka katika mazingira magumu, kutoka kwenye vituo mbalimbali vya kulelea watoto wenye mahitaji maalumu jijini Arusha.

Vile vile, alisema kundi hilo walichangishana Sh. 1,000,000 ambazo walizitumia kukata kadi za matibabu ya watoto hao.

"Kupitia kikundi chetu tulichangishana na kupata fedha kiasi cha Sh. 1,000,000 na fedha hizo tumezitumia kukata kadi za watoto wenye mahitaji maalumu na wazee, hivyo tunaiomba jamii kujitolea kusaidia makundi haya bila kukata tamaa," alisema Batuli.

Alisema, licha ya kutoa kadi kwa watoto hao na wazee, pia wametoa msaada wa vyakula, ikiwamo mahindi gunia moja, mafuta ndoo ndogo ya kupikia, katoni moja ya sabuni ya kufulia na maji ya kunywa katoni tatu kwa wazee saba kutoka katika kituo cha Herototo kilichopo kata ya Moshono.

Mgeni rasmi katika shughuli hiyo alikuwa mfanyabiashara maarufu jijini Arusha, Filemon Mollel.

Alitoa rai kwa jamii kuwa mstari wa mbele kuwasaidia watu wanapopatwa na matatizo bila kujali hali zao za kimaisha, dini na kabila.

"Siri ya mafanikio katika maisha ni kuwasaidia watu wenye matatizo na mahitaji maalumu katika jamii, pia sijawahi kuona Mungu akiwaacha bure watu ambao ni watoaji wazuri wa sadaka zaidi amekuwa akiwazidishia maradufu pale watoapo," alisema Mollel.

Ofisa Maendeleo ya Jamii katika Jiji la Arusha, Mather George, alisema Jiji la Arusha kuna wazee 9307, kati ya hao, wazee 3307, wamepewa kada za afya na huduma za afya wanapata bure katika hospitali, vituo vya afya na zahanati mbalimbali za jiji la Arusha.

Kwa upande wa watoto yatima, wenye ulemavu na wenye mahitaji maalumu, alisema wapo 21,000, na wazee wenye ulemavu ni 560, na kuiomba jamii kujitokeza kusaidia makundi hayo kutokana na idadi kubwa ya kundi hilo.

# Askofu ampongeza JPM viongozi dini kuombea taifa

**Na Allan Isack, MANYARA**

ASKOFU mstaafu wa Kanisa la (TAG), Jimbo la Manyara Magharibi, Nicodemus Panga, amempongeza Rais John Magufuli, kwa uamuzi wake wa kuliombea taifa kuondokana na ugonjwa wa corona.

Pia, amewataka viongozi wa dini na wananchi kuendelea kufanya ibada za kuliombea taifa liondokane na ugonjwa wa corona.

Askofu Panga alitoa pongezi hizo, wakati akiwasilisha ujumbe wa Askofu Mkuu wa Kanisa la TAG, Dk. Barnabas Mtokambali.

Alisema kanisa hilo limetenga siku ya Ijumaa ya kila wiki kufanya maombi na kufunga ili kumuomba Mungu kumaliza ugonjwa huo.

"Ndugu zangu kusiwapo na muumini atayepuuzia maelekezo ya serikali na wataalamu wa afya kunawa mikono kwa kuwa tumeweka ndoo za kutosha ili waumini wanawe," alisema Panga.

Alisema nchi yoyote duniani kama kiongozi wake amemtanguliza Mungu kwenye jambo lolote, taifa hilo litakuwa salama kwa kuwa Mungu analipigania.

Alisema maelekezo aliyotoa Rais John Magufuli ni mtihani mkubwa kwa waumini wa dini zote, hivyo hawapaswi kwenda kinyume na maelekezo na kuchukua tahadhari katika nyumba za ibada na shughuli za biashara.

Alisema kuna baadhi ya nchi zimechelewa kuchukua tahadhari mapema na zimepata maambukizi kwa kiwango kikubwa.

Aliwataka waumini kumrudia Mungu ili awaepushe na adha ya ugonjwa huo.

"Pamoja na kumuomba Mungu atuepushe na ugonjwa wa corona, tunapaswa kuchukua tahadhari kwa kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya na serikali kujikinga na maambukizi ya virusi hivyo," alisema.



Naibu Waziri wa Uvuvi na Mifugo, Abdallah Ulega (kushoto), akikabidhi vifaa vya kutakasa mikono kwa Mkuu wa Wilaya ya Longido, Franck Mwaisumbe, wilayani humo, mkoani Arusha jana, kwa ajili ya kuweka katika maeneo ya minada ya mifugo, ili kuwakinga wafanyabiashara dhidi ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Mbaroni tuhuma kuomba, kupokea rushwa

**Na Allan Isack, MANYARA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), mkoani Manyara, inawashikilia mawakala watatu wa ushuru katika Halmashauri za Wilaya ya Babati kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa.

Mkuu wa Takukuru wa Mkoa wa Manyara, Holle Makungu, akizungumza na waandishi wa habari juzi, alisema mawakala hao, walikamatwa Machi 29, mwaka huu, katika baa moja wakiwa wanakunywa pombe.

Aliwataja mawakala hao kuwa ni Iddi Sulle na Ezekiel Samwel.

Alisema mawakala hao, wanadaiwa kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 120,000 ili kutoa kibali cha kusafirisha mazao kutoka mkoani Singida kwenda jijini Arusha.

Alisema mawakala hao walimsimamisha mfanyabiashara Elias Umbu, katika kituo cha Sinai mjini akiwa na mazao yake na wakamchukulia nyaraka zake.

"Mfanyabiashara huyo alikuwa na bidhaa ya mchele, vitunguu na viazi mviringo akisafrisha kwenda kuuza jijini Arusha, alitii agizo lao na siku iliyofuata alikwenda kuchukua nyaraka zake," alisema Makungu.

Alifafanua kuwa baada ya kufuata nyaraka hizo, walimwambia awapatie rushwa ya Sh. 120,000 ili watie saini na wamruhusu kuendelea na safari.

Alisema mfanyabiashara huyo, alitoa taarifa kwa Takukuru na waliweka mtego wa kuwakamata.

"Licha ya kucheleweshwa kwa mfanyabiashara huyo kwa sababu za rushwa, pia baadhi ya mazao yake kama vitunguu na viazi vimeharibika hivyo watuhumiwa, pamoja na kufikishwa mahakamani watawajibika kulipia hasara hiyo," alisema.

Alitoa rai kwa wakurugenzi wa halmashauri mkoani humo, kuweka mawakala waadilifu kwenye vizuizi ili kuondoa usumbufu na kudhibiti upotevu wa mapato.

Mfanyabiashara Elias Umbu, alisema mawakala hao, wanapaswa kubadilika na kutambua kuwa nyakati za kuchukua rushwa kwenye mazao zimepitwa na wakati na waridhike na wanachopata.

# Kinapa yachangia bil. 4/- miradi 48

**Na Mary Mosha, MOSHI**

HIFADHI ya Taifa ya Kilimanjaro (Kinapa), imechangia miradi ya maendeleo 48 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 4.4 katika vijiji vinavyozunguka hifadhi hiyo kwa miaka 10.

Taarifa iliyotolewa jana na Kamishna wa Uhifadhi wa Kanda ya Kaskazini wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Herman Batiho, inaeleza kuwa miradi hiyo ni ile inayotokana na mpango wa ujirani mwema.

Katika bajeti ya hifadhi hiyo kwa mwaka 2019/2020, jumla ya miradi 25 yenye thamani ya Sh. milioni 899.5 inaendelea kutekelezwa kwenye vijiji mbalimbali vinavyopakana na mlima huo.

Kwa mujibu wa Batiho, vijiji vilivyonufaika na ujirani mwema ni Mowo, Kokirie, Mahoma, Arisi, Mshiri, Kinyamvuo, Mbahe, Omarini, Kimanganuni na Lyasongoro.

"Mradi huu umelenga kuboresha kiwango cha elimu katika shule hii ambayo ilikuwa na changamoto za upungufu wa madarasa, madawati na ofisi ya walimu, umegharimu Sh. milioni 123.3 ambapo Tanapa imetoa Sh. milioni 120.4 na michango ya wananchi Sh. milioni 2.8," alisema.

Aidha, Kamishna Batiho alisema baadhi ya miradi ni awamu ya pili ya utekelezaji kwa miradi ya mwaka 2018/2019 katika Wilaya ya Moshi, inatekelezwa katika vijiji 10.

"Lengo la Tanapa katika kutekeleza miradi hii ni kutimiza azma yake ya kutoa sehemu ya mapato yake kwa jamii ili wananchi wapate manufaa yatokanayo na shughuli za uhifadhi," alisema.

Kamishna Batiho alisema miradi yote ni matunda ya idara ya ujirani mwema kwani hifadhi hiyo imepakana na vijiji 92 katika wilaya za Hai, Moshi, Rombo, Siha na Longido, pia vimepewa elimu kuhusu hifadhi ya mazingira.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, alitaka viongozi wa vijiji na Kinapa kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira kwa watoto na faida za uwepo wa mlima kwa ajili ya utalii.

Alitaka hifadhi kutoruhusu watoto kuingia msituni kwa ajili ya kuokota kuni kwani kwa kufanya hivyo ni sehemu ya uharibifu wa mazingira na wanaweza kudhurika kwa kuingia humo bila utaratibu.

Mghwira alimtaka Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro (RAS), Dk. Habibu Kazungu kuandaa safari ya kupanda mlima Kilimanjaro kwa ajili ya kubaini matatizo ya mlima huo, lakini kuona maeneo korofi kutafuta ufumbuzi.

Pia, safari hiyo itatoa fursa ya kutoa maelekezo ya wapi wananchi wasifike na wapi wafike kwa maslahi ya hifadhi ya mazingira.

# W'biashara wavunja makufuli yaliyowekwa na manispaa

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

WAFANYABIASHARA 10 wanaomiliki maduka ya biadhaa mbalimbali kuzunguka kituo kikuu cha mabasi cha Moshi Mjini, wameyavunja makufuli yaliyowekwa mlangoni na maofisa wa manispaa, baada ya kudaiwa kuwa sio wapangaji halali.

Waliokumbwa na mkasa huo ni wafanyabiashara wanaouza bidhaa za nguo, viatu na simu kuzunguka vituo vyote viwili vya mabasi yaendayo mikoani na yanayofanya safari zake ndani ya mkoa wa Kilimanjaro.

Kwa nyakati tofauti jana, wafanyabiashara hao walieleza masikitiko yao baada ya watu wanaodaiwa kuwa askari mgambo wa manispaa hiyo kuendesha zoezi hilo la kuyafunga maduka ya wafanyabiashara wanaodaiwa kuwa sio wapangaji halali.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Irene Charles, alieleza kwamba wananyanyaswa na mgambo wa Manispaa ya Moshi, kwa kuwavamia na kufunga maduka yao, jambo ambalo liliwapa hasira na kulazimika kuvunja kufuli hizo.

"Tulifungua kesi mahakamani kupinga kufungiwa maduka yetu na mahakama ikaturuhusu kuendelea na biashara kama kawaida, lakini cha kustaajabisha mgambo wa Manispaa ya Moshi wamekuwa wakifika katika maduka yetu na kulazimisha kufunga kwa nguvu.

Zaidi Irene aliongeza: "Sisi tunamiliki maduka haya kwa muda mrefu, ni zaidi ya miaka 15 sasa na tumekuwa tukilipa kodi zote na kutambulika na Manispaa ya Moshi, lakini kilichotokea ni madalali kuingilia kukodisha maduka yetu kwa gharama kubwa."

Alisema madalali hao, ndio chanzo cha wao kuyakosa maduka hayo, kwa kuwa zabuni iliyotangazwa ilikuwa ni kubwa na yenye lengo la kuwakwamisha kibiashara.

Akijibu malalamiko hayo, Mkurugenzi wa Manispaa ya Moshi, Michael Mwandezi, alikiri ni kweli wafanyabiashara hao walikuwa na mikataba kati yao na halmashauri, lakini ilishakwisha muda wake na walitangaza zabuni kwa mujibu wa sheria.



Waumini wa Kanisa la TAG, mjini Babati, mkoani Manyara, wakielekezwa na mzee wa kanisa hilo, kunawa mikono mlangoni ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Walalamikia kero sugu ya kukosa umeme

**Na Mwandishi Wetu, SIHA**

WAKAZI wa Kata ya Songu katika Wilaya ya Siha, wamelalamikia kero ya kukosa umeme kwa miaka mingi na kukwama kimaendeleo.

Wakazi hao hawajawahi kupata umeme tangu nchi ilipopata Uhuru mwaka 1961.

Akieleza jana namna wanavyopigania kupata nishati ya umeme, hasa ule unaosambazwa na Wakala wa Umeme Vijijini (Rea), Diwani wa Kata ya Songu, Dawson Ndosi, alisema hali hiyo inasababisha shughuli za kiuchumi kushindwa kufanyika kwa kiwango kinachotakiwa.

"Tunamuomba Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, kusaidiana kuepukana na adha hii ya muda mrefu, atusaidie kutafuta ufumbuzi wa jambo hili, kwa sababu hatujaunganishiwa umeme, hatujui shida iko Rea au Tanesco maana hatuna majibu ya maswali haya," alisema na kuongeza:

"Wananchi wa kata nzima ya Songu, wamekuwa wakisafiri umbali mrefu kila siku na kutumia nauli shilingi 2,000 kwenda kuchaji simu kwa gharama ya shilingi 500 katika Soko la Lawate lililopo Kata ya Kirua, hali hii inawaumiza wananchi wangu."

Alisema wananchi wa kata hiyo wamekuwa wakipata tabu kwa kukosa nishati ya umeme, hivyo kusababisha shughuli za maendeleo kufanyika kwa kutumia gharama kubwa kwa kufuata nishati hiyo, Kata ya Kirua.

Diwani huyo akionyesha hisia zake namna wananchi hao wanavyoumia kwa kukosa nishati hiyo alisema: "Ukiangalia gharama ya kuchaji simu inakuwa ni ndogo kuliko nauli anayotumia mwananchi kufuata umeme katika kata jirani ya Kirua."

Hata hivyo, baadhi ya wakazi wa kata hiyo akiwamo, Omari Mlekwa na Aisha Mbaga kwa nyakati tofauti, walieleza kuwa wanashangazwa na kitendo cha miundo mbinu ya umeme kupita katika makazi yao, lakini hawanufaiki nayo, licha ya viongozi wa serikali akiwamo Waziri wa Nishati kuhimiza vijiji vinavyopitiwa na umeme kuunganishwa na nishati hiyo.

"Tunaumia sana na tunauhitaji wa umeme, hata Rais John Magufuli kwenye vyombo vya habari tulimuona akisisitiza umeme huu kufika nyumba kwa nyumba, hata kama nyumba iwe ya nyasi, sasa tunashangaa! Huu umeme haujafika, tunajiuliza sisi ni kina nani mpaka tukose na sisi tunatamani tuonje huu umeme kwani sisi sio Watanzania?" Alihoji Mlekwa.



Ukurasa 14

**Buriani Khalifa mwanasiasa mwenye msimamo usioyumba**

## Bunge 2015/2020 na alama zisizofutika



Ukurasa 15


# siasa

JUMATANO APRILI 1, 2020

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 19

**Darasa la JPM na utata wa corona uchaguzi mkuu**



Ukurasa 18

**Afrika yaweka vikwazo mataifa ya Magharibi**

# Corona kuamua hatima uchaguzi mkuu 2020

- Ni wa mataifa 19 imo Tanzania, Marekani, Burundi, Niger, Malawi

**Na Maulid Mmbaga**

PAMOJA na janga la mlipuko wa homa ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona -COVID 19, bado mwaka wa 2020, ni msimu ambao umesheheni uchaguzi wa kisiasa katika nchi mbalimbali duniani ikiwamo Tanzania na Marekani.

Viongozi wanaotarajiwa kuchaguliwa kwa Tanzania Oktoba mwaka huu ni pamoja na marais wa Zanzibar na wa Jamhuri ya Muungano, wabunge, wawakilishi na madiwani.

Mbali na suala hilo la uchaguzi, virusi vya corona vimezua taha-

INAENDELEA UK.16



Rais John Magufuli akipiga kura yake. **PICHA: MTANDAO.**

**Rais Congo Brazzaville afariki dunia na corona** Ukurasa 17

# Buriani Khalifa mwanasiasa mwenye msimamo usioyumba




Katibu Mkuu wa CUF, Khalfa Suleiman Khalifa (katikati), enzi za uhai wake. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha Wananchi (CUF), kimepata pigo baada ya kumpoteza Katibu wake Mkuu, Khalifa Suleiman Khalifa, ambaye alifariki dunia usiku wa kuamkia jana, katika Hospitali ya Aga Khan jijini Dar es Salaam.

Katibu huyo ambaye amewahi kuwa Mbunge wa Gando Pemba, kuanzia mwaka 1995 hadi 2015 kupitia chama hicho, alichaguliwa kushika nafasi hiyo Machi 17, mwaka jana.

Hatua ya chama hicho kufanya uchaguzi huo ilikuwa ni kuhitimisha mgogoro wa uongozi ndani ya CUF uliodumu kwa zaidi ya miaka miwili, hasa pale Prof. Ibrahim Lipumba aliporudi kwenye nafasi ya mwenyekiti.

Prof. Lipumba aliacha nafasi hiyo kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, lakini mwaka 2016 akarudi tena kwenye nafasi hiyo na kusababisha mgogoro uliozaa makundi mawili ya wanachama yanayohasimiana.

Kulikuwa na kundi linalomuunga mkono Prof. Lipumba na lingine Maalim Seif Shariff Hamad, hali ambayo ilisababisha mgogoro huo kufikishwa mahakamani na hatimaye upande wa Prof. Lipumba ukaibuka na ushindi.

Katika mgogoro huo, hata baadhi ya viongozi wakiwamo wabunge, waligawanyika, lakini kwa upande wa Khalifa aliendelea kuwa upande wa Prof. Lipumba licha ya kwamba anatoka kisiwa kimoja na Maalim Seif.

> Aliweka wazi kuwa itikadi ya chama chao ya kudai haki kwa watu wote, inawarudisha katika dhamira yao ya msingi, na ndiyo inayofanya wanachama kuendelea kubaki kwenye chama hicho.

Hatimaye Baraza Kuu la Uongozi la CUF liliitisha uchaguzi na kumchagua Khalifa aliyekuwa akitajwa kuwa hasimu wa Katibu Mkuu wa zamani wa chama hicho, Maalim Seif kurithi nafasi hiyo.

Tangu kuchaguliwa, Khalifa amedumu ofisini kwa mwaka mmoja tu na sasa amefariki dunia na nafasi yake kubaki wazi, huku mwenyekiti wa chama hicho, Prof. Lipumba akisema ni pigo kubwa kwa CUF.

## MSIMAMO

Wakati CUF inaingia katika mgogoro wa uongozi na kusababisha hata wabunge kugawanyika, Khalifa hakuyumba licha ya kwamba anatoka kisiwani Pemba ambako ni ngome ya Maalim Seif.

Hata wakati baadhi ya wanachama wakimfuata Maalim Seif alipohamia ACT- Wazalendo, bado aliendelea na msimamo wake wa kutofuata mtu na hatimaye akachaguliwa kuwa katibu mkuu.

Aliamini katika kusimamia taratibu, kanuni, sheria na katiba ya chama badala ya kuwa bendera fuata upepo licha ya kwamba anatoka kisiwa kimoja na Maalim na huenda hali hiyo ilisababisha wakawa mahasimu.

Msimamo wake haukuwa kwenye hilo tu bali hata mambo yanayohusu maslahi ya Zanzibar, alikuwa mstari wa mbele kuyatetea bungeni bila woga wala kigugumizi hadi kukwaruzana na wabunge wenzake.

Iliwahi kutokea kutaka kukunjana na mbunge mmoja nje ya ukumbi wa bunge jijini Dodoma, baada ya mbunge huyo kuwarushia 'madongo' wabunge kutoka visiwani Zanzibar wakati wakijadili maslahi ya muungano.

## MSAMAHA

Pamoja na hayo, Khalifa alikuwa ni mtu anayependa msamaha, kwani hata baada ya kuibuka na ushindi na kuukwaa ukatibu mkuu wa CUF aliwataka wa Baraza Kuu la Uongozi kusameheana.

Wakati wa uhai wake alikaririwa na vyombo vya habari akiwaambia wajumbe kuwa chama kimeshapata uongozi mpya, na sasa wanachama kusameheane na kujenga umoja mpya kwa maendeleo ya chama.

Kwamba CUF kimepita katika mikwaruzo mingi, hivyo wanachama wanatakiwa kuweka ubinadamu mbele kwa kuachana na yaliyopita kwa sababu hayajengi.

Aliweka wazi kuwa wanachama walioondolewa uanachama wao na mkutano mkuu siwezi kuzungumza lolote kwa sababu huo ni uamuzi wa wajumbe wa mkutano mkuu, lakini wengine waliobaki wasameheane.

"Watusamehe na sisi tuwasamehe kwa sababu tumepita kwenye mikwaruzano mikubwa, tumeshambuliana vya kutosha, tumesemana vya kutosha na mimi kwa nafasi yangu napenda kuwaambia wanachama kwamba yaliyopita si ndwele tugange ya jayo kwa maendeleo ya CUF yetu," alihimiza Khalifa enzi ya uhai wake.

Baada ya hapo, Khalifa alianza kazi za chama na kufika katika ofisi zake jijini Dar es Salaam na kukuta zimefungwa kwa muda, lakini akasema pamoja na hali hiyo ataendelea na majukumu yake kama kawaida.

## ITIKADI

Katika uongozi wake aliamini kwamba kuondoka kwa Maalim Seif ndani ya chama na kwenda ACT-Wazalendo ni njia mojawapo ya kuimarika kwa CUF kwa vile ina wanachama wanaoamini itikadi ya chama.

Aliweka wazi kuwa itikadi ya chama chao ya kudai haki kwa watu wote, inawarudisha katika dhamira yao ya msingi, na ndiyo inayofanya wanachama kuendelea kubaki kwenye chama hicho.

Kwamba wanachama wa CUF wamepambana kuhakikisha chama kinaendelea kusimama imara na pia chama hicho kina itikadi yake ya msingi ya kudai haki kwa wote hakuna chama kingine chenye itikadi hiyo.

Khalifa alikuwa akiamini kwamba CUF kinaendelea kuwa imara kwa vile wanachama wanajua chama hicho kimewatoa mbali, na hawana imani nje ya CUF na aliamini hata wale waliokwenda ACT-Wazalendo wangerudi tu.

Katibu huyo na viongozi wenzake walikuwa wakifanya kazi bila kuchoka katika maeneo mbalimbali, kwa ajili ya kuweka sawa wanachama wao ikiwa ni njia ya kuimarisha chama.

UCHAMBUZI

# Bunge 2015/2020 na alama zisizofutika

**Na Mwandishi Wetu**



Profesa Assad aliyetofautiana na Bunge linalomaliza muda wake. **PICHA: MTANDAO**

BUNGE la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lililozinduliwa rasmi na Rais John Magufuli Novemba 20, 2015, linafikia ukomo baada Bunge la Bajeti ambalo limeanza jijini Dodoma jana.

Bunge la Tanzania limeanzishwa kwa mujibu wa ibara ya 62(1) ya katiba, linaishi kwa miaka mitano na kwa muundo lina sehemu mbili ambazo ni Rais na wabunge, wakiwamo wa kuchaguliwa majimboni na wa kuteuliwa.

Bunge la Tanzania linaendeshwa kwa misingi ya Bunge la Jumuiya ya Madola na linafuata mtindo wa bunge hilo kwa kiasi kikubwa, unaeleza mtandao wa Jumuiya ya Madola kwa kiwango kikubwa, inaeleza tovuti ya bunge.

**UHAI WA BUNGE**

Ibara ya 65 ya katiba inaeleza kuwa maisha ya kila bunge yatakuwa ni miaka mitano, kwa hiyo, maisha ya bunge yanaanza kuhesabiwa tarehe bunge jipya limeitishwa na Rais na kukutana nalo kwa mara ya kwanza baada ya uchaguzi mkuu na kumalizika na huishia tarehe ya kuvunjwa kwa bunge hilo kwa ajili ya kuanza michakato mingine kwa ajili ya uchaguzi mkuu mwingine ambao hufanyika kila Oktoba baada ya miaka mitano.

Kwa mujibu wa tovuti ya bunge, muhula wa bunge ni vikao mbalimbali vinavyoanzia mkutano wa kwanza wa bunge baada ya kuzinduliwa na vile vinavyoishia linapovunjwa kwa ajili ya matayarisho na michakato ya uchaguzi mkuu mwingine.

Katiba ya Tanzania inaelekeza kuwa baada ya uchaguzi mkuu, Rais ataitisha mkutano wa bunge jipya unaofanyika kabla ya kupita siku saba tangu kutangazwa matokeo ya huo uchaguzi mkuu katika majimbo ya uchaguzi yote isipokuwa katika majimbo yale ambako uchaguzi umefutwa na kufanywa upya.

Aidha, inaelekeza kuwa rais hatakuwa na uwezo wa kulivunja bunge wakati wowote, isipokuwa tu kama bunge limemaliza muda wa uhai wake kwa mujibu wa ibara ya 65 ya katiba, pia linaeleza mambo mengine kadhaa yatakayolazimisha hatua hiyo kuchukuliwa.

Muda wa maisha ya bunge ukimalizika litahesabiwa kuwa limevunjwa kwa mujibu wa ibara ya 65 maisha ya bunge hayawezi kuongezwa, hivyo ukomo wa miaka mitano ukishatimia ndiyo linaondoka.

**UONGOZI**

Bunge linaongozwa na Spika ambaye huchaguliwa na wabunge miongoni mwao au anaweza asiwe mbunge, lakini ni lazima awe mwanachama wa chama kimojawapo ambaye atapitishwa na chama chake na mwisho kupigiwa kura na wabunge.

Kwa mujibu wa kanuni ya 22 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, Rais ndiye huliitisha bunge jipya na kwa bunge hili linalomaliza maisha yake Rais John Magufuli, aliliitisha Novemba 2019.

Tovuti ya bunge inaeleza kuwa kwa kawaida, bunge la kwanza huanza mnamo mwezi Oktoba baada ya uchaguzi mkuu.

**MKUTANO WA BUNGE**

Mara nyingi kumekuwa na kuchanganya kati ya vikao na mikutano ya bunge, hivyo ni vyema kufahamu tofauti ambazo ni kuwa bunge limeundwa na vipindi viitwavyo mikutano ambayo kwa mujibu wa tovuti hiyo, ni mfululizo wa vikao vya bunge, kuanzia kikao cha kwanza hadi cha mwisho. Inaeleza kuwa kuna mikutano 20 katika bunge moja.

> Kwa hiyo kwa wapigakura mkutano unaoendelea bungeni Dodoma ukimalizika wafahamu kuwa ndiyo mwisho wa uhai wa bunge la 2015-2020.

Aidha, inafafanua kuwa kuna mikutano minne katika bunge, ambayo ni mkutano wa kwanza unaoanza kati ya Oktoba hadi Novemba, mwingine ni wa pili unaofanyika kati ya Januari hadi Februari.

Mkutano wa tatu hufanyika kati ya Aprili na Juni na huo ndiyo wa bajeti ambao umeanza wiki hii jijini Dodoma. Si kwa Tanzania peke yao bali hata mataifa mengine ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yanafanya mkutano huo, kipindi hiki.

Mkutano wa nne hufanyika kati ya Agosti na Septemba na hiyo ndiyo ratiba ya bunge kwa mwaka mzima.

Tovuti inaeleza kuwa kikao cha bunge ni kipindi cha siku moja wabunge wanapokutana kwenye kinaanza kwa kusomwa dua ya kuliombea taifa hadi kumalizika kwa kuahirisha bunge kwa siku hiyo na kutangazwa kuwa litaendelea wakati gani. Kanuni ya 29(2), Waziri Mkuu ambaye ndiye Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni hutoa hoja ya kuliahirisha bunge kwa kutaja siku, mahali na saa mkutano unaofuata utaanza.

Kwa hiyo kwa wapigakura mkutano unaoendelea bungeni Dodoma ukimalizika wafahamu kuwa ndiyo mwisho wa uhai wa bunge la 2015-2020.

Wakati litakapovunjwa ni fursa nyingine kwa vyama vya siasa kuteua wagombe, Tume ya Uchaguzi kupokea majina yao, kusikiliza mapingamizi, kuyatolea maamuzi kuwatangaza na watakaoidhinishwa kuanza kampeni za uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 2020.

**YALIYOJIRI 2015-2020**

Ni kipindi kilichoshuhudia wabunge wengi wakihama kutoka upinzani na kujiunga CCM kwa maelezo ya kufurahishwa na utendaji bora wa serikali ya Rais John Magufuli na kujiaminisha kuwa yale waliyokuwa wakiyapigia kelele yameanza kutekelezwa.

Baadhi ya majimbo ni Kinondoni, Maulidi Mtulia aliyekuwa CUF, mwingine ni mbunge wa Temeke Abdallah Mtolea (CCM) aliyehamia CCM, Aidha, Dk. Mollel aliyekuwa Mbunge wa Siha alijiunga na CCM.

Mbunge mwingine ni Mwita Waitara (Chadema) Ukonga, Julius Kalanga Monduli (Chadema), Chacha Warioba aliyekuwa Serengeti na Pauline Gekuli Babati Mjini.

Hata hivyo, mbunge wa CCM , Lazaro Nyalandu alikihama chama chake na kujiunga na Chadema.

**KUKOSA UBUNGE**

Mbunge wa Singida Mashariki Tundu Lissu, alipigwa risasi kwenye makazi ya wabunge Dodoma na watu wasiojulikana. Hiki kilikuwa ni kisa cha kwanza kwa mbunge kupigwa risasi kwenye maeneo ya bunge.

Mbunge huyo akiwa majeruhi alikwenda Ulaya kwa matibabu lakini ofisi ya Spika ikitangaza kuwa hakuwasiliana na Spika kuomba ruhusa ya matibabu. Aidha, pia hakujaza taarifa za mali na madeni alizotakiwa kuziwasilisha katika ofisi ya maadili ya viongozi. Yote hayo yalimwondoa kwenye nafasi ya ubunge aliyokuwa nayo.

Kwa upande wake, Mbunge wa Arumeru Mashariki (Chadema) Joshua Nassari, naye alipoteza ubunge baada ya kutohudhuria vikao vya bunge kwa muda mrefu bila ya ruhusa ya Spika.

Mbunge huyo wa zamani alitoa maelezo ya kujitetea kuwa alikuwa Marekani kumhudumia mkewe aliyekuwa mgonjwa.

**KUMSUSIA CAG**

Bunge linalomaliza muda wake lilimsusa na kutangaza kutoshirikiana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Profesa Mussa Assad, kwa kile lilikiita kulidharau bunge.

Profesa Assad, aliripotiwa kuwa katika ziara yake nchini Marekani alifanya mahojiano na vyombo vya habari na kueleza kuwa Bunge la Tanzania halina meno.

Kauli yake ilileta utata na mkanganyiko na kulazimisha kuitwa na kuhojiwa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, hata hivyo hakukanusha wala kukana matamshi yake hatua iliyosababisha kuhasimiana na bunge, hadi alipoondoka kwenye nafasi hiyo mwaka jana na wadhifa huo kuchukuliwa na Charles Kicheere.

**WABUNGE KUFUNGWA**

Bunge la 2015-2020 lilishuhudia wabunge kadhaa wakifungwa gerezani. Miongoni mwao ni Mbunge wa Mbeya Mjini Joseph Mbilinyi alihukumiwa kifungo cha miezi sita gerezani wakati Mbunge wa Kilombero, Peter Lijuakili, alihukumiwa pia kufungwa miezi sita.

Mbilinyi au Sugu aliachiwa kwa msamaha wa Rais kwa wafungwa, wakati Lijualikali alishinda rufani.

**KOROSHO KUTIKISA**

Moja ya mjadala uliolitikisha bunge linaloondoka ni hoja ya korosho, wabunge maarufu wa mikoa inayozalisha korosho akiwamo Mbunge wa Mtama, (CCM), Nape Nnauye alichomoa shilingi ya mshahara wa Waziri wa Kilimo wa wakati huo, Dk. Charles Tizeba, akielezea kutokuridhishwa na majibu yake serikali kuhusu fedha za ushuru wa mauzo ya nje ya korosho.

# Corona kuamua hatima uchaguzi 2020

INATOKA UK.13

ruki na kusababisha vifo vya watu wengi takribani 700,000 na kuua zaidi ya 34,000 katika mataifa tofauti duniani, hali iliyosababisha shughuli mbalimbali za kijamii kusitishwa kwa muda ikiwa ni miongoni mwa jitihada za kupambana na kuenea kwa maradhi hayo.

Miongoni mwa shughuli zilizo taarifiwa kusitishwa kwa muda hapa nchini na sehemu nyingine duniani ni pamoja na kusitishwa kwa ligi ya soka, matamasha ya muziki, shule na vyuo vikuu vimefungwa, mikutano na misongamano isiyokuwa na ulazima yote imepigwa marufuku kwa sasa.

Hivyo jambo hilo la kusitishwa kwa mikutano na mikusanyiko mingine ya kijamii linaonekana kuathiri mchakato wa uchaguzi na endapo ugonjwa huo utaendelea kusumbua hadi kufikia nyakati za kufanyika uchaguzi, pengine hakuna mwenye maelezo.

Licha ya serikali Rais John Magufuli kunukuliwa siku chache zilizopita akisema kuwa, "uchaguzi mkuu wa 2020 utafanyika nchini kama ulivyopangwa".

Hali hiyo hata hivyo inatazamwa na wengi kuwa ni suala la kusubiri na kuona hali itakavyokuwa kwani mwelekeo wa corona bado haufahamika pamoja na kwamba Oktoba ni mbali.

Uchaguzi wa Tanzania unatarajiwa kutazamwa zaidi si tu barani Afrika bali na nchi zinginezo duniani ambazo zimekumbwa na ugonjwa huu wa COVID-19.

Katika uchaguzi huo Rais John Magufuli kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) anatarajiwa kuwania tena muhula wa pili kama ambavyo imezoeleka kila baada ya miaka mitano kufanyika uchaguzi mkuu upya.

Kama ilivyo ada katika uchaguzi huo, Rais Magufuli anatarajiwa kukumbana na upinzani kutoka vyama pinzani hapa nchini ambavyo ni Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) ambacho ni chama kikuu cha upinzani, Chama cha Wananchi (CUF), ACT-Wazalendo, NCCR-Mageuzi na vinginevyo vidogo kama Chauma, TADEA, UMD na NRA.

Uchaguzi mkuu wa 2015 Rais Magufuli aliibuka mshindi kwa kupata kura 8,882,935 sawa na asilimia 58.46 huku mpinzani wake Edward Lowassa aliyegombea kupitia muunganiko wa vyama vya upinzani uliobeba jina la Ukawa akipata kura 6,072,848 sawa na asilimia 39,97 ya kura zote.

Kwa sasa Lowassa amesharejea kwenye chama chake kwani kabla hajajiunga na Ukawa alikuwa akitumikia CCM na kuwahimiza wananchi kuendelea kumuunga mkono Rais Magufuli kwa kile anachoeleza kuwa anatekeleza yale yaliyokuwa yakipigiwa kelele kwa kipindi kirefu.

Licha ya kuwapo kwa mageuzi makubwa ambayo yamefanywa na Rais Magufuli lakini bado upinzani umekua wakijinasibu kwa hoja zao ambazo wanaamini kuwa zinawafanya wastahili kuchukua kijiti cha uongozi kwa mwaka huu.

Hiyo inaongeza shauku na chachu ya kutaka kufahamu zaidi kuwa vyama hivyo vya upinzani vitakuwa na mgombea mmoja tena au kila chama kitasimamisha mwakilishi wao chenyewe, hili ni jambo ambalo linaongeza mvuto zaidi katika uchaguzi wa mwaka 2020.




Kubandika picha na majina ya wagombea mbalimbali wa nafasi katika uchaguzi ni michakato inayofanywa ili kuwawezesha wananchi kuwachaguza viongozi. Uchaguzi mkuu wa Tanzania na Mrekani upo kwenye hatihati kutokana na tishio la corona. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> Canada inatarajia kufanya uchaguzi Oktoba 26, wakati Brazili ni Oktoba 25 sambamba.




Rais Trump katika harakati za uchaguzi mkuu wa Marekani wa mwaka 2018.

### UPINZANI LEO

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na mchambuzi wa siasa na utawala bora, Richard Ngaya, ananukuliwa siku chache zilizopita anapohojiwa na baadhi ya vyombo vya habari, anasema, "Siioni Ukawa ya mwaka 2015 katika uchaguzi mkuu ujao, hasa kwa kuzingatia historia ya Zitto Kabwe ambaye ni kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo na Chadema na wakati huu ambao ACT-Wazalendo kilichochukua mtaji wa zamani wa chama cha CUF visiwani Zanzibar".

"Vyama binafsi vinasimama kila chama peke yake ama wakati mwingine vinaunda kambi mbili moja ikiwa na Chadema na nyingine ya ACT-Wazalendo kama kiongozi, huku chama tawala CCM kikipita kiurahisi hata bila kutumia nguvu kubwa," anasema Ngaya.

Aidha, uchaguzi huo ambao pia utaihusisha Zanzibar Rais wa sasa, Ali Mohamed Shein, anatarajiwa kuhitimisha muhula wake wa pili.

CCM kwa Zanzibar inatarajiwa kuja na mgombea mwingine anayechukua nafasi ya Shein.

### MATAIFA JIRANI

Kwa upande wa Afrika Mashariki Burundi pia inatarajia kufanya uchaguzi wake wa rais, ambapo kiongozi anayeliongoza taifa hilo kwa sasa ni Pierre Nkurunziza, ameshatangaza kuachia nafasi hiyo na kumpisha mtu mwingine.

Pamoja na kwamba Mei 17, mwaka 2018 wananchi wa nchi hiyo walipiga kura kuunga mkono marekebisho ya katiba mpya ambayo yangemwezesha kiongozi huyo kusalia madarakani hadi 2034, lakini Rais Nkurunziza wa chama tawala cha CNDD FDD, alinukuliwa hivi karibuni akisema kuwa hataomba kuchaguliwa tena baada ya muhula wake wa sasa kumalizika mwaka huu.

Nkurunziza alitoa kauli hiyo wakati akiidhinisha katiba mpya ya nchi hiyo katika eneo la Bugendana, Gitega.

Aidha, inakadiriwa kuwa karibu watu nusu milioni wamekimbia tangu Nkurunziza ashinde muhula wa tatu wa urais katika uchaguzi uliokuwa na ghasia wa mwaka 2015.

Hata hivyo muungano wa vyama vya upinzani nchini humo umekuwa ukiweka ngumu kwa kiongozi huyo kuendelea kusalia madarakani, ambapo katika uchaguzi wa mwaka 2015 vyama hivyo vya upinzani vilimaliza katika nafasi ya pili.

### MAREKANI

Marekani inatarajia kufanya uchaguzi wake Novemba mwaka huu, ambako Rais Donald Trump, anatarajiwa kuchuana na Joe Bidden kutoka chama cha Democrat.

Canada inatarajia kufanya uchaguzi Oktoba 26, wakati Brazili ni Oktoba 25 sambamba.

### BARANI AFRIKA

Nchi nyingine zinazotarajia kufanya uchaguzi mwaka huu ni pamoja na Burkina Faso ambayo itafanya uchaguzi wa rais pamoja na wabunge Novemba 22.

Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR) nayo inatarajia kufanya uchaguzi wake mwaka huu wa kumpata rais, ni vyema kukumbuka kuwa kwa kipindi kirefu CAR imekuwa ikiandamwa na vita.

Misri pia inatarajiwa kufanya uchaguzi wa wawakilishi Mei wakati Malawi itafanya uchaguzi wake wa marudio Julai 2 mwaka huu, baada ya Mahakama Kuu kufutilia mbali ule uliofanyika mwaka jana.

Taifa jingine ni Ethiopia utafanyika Agosti 29, na Ghana inatarajia kufanya uchaguzi wa rais na wabunge Desemba mwaka huu.

Ivory Coast itafanya uchaguzi wa Rais Oktoba 31 mwaka huu, Mali utafanyika Mei kuwachagua wabunge na Namibia inatarajiwa kufanya uchaguzi mkuu Novemba.

Pia kuna Niger Desemba 27, Senegal Desemba pia wakati visiwa vya Ushelisheli nao uchaguzi mkuu wa rais na wabunge utafanyika mwaka huu.

Chaguzi hizo zitatazamwa zaidi kwani kwa nchi kama Ivory Coast imeshuhudia namna ambavyo uchaguzi wake umekuwa ukileta mvutano.

> Ndani ya bara la Ulaya nchi zinazotarajia kufanya uchaguzi kwa kipindi hiki ni Hispania Aprili 5, na Ureno.

### BARANI ASIA

Bara la Asia mataifa kadhaa yanatarajiwa kufanya uchaguzi kwa kipindi cha hivi karibuni ni Hong Kong na Indonesia Septemba 23, Korea Kusini Aprili 15 na Siri Lanka Aprili 25.

### ULAYA

Ndani ya bara la Ulaya nchi zinazotarajia kufanya uchaguzi kwa kipindi hiki ni Hispania Aprili 5, na Ureno.

### MASHARIKI YA KATI

Mataifa ya Mashariki ya Kati, Syria nayo itafanya uchaguzi Mei 20, Jordan ambayo itafanya chaguzi Septemba.

Hizo ni baadhi ya nchi duniani ambazo zinatarajia kufanya uchaguzi mwaka huu huku zikitazamwa zaidi kutokana na uwepo wa corona unaoweza kusababisha kusimamishwa au kuahirishwa.

## Rais Congo Brazzaville afariki dunia na corona



Rais wa zamani Jacques Joachim Yhombi Opango, aliyefariki nchini Ufaransa. P**ICHA: MTANDAO**

RAIS wa zamani wa Congo-Brazzaville, Jacques Joachim Yhombi Opango, ambaye aliyetawala nchi hiyo kati ya mwaka 1977 na 1979, amefariki dunia akiwa na umri wa miaka 81.

Kifo chake kilielezwa kuwa kilitokea juzi Machi 30 nchini Ufaransa na kwamba alifariki dunia kutokana na ugonjwa wa Covid-19 akiwa na umri wa miaka 81, familia yake ikieleza zaidi.

Hali ya afya ya rais huyo wa zamani wa Congo-Brazzaville ilikuwa imezorota hivi karibuni, na kumlazimu kuishi mbali na nchi yake, nchini Ufaransa hasa, kwa mujibu wa familia yake.

Alikuwa akiishi nchini Ufaransa na Congo-Brazzaville tangu kumalizika kwa muda wake wa kuishi ukimbizini mwaka 2007.

"Baba yangu, rais wa zamani Yhombi Opango, alifariki dunia Jumatatu mchana katika hospitali ya Neuilly-sur-Seine karibu na Paris. Alikuwa mwathirika wa ugonjwa wa corona," mtoto wake Jean-Jacques Yhombi Opango aliliambia shirika la habari la AFP kwa simu.

Taarifa hiyo ilithibitishwa baadaye jioni na televisheni ya serikali ya Congo-Brazzaville, Télé-Congo. Jacques Joachim Yhombi Opango alizaliwa mwaka 1939 huko Cuvette, Kaskazini mwa Congo-Brazzaville. Yhombi Opango, ambaye alikuwa ofisa wa zamani, alichukuwa madaraka mara tu baada ya mauaji ya kuhuzunisha ya Rais Marien Ngouabi.

Jacques Joachim Yhombi Opango aliongoza Congo-Brazzaville kwa miaka miwili tu kabla ya kutimuliwa madarakani na Waziri wake wa Ulinzi, ambaye ni Rais wa sasa Denis Sassou Nguesso, anayetokea katika mkoa wa Cuvette.

Hata hivyo Rais Jacques Joachim Yhombi Opango alikamatwa kufungwa kwa kipindi cha miaka 10, kabla ya kuachiliwa huru muda mfupi kabla ya mkutano wa kitaifa wa mwaka 1991 ambao ulifungua ukurasa mpya kwa nchi kwa kuanzishwa mfumo wa vyama vingi.

Rais wa Congo-Brazzaville Denis Sassou Nguesso, aliyechukua uongozi wa nchi hiyo tangu mwaka 1979 ameendelea kuongoza nchi hiyo kwa muda mrefu na mwaka huu aliteuliwa tena na chama chake cha PCT kuwania urais mwaka 2021.

Uamuzi huu ulifanywa na wajumbe wa chama hicho zaidi ya 2,500 katika mkutano mkuu wa chama hicho.

Nguesso mwenye umri wa miaka 76, amekuwa kiongozi aliyetawala kwa miaka mingi taifa hilo la Afrika ya Kati.

Wakati wa uamuzi huo, wajumbe wa chama hicho walisema kuwa, hatua ya kutaka rais Nguesso kuendelea kuongoza ni kwa sababu wanataka mwendelezo wa maendeleo na mabadiliko ambayo ameleta katika taifa hilo ambalo hata hivyo, wananchi wengi wote ni maskini. **RFI**

TISHIO CORONA

# Afrika yaweka vikwazo mataifa ya Magharibi



Rais wa Afrika ya Kusini, Cyril Ramaphosa, akitangaza hatua za kudhibiti corona, nchi yake ikiwa na idadi kubwa ya wagonjwa barani Afrika. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mashaka Mgeta**

WAKATI takribani watu zaidi ya 600,000 wameambukizwa corona duniani na wengine takribani 30,000 kufariki dunia, hadi sasa takwimu zinaonyesha kuwa Afrika imerekodi idadi ndogo ya maambukizi ya virusi vya COVID - 19 ikilinganishwa na maeneo mengine.

Hata hivyo, serikali kadhaa kwenye mataifa hayo zinaonekana kuchukua hatua madhubuti za kuwezesha kuzuia kuenea kwa virusi hivyo kwenye nchi zao.

Sudan imefunga mipaka yake ya baharini, ardhini na viwanja vya ndege, Msemaji wa Baraza la Uongozi wa Mpito la nchi hiyo, Mohammed Al-Faki Suleiman, anakaririwa akisema. Baraza hilo limetangaza hali ya dharura ya matibabu na kuunda kamati itakayosimamia mipango ya kuzuia kuenea kwa virusi vya corona.

Kamati hiyo itahusika na kuwachukua raia waliozuiliwa mipakani na kuwapeleka kwenye maeneo maalum yenye karantini nchini humo, ambapo hadi makala haya yanaandikwa kulikuwa na mtu mmoja aliyethibitika kuathiriwa na virusi hivyo. Miongoni mwa takwimu rasmi zilizopo ni zile ya Shirika la Afya Duniani (WHO) zinazoonyesha kuwa nchi 27 za Afrika zilikuwa zimethibitisha kuwa na watu 347 waliobainika kuathiriwa na virusi vya corona.

Nchi nne za Misri, Afrika Kusini, Algeria na Morocco zilikuwa na zaidi ya nusu ya idadi ya maambukizi ya virusi hivyo barani Afrika.

Mataifa hayo ukiondoa Afrika Kusini, yametajwa kuwa na ripoti ya watu saba (wa awali ) kufariki kutokana na corona, wanne wakiwa ni Algeria, wawili wa nchini Misri na mmoja wa Morocco.

> Tunazuia usafiri kwa abiria kutoka nchi zilizoathirika zaidi na corona, zikiwamo Italia, Iran, Korea Kusini, Hisipania, Ujerumani, Uingereza na China kuanzia Machi, 18, mwaka huu.

**VIKWAZO VYA KUSAFIRI**

Nchi nyingi za Afrika zinafunga viwanja vya ndege na mipaka ya ardhini ikiwa ni moja ya njia za kudhibiti maambukizi hasa kutoka kwa watu wanaoingia kutokea nchi zenye idadi kubwa ya maambukizi.

Mamia ya safari za ndege zimefutwa, shule na vyuo vimefungwa na abiria hasa kutoka kwa nchi zilizoathirika zaidi kwa corona wamezuiwa ama kwa namna nyingine, kupigwa marufuku kabisa kuingia kwenye baadhi ya nchi barani Afrika.

Kwa mujibu wa chapisho la mtandaoni la Ahram Online la Misri, nchi hiyo inayotajwa kwa kuwa na idadi kubwa ya watu walioathirika na virusi vya corona barani Afrika na imetangaza kufunga viwanja vyake vya ndege nchi nzima kuanzia Alhamisi iliyopita kudhibiti kuenea kwa virusi hivyo.

Takwimu za maambukizi barani Afrika na idadi ya wagonjwa zinaonyesha kuwa wamefikia 126.

Kwa mujibu wa WHO, shule na vyuo vikuu vimefungwa nchini humo kwa takribani wiki mbili.

Nchi nyingine kama Djibouti zilikuwa hazijaripoti tukio la kuwapo mtu aliyethibitika kuambukizwa virusi hivyo, lakini imezuia ndege zote za kimataifa kuingia nchini humo. Hatua za serikali nyingi barani Afrika kuzuia safari za ndege za kimataifa zinaonekana kuungwa mkono kimataifa.

Mchangiaji mmoja kupitia mtandao wa twitter anaandika akipongeza hatua hiyo na kusema, zingechukuliwa na mataifa ya Magharibi kama maambukizi hayo yangeanzia barani Afrika.

"Natumaini nchi za Afrika zifunge mipaka yao kwa nchi zote zilizoathiriwa kwa virusi vya Corona kwa sababu wote tunajua wazi kwamba mataifa ya Magharibi zingezuia wasafiri kutoka Afrika kama mlipuko wa virusi hivyo ungeanzia huko," anaandika.

Afrika Kusini ikiwa miongoni mwa nchi zenye idadi kubwa ya watu waliothibitika kuathirika kwa corona barani Afrika, inatangaza kuzuia wasafiri kutoka nchi zenye maambukizi makubwa duniani.

"Tunazuia usafiri kwa abiria kutoka nchi zilizoathirika zaidi na corona, zikiwamo Italia, Iran, Korea Kusini, Hisipania, Ujerumani, Uingereza na China kuanzia Machi, 18, mwaka huu," Rais Cyril Ramaphosa anatangaza anapolihutubia taifa hivi karibuni.

Ramaphosa anasema nchi hiyo ilimshuhudia mtu wa kwanza kuthibitika kuwa na corona, akitokea Italia.

Kwa msisitizo, Rais Ramaphosa anasema hata viza zilizokuwa zimeshatolewa kwa raia wa mataifa hao waliopanga kwenda Afrika Kusini, zilisitishwa kupitia tamko hilo.

Pia, Ramaphosa anasema hata watu waliowahi kuzitembelea nchi hizo kwa siku 20 hadi kufikia muda ulipotolewa tamko hilo, nao walikosa sifa za kupewa viza za kuingia nchini humo.

Kisha akatangaza kufungwa kwa takribani nusu ya mipaka ya ardhi ya nchi hiyo, shule na mikusanyiko ya watu wanaozidi 100.

**VIKWAZO**

Kupiga marufuku safari na vikwazo vingine kama hivyo vinatajwa kuwa kinyume na ushauri wa WHO iliyoshauri kuwa hakuna sababu ya vikwazo vya usafiri kwa namna inayoweza kuathiri biashara na usafiri.

Ofisa Mtaalamu wa WHO barani Afrika, Dk. Mary Stephen, anakaririwa na shirika la habari la CNN akisema kwamba nchi ambazo awali zililikuwa zinawapima abiria kutoka mataifa yaliyaoathirika zaidi kwa virusi vya corona na kuwaweka kwenye karantini, wameweza kuweka vikwazo kwa sababu ya mshtuko.

"Mlipuko unaenea. Ulikuwa China na sasa ni Italia na nyingi nyingine zinafuata baada ya hapo. Hivyo tunapaswa kuwa makini kwa sababu tumeona ongezeko la nchi zinazozuia safari, na hiyo inamaanisha kuwa fikra kuhusu hatari iliyopo zimebadilika..."

"Lakini wameshafanya tathmini ya athari kwa nchi zao ama kama wanatekeleza tu hatua hizo kwa hisia," anahoji.

Dk. Stephen, mjumbe wa timu ya dharura ya WHO anasema nchi za Afrika zinapaswa kuboresha uwezo wao wa kubaini virusi vya corona mapema, kujitenga na kuwasaka washukiwa wa maambukizi, kuwatibu kwa ufanisi ili kuzuia kuenea kwa virusi hivyo.

Anasema kupima abiria wanapowasili kwenye viwanja vya ndege na mfumo wa uchunguzi wa afya ni njia nzuri kuwatambua na kuwadhibiti abiria wenye dalili za corona.

**MADHARA UTALII**

Nchini Kenya, serikali nayo inaelezea kuzuia kwa safari za abiria kutoka nchi hizo, angalau kwa mwezi mmoja.

Baada ya kutangazwa kwa mtu wa kwanza kuathirika kwa corona nchini humo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utalii wa Kenya, Najib Balala, anasema uchumi wa nchi hiyo 'ungeyumba vibaya' na kwamba sekta ya utalii ingeathirika sana.

Balala anasema Kenya imetenga Shilingi milioni 500 za nchi hiyo (sawa na dola milioni 4.8 za Marekani) kwa ajili ya mahusiano na masoko baada ya zuio la corona.

Nayo Morocco imepitisha zuio la safari kama hizo "mpaka itakapotangazwa baadaye " ikiwa ni njia ya udhibiti wa maambukizi ya virusi vya corona.

Awali nchi hiyo ilipiga marufuku abiria kutoka ama kwenda mataifa ya Ujerumani, Uholanzi, Ureno na Ubelgiji.

Nchini Ghana, ilifikia hatua kama hiyo, huku ikiwa na takwimu za watu sita waliothibitika kuambukizwa corona na ikayaonya mashirika ya ndege kutowapakia abiria wa kigeni zilizothibitika kuwa na watu zaidi ya 200 wenye corona kwa kipindi cha wiki mbili tangu kutolewa kwa tamko hilo.

Akitangaza hatua hiyo kwa video iliyosambazwa kwenye mitandao ya kijamii, Waziri wa Habari za Ghana, Kojo Oppong Nkrumah akasema "safari zote za kuja Ghana zinashauriwa kwa nguvu zote kusitishwa." Naye Rais Nana Akudo-Addo, kwa upande wake akatangaza kufungwa kwa vyuo vikuu vyote na shule katika taifa hilo lililopo Magharibi mwa Afrika.

Pia mikusanyiko ya kijamii, mikutano na huduma za kiroho makanisani vikasitishwa kwa wiki nne.

Nchi nyingine zilizochukua hatua za kufunga vyuo, shule na mikusanyiko barani Afrika ni pamoja na Tanzania, Ethiopia, Senegal na Kenya.

***Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali kwenye mtandao.***

***Maoni: 0754691540***

# Darasa la JPM na utata wa corona uchaguzi mkuu

**Na Ani Jozeni**

MATAYARISHO ya kufanyika uchaguzi mkuu mwishoni mwa mwaka huu yameingia katika sintofahamu kutokana na kusimamishwa shughuli nyingi za kijamii na kiserikali baada ya kuingia katika wasiwasi mkubwa wa homa ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona.

Hakuna mwenye uhakika vizuizi vya shughuli za kawaida nchini vitaondolewa wakati gani, ikiwa ni pamoja na kufunguliwa shule na vyuo, wakati hadhara nyingine ziliruhusiwa kuendelea, kama zile za dini. Hata hivyo, kuna wasiwasi zitafungwa vile vile, endapo idadi ya maambukizi ikiongezeka, kama ilivyo sehemu nyingine duniani.

Endapo shughuli za kawaida za jamii na hasa kuhusiana na mikusanyiko ya aina mbalimbali zitakuwa bado hazijakaa sawa hadi kufikia katikati ya mwaka huu, uwezekano wa kujipanga upya kuendelea na uchaguzi mkuu utakuwa mashakani. Ninavyoona haielekei kuwa Rais John Magufuli anawaza kuwa hadi kufikia Julai corona itakuwa bado tishio na mikusanyiko haipo, lakini si ajabu ameanza kuona huo uwezekano.

Ina maana kuwa uchaguzi ufanyike katika mazingira yoyote yale, nje tu ya hali ya kufungiwa ndani watu wasitoke nje kwa tahadhari ya corona.

Ndiyo sababu ya kusititiza kuwa uchaguzi utakuwapo katika hali yoyote ile, hata kama shughuli za kawaida hazitaanza tena katika mwezi mmoja uliopangwa wa kusikilizia hali ya corona nchini, na kuhamasishana kuhusu tahadhari zinazohitaji kuchukuliwa.

Ingekuwa matazamio hayo yana uhakika, kusingekuwa na haja ya msisitizo kuwa uchaguzi lazima ufanyike, kwani kipindi hiki cha awali cha tahadhari dhidi ya corona hakivurugi chochote katika matayarisho ya uchaguzi mkuu. Labda kwa waliotaka kuharakisha kiasi, hata kwa shari, ikawa tatizo jipya.

Ukisikiliza alichosema JPM unakuwa wasiwasi wake mkubwa ulikuwa siyo hasa katika uwezekano wa mazingira ya afya kitaifa yanayoruhusu maandalizi ya uchaguzi mkuu, ila athari za kushindwa kuendelea na maandalizi, halafu na uchaguzi mkuu wenyewe.

Kwa kile alichokisema, ikiwa itashindikana kufanya maandalizi ya kutosha na halafu uchaguzi mkuu wenyewe, inawezekana shughuli hiyo iahirishwe mwakani, yaani serikali iongezewe mwaka mmoja madarakani. Ndicho alichohofia, kuwa ina maana atakaa madarakani zaidi ya muda wa kikatiba.

Kwa kile anachozungumza, Rais Magufuli anaonekana yuko makini kuhusu muda wake wa kikatiba kama alivyo makini katika utendaji serikalini, kwamba anataka kufanya yote anayoweza kufanya ndani ya kipindi chake ila hatakiongeza hata kwa siku moja.

'Kaa ndani' inayohofiwa kwa siku zinazokuja endapo kutakuwa na ongezeko la maambukizi ya corona, haitawezesha maandalizi ya kawaida ya uchaguzi mkuu, ambao inawezekana ufanyike katika hali ya dharura, si ya kawaida. Hakuna anayetazamia kuwa hadi Oktoba corona itakuwa bado tishio.



Rais John Magufuli katika majukwaa ya kazi. Hivi karibuni amewatoa Watanzania wasiwasi na kuwahakikishia kuwa uchaguzi mkuu wa Oktoba 2020 utafanyika. **PICHA MTANDAO**

> Bila hayo yote kufanyika haiwezekani kuingia katika kampeni, kwani itakuwa kana kwamba watu wanachagua majina ya watu ambao hawajawaona na hawafahamiani nao.

Ina maana kuwa kwa akili au matazamio ya hivi sasa, suala ni matayarisho ya uchaguzi mkuu kwa maana ya watu kuwapo ofisini na kuendesha shughuli kama kupokea majina, kutoa fomu, kupokea, kuzishughulikia na kupata watu wa kusaidia kuhamasisha. Bila hayo yote kufanyika haiwezekani kuingia katika kampeni, kwani itakuwa kana kwamba watu wanachagua majina ya watu ambao hawajawaona na hawafahamiani nao.

Mpigakura anatakiwa amwone mtu akijadili hiki au kile, asikilize na kupima kama ndiye mwelewa bora zaidi, kama ni mkweli kwa yale anayozungumza au kuna walakini.

Nje ya hapo inakuwa ni kama kubahatisha, kwani kitakachokuwa kinajulikana ni chama, na si mgombea halisi.

Ndiyo maana kimantiki unaweza kuruhusu tafsiri ya alichosema JPM kuwa siyo vibaya (Nyerere angesema siyo dhambi) kuchagua vyama badala ya wagombea ambao hawafahamiki, kutokana na kuwapo dharura ya corona.

Ni kusema kuwa lililo baya zaidi ni kutokufanya uchaguzi mwaka huu an kuongeza mwaka mmoja wa utawala kwa serikali, kwani inabidi muhula uishe, uchaguzi ufanyike ndipo muhula mwingine uanze kuhesabiwa, kama ridhaa mpya ya wapigakura.

Hakuna kitu kama kufupisha muhula mwingine kwa mwaka mmoja uchaguzi ukiahirishwa.

Ni somo la katiba ambalo litaanza au limeanza kueleweka, kuwa jambo la msingi katika masuala ya uchaguzi ni ridhaa, na siyo hasa mazingira ya kupatikana kwa ridhaa hiyo. Ni mpangilio wa hisia, hoja au dhana ambao pia unagusa hili suala la kupatikana kwa tume huru ya uchaguzi, na hata katiba mpya kwa baadhi ya hao wanaotaka angalau tume huru ya uchaguzi. Kwa hisia hii kuhusu corona, ambacho kinaleta wasiwasi kuhusu uchaguzi ni mazingira yake, na ambacho hakileti tatizo lolote ni kama katika mazingira hayo ridhaa ya wapigakura itakuwa imetolewa au la.


Ni wazi kuwa itakuwa imetolewa, hivyo serikali itakayoingia madarakani itakuwa halali na yenye ridhaa ya kutosha kusimamia shughuli za nchi, bila kujali ubora wa mazingira ya kufanyika uchaguzi mkuu, vile si lazima yawe yametakata.

Kutokana na muhula wa kwanza wa awamu ya tano kuendeshwa kidharura na sasa wakati wa kutaka kupumua na kufanya siasa za kawaida inaingia hadhari mpya ya corona. Ni kuendelea kuchechemea katika masuala ya siasa baada ya serikali kuona kuna haja ya kuondoa msisimko usio na ulazima wa siasa kwani mengi yanayotawala majukwaa ni juhudi za kufurahisha wasikilizaji na kukwaza juhudi za serikali kubadili taswira ya nchi. Licha ya kuwa demokrasia ni raha, mara kadhaa imekuwa haitofautiani na mzaha; nchi haiwezi kuimarishwa kwa njia hiyo.

Mantiki ni kuwa ugonjwa wa corona ni mtihani mwingine wa kuendesha uchaguzi mkuu baada ya kukaribia kuvuka mtihani wa kutofahamiana kisiasa kutokana na dharura ya kuendesha nchi kwa 'matokeo makubwa sasa.'

Ni kampeni ambayo ilianza wakati wa awamu ya nne ikajikongoja ilivyoweza na kuanza kwa awamu ya tano ikawa ndiyo njia ya kupitisha malengo hayo kwa utaratibu tofauti.

Somo la JPM ni kuwa uchaguzi mkuu ufanyike kwa hali yoyote ile mradi kuchagua kati ya watu wawili kutakuwapo mezani, na suala la kufahamiana kwa undani si muhimu.



Mwonekano wa kirusi cha corona kwenye hadubini. **PICHA: MTANDAO.**

# Corona; kipaumbele ni uhai au kulinda uchumi?

**Na Mwandishi Wetu**

SWALI la msingi linaloulizwa wakati huu wa corona linalostahili kutafakariwa na wengi ni hili la maiti wangapi wanahitajika watoshe kutufanya taifa lichukue hatua dhidi ya maradhi ya corona?

Hili ni swali linaloulizwa wakati huu dunia ikipambana na corona, hoja inayoibuliwa ni hii, je, kipi bora zaidi kati ya kulinda afya ya kila mmoja wetu au kujilinda dhidi ya kuporomoka kwa maendeleo na hali ya uchumi?

Hii ni kwa sababu mataifa mengi yameanza kufikiria kuhusu fedha za kujenga uchumi, lakini kuna giza kuhusu mikakati ya kulinda afya.

Mwandishi wa Idhaa ya Kiswahili ya Sauti ya Ujerumani, Henrick Böhme, anajibu swali hilo kwa kuliangalia kwenye mitizamo ya kifalsafa.

Akisema amewahi kuandika athari za kiuchumi za migogoro ya kila aina kwa miongo kadhaa iliyopita. Baada ya mashambulizi ya Septemba 11 huko Marekani, ameandika pia kilichotokea baada ya kuporomoka kwa kampuni ya Lehman Brothers.

Lehman Brothers ilikuwa kampuni kubwa la fedha duniani nchini Marekani ambayo ilifilisika rasmi mwaka 2008 na kutangazwa kuwa mufilisi, hatua iliyoendeleza changamoto na hali ngumu ya kiuchumi hasa kwenye masoko ya mitaji . Lehman Brothers hapo awali iliwahi kuwa benki kubwa sana nchini Marekani ikishika nafasi ya nne na hata leo kufilisika kwake kumekuwa ni kitendawili kilichoacha maswali mengi.

> Umri wa wagonjwa wetu hospitalini uko juu, huku umri wa wastani ukiwa 67 ikilinganishwa na China ambao umri wao wa wastani ni miaka 47.

Aidha, mwandishi huyo ameshuhudia moja kwa moja jinsi mfumo mzima ulivyoporomoka mwaka 1989, siku hizo ilipokuwa Ujerumani Mashariki.

Lakini sasa, kimekuja hiki kirusi cha corona. Hakionekani. Hakiandikiki. Hakijuilikani. Kipo kimya tu. Huku kutokujulikana kwake ndiko kunakokifanya hatari zaidi. Ndiko kunakowaogofya. Huko ndiko kunakotufanya kuingia kwenye marufuku za kufunga mawasiliano na kuzuia uhuru wetu wa kutembe, na kuufungia kabisa mwenendo wetu wa maisha na, kwa hivyo, uchumi wetu pia. Taswira halisi ya mwisho wa kila kitu ndiyo pengine inayoonekana kutokana na ujio wa corona.

Tunajifunza kuzizoea nambari kubwa zaidi hata kuliko kwenye nyakati za mzozo wa kifedha duniani.

Kitita cha kuokoa uchumi wa nchini Marekani pekee usiangushwe na corona ni dola trilioni mbili, Benki ya Ulaya inaachia Euro bilioni 750, serikali kuu ya shirikisho nchini Ujerumani inaweka Euro bilioni 600.

Vitita hivi vya pesa vinatolewa na serikali kadhaa duniani kuokoa uchumi wao dhidi ya madhara yanayosababishwa na kirusi cha corona.

Na bila shaka, wengi wanauliza ni nani anayepaswa kulipia haya yote?

Hatimaye, si itakuwa yale yale tu yanayojiri kila unapomalizika mzozo mmoja wa kifedha kwa sekta ya umma kujikuta ikiwa umefunikwa na madeni mpaka shingoni?

Ni kwamba michango imekusanywa kutoka akiba iliyowekwa kwenye mifumo ya kijamii, huduma za afya, elimu na uwekezaji.

### HASARA YA UHAI JE?

Kuna utafiti wa uhakika uliofanywa na madaktari nchini Uingereza, ambao ulibaini kwamba watu zaidi ya 500,000 walipoteza maisha kutokana na mzozo wa kifedha wa mwaka 2008 hadi 2010 kutokana na maradhi ya saratani kwa kuwa hawakuweza kupata matibabu yanayostahili.

Hii ilitokea kwa vile hatua za kubana matumizi au ukosefu wa ajira ambao uliwafanya wapoteze dhamana ya kampuni zao za bima.

Kwa hivyo, sasa ni wakati wa kuyatazama tena mambo haya kwenye mizania hapa ni kwa kuhoji maiti wangapi tunataka tuwe nao na tunaoweza kuwahudumia?

Swali hili linaweza pia kuulizwa kwa njia tofauti, kwa mfano maisha ya binadamu yana thamani gani kwetu, kwa serikali na hata ukilinganisha na uchumi?

Je, tunaweza nasi kuuliza, kama anavyofanya Alexander Dibelius - Mkuu wa zamani wa Goldman Sachs nchini Ujerumani - ambaye anahoji: Je, ni kweli kwamba asilimia 10 ya watu ndiyo hasa walio hatarini kuangamizwa na kirusi cha corona, lakini waliosalia, ukiwamo uchumi wote, wako hatarini zaidi kuangushwa vibaya na matokeo mabaya ya kuporomoka kwa uchumi huo kutokana na corona kwa kipindi kirefu kijacho?

Unaweza kuwa na roho ngumu zaidi ya hapo? Au hata kujifanya na mahesabu makubwa zaidi? Juu ya yote, huyu ni daktari kwa taaluma yake.

### VIPI MADAKTARI

Swali jingine ni hili vipi kuhusu kiapo cha maadili ya utabibu? Je, kuna picha za wazi zaidi ya zile zinazotufikia kutoka Italia, ambako madaktari wanakabiliwa na uamuzi wa kikatili kabisa wa kuchagua nani wamtibu na nani wamuachie afe?

Kuzuiliwa mfumo wa huduma za afya kuporomoka kabisa ndilo lengo kuu la marufuku hii ya kutotoka nje iliyowekwa na mataifa kadhaa duniani?

Kwa sababu kama hali ikiendelea kuwa mbaya hivi nchini Italia, kwa mfano, wagonjwa wengi waliolazwa wakiwa na matatizo ya moyo au kiharusi, watalazimika kufa itakuwaje?

### TUJIKUMBUSHE

Corona ilianzia China ilikuwa na idadi kubwa ya maambukizi lakini ni watu 3,274 pekee waliofariki dunia. Hii inamaanisha kwamba asilimia tisa ya maambukizi ya corona ilivyothibitishwa nchini Italia wamefariki, ikilinganishwa na asilimia nne nchini China.

Kwa kiwango hicho Ujerumani, ambayo kufikia sasa imebaini maambukizi 50,871 na vifo 351 ina asilimia 0.5 ya viwango vya vifo.

Profesa Walter Ricciardi, ambaye ni mshauri wa kisayansi wa Wizara ya Afya nchini Italia, anasema vifo nchini humo ni vingi kwa kuwa taifa hilo ndilo lenye watu wazee zaidi duniani mbali na jinsi hospitali zinavyorekodi vifo.

"Umri wa wagonjwa wetu hospitalini uko juu, huku umri wa wastani ukiwa 67 ikilinganishwa na China ambao umri wao wa wastani ni miaka 47," anasema Profesa Ricciardi.

Wagonjwa wengi ni wazee ndiyo maana viwango vya vifo viko juu.

Utafiti mmoja uliofanywa nchini humo ulibaini kwamba asilimia 40 ya maambukizi na asilimia 87 ya vifo nchini humo vimekuwa katika wagonjwa walio na zaidi ya umri wa miaka 70.

Na kulingana na utafiti uliofanywa na taasisi ya Imperial ya jijini London, idadi kubwa ya watu wenye umri huo watahitaji uangalizi wa karibu.

Profesa Ricciardi pia anasema kwamba viwango vya vifo nchini Italia vinaweza kuwa vya juu kutokana na jinsi madaktari wanavyovirekodi.

"Jinsi tunavyorekodi vifo vyetu vya ni kwamba watu wote wanaofariki wakati wa janga hili wanafariki kutokana na virusi vya corona."

Taasisi ya kitaifa ya afya inasema kwamba umri wa wastani wa wale waliofariki ni miaka 81, huku idadi kubwa yao wakiwa wanaugua magonjwa mengine. **DW/BBC**



## Mbarali sasa wahimizwa fursa ya kilimo

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WANANCHI wa Kata ya Chimala wilayani Mbarali, wamekumbushwa kutumia vyema fursa za uchumi zilizopo katika wilaya hiyo, ikiwamo kilimo cha zao la mpunga.

Aidha, wameshauriwa kuhakikisha wanafuata ushauri wa wataalamu wa kilimo ili kujiongozea kipato.

Wito huo ulitolewa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ambaye ni Diwani wa Kata ya Chimala, Francis Mtega, ambaye alisema ni vyema wananchi kufuata kanuni bora za kilimo ili kuongeza uzalishaji kwa kuwatumia wataalamu kupitia programu ya kilimo shadidi.

Mtega alisema zao la mpunga ni miongoni mwa mazao ambayo yana faida, lakini mkulima akipuuza ushauri wa kitaalamu anaweza kuingia hasara.

Wilaya ya Mbarali ambayo kilimo chake hutumia njia ya kupandikiza huku mvua ikitegemewa zaidi, wakulima wake wamekuwa wakipata mavuno ya kuridhisha ukilinganisha na Wilaya ya Kyela ambayo kilimo hicho hutumika kwa kumwaga na kupandikiza miche.

"Tumeingia mwaka mwingine, hivyo kila mkulima wa Mbarali anatakiwa kuzingatia kilimo cha kisasa na hasa kuwashirikisha wataalamu wetu, cha msingi tuongeze bidii katika kilimo," alisema Mtega.

Akizungumzia maendeleo kuhusu vijana, Mtega aliwataka kuutendea haki mwaka mpya 2020 kwa kutofanya vitendo vibaya ambavyo vinaweza kuhatarisha amani ya nchi ikiwamo wizi, dawa za kulevya, huku akiwataka vijana kujishughulisha na hatimaye kutimiza ndoto zao.

Mmoja wa wananchi wa Chimala, Stella David, alisema ili kujiletea maendeleo ni vema mwaka mpya wananchi wakajituma kufanya kazi kwa bidii sambamba na kutumia fursa zilizopo.

Alisema kuwa kila mmoja ana wajibu wa kubadilika kwa kuangalia ni wapi alikosea kwa mwaka uliopita na kufanya yale ambayo hakuweza kufanikisha.

**"Tumeingia mwaka mwingine, hivyo kila mkulima wa Mbarali anatakiwa kuzingatia kilimo cha kisasa na hasa kuwashirikisha wataalamu wetu, cha msingi tuongeze bidii katika kilimo," alisema Mtega.**

# Walia na aliyezalisha mgonjwa wa akili kisha kutelekeza watoto

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WAKAZI wa Mtaa wa Iyela, jijini Mbeya, wameiomba serikali, kumsaka na kumkamata mtu asiyejulikana, ambaye amekuwa akifanya mapenzi na kumzalisha watoto mgonjwa wa akili kisha kuwatekeleza watoto waliozaliwa.

Imeelezwa kwamba mtu huyo aliwatelekeza watoto hao kwa bibi yao, ambaye hata hivyo, hana uwezo wa kuwahudumia.

Wakazi wa Mtaa huo walionyesha kusikitishwa na kitendo hicho na kuamua kuvitafuta vyombo vya sheria ili hatua zichukuliwe kwa mwanaume huyo.

Mmoja wa majirani wa familia hiyo, Joyce Moses, alisema mwanamke huyo alizalishwa watoto watano ambao kutokana na hali duni ya maisha, alishindwa kuwahudumia na kusababisha watoto watatu kati yao kufariki dunia.

Alisema maisha ya nyumbani kwao na mwanamke huyo ni ya ufukara kiasi cha kukosa hata mlo wa uhakika kwa siku na kuwasababishia matatizo ya kiafya watoto hao na baadhi yao kufariki dunia.

Bibi wa watoto hao ambaye ndiye mzazi wa mwanamke huyo, Anna Kipesile, alisema pamoja na mateso anayoyapata kuwalea watoto wa mwanawe, alieleza kusikitishwa na taarifa kwamba binti yake ana ujauzito mwingine.

"Huyo mwanaume anayempa ujauzito mara kwa mara mwanangu hafahamu kuwa ninaumia mno kwa sababu mzigo nilionao ni mkubwa wa kuhudumia familia na ukiangalia ana matatizo ya akili... naomba serikali na wadau wengine wa haki za binadamu wamtafute huyo mwanaume," alisema Kipesile.

Mkuu wa Dawati la Jinsia, Mkoa wa Mbeya, Mrakibu Msaidizi wa Polisi, Jannet Masangano, alisema kitendo anachofanyiwa mgonjwa huyo wa akili ni kinyume cha sheria kwa kuwa ni ubakaji.

Alisema Jeshi la Polisi Kitengo cha Dawati la Jinsia kinafanya utaratibu wa kwenda kwa mwanamke huyo kuongea naye, lakini kumtafuta mhusika anayempatia ujauzito na kumtelekezea watoto.



Wakazi wa Kijiji cha Holongo, Kata ya Igale, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wakiwa kwenye msongamano sokoni jana, kwa ajili ya kujipatia mahitaji mbalimbali bila kuwa na tahadhari ya tishio la maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona nchini. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Waonywa kuzaa bila mpangilio

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WANAWAKE mkoani Mbeya, wamekumbushwa kutumia njia sahihi za uzazi wa mpango.

Wameshauriwa kuwa kama hawana utayari wa kuzaa au kuwa na familia wasizae ili kuondoa wimbi la ongezeko la watoto wa mitaani wanaotupwa na wazazi wao.

Wito huo umetolewa na Mwenyekiti wa Wanawake Wajasiriamali Mkoa wa Mbeya, Priscilla Mbwaga, alipokuwa akizungumza na Nipashe ambapo alisema ni muda mwafaka sasa kwa wanawake kujikita kwenye shughuli za kiuchumi badala ya kuzaa bila mpangilio.

Alisema kumekuwapo na ongezeko la watoto wa mitaani na kudai kuwa mwanamke ndio chanzo, hivyo kila mmoja ana jukumu la kuzingatia uzazi wa mpango na hata kutumia njia za uzazi wakati ambao hana utayari.

"Sisi wanawake tunaongoza kwa kuwatupa watoto na kuwafanya wawe watoto wa mitaani, wakati huo huo tunasifika kwa kuwa wazazi au walezi bora katika familia zetu, umefika wakati wa kujitathmini na kuzingatia uzazi wa mpango," alisema Mbwanga.

Ofisa Maendeleo ya Jamii, Mkoa wa Mbeya, Stella Kategile, alisema mkoa una vituo vingi vya kulelea watoto yatima ambao wengi wao wametokana na kutelekezwa na wazazi wao.

Alisema vituo hivyo vimebeba jukumu kubwa la kuwahudumia watoto, hivyo aliiomba jamii kuendelea kutoa misaada ya hali na mali.

Akizungumzia umuhimu wa kutumia uzazi wa mpango kwa makubaliano ya wenza, Mganga Mfawidhi katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Mbeya, Dk. Glory Mbwile, alisema kuna matatizo kwa baadhi ya wanawake wanaokwenda kujifungua hospitalini hapo kukosa fedha kwa ajili ya mahitaji mbalimbali kutokana na kutelekezwa na wanaume waliowapa ujauzito.

Alisema hali hiyo inatokana na wanawake kutokuwa makini au kupuuza kutumia njia za uzazi wa mpango ili kudhibiti mimba zisizotarajiwa.





## Ahimiza ubunifu vifaa vya corona

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, amewahimiza Watanzania kubuni vifaa vitakavyorahisisha unawaji mikono ili kukabiliana na ugonjwa wa corona.

Bashungwa alisema hayo jana alipokuwa akipokea kutoka kwa mjasiriamali kutoka mkoa wa Manyara, kifaa maalum cha kunawia mikono alichokitengeneza.

Alimshauri mjasiriamali huyo kukifanyia maboresho haraka yanayotakiwa ili kiingie sokoni na kiwasaidie wananchi.

"Nakupongeza Jonas Urio kwa ubunifu wako huu wa kutengeneza kifaa kizuri na bora cha kunawia mikono ambacho kinaweza kutumiwa na taasisi mbalimbali za serikali na binafsi kuhudumia watu mbalimbali kusafisha mikono yao ili kuendeleza mapambano dhidi ya corona," alisema.

Kwa upande wake, Mjasiriamali Urio ambaye ni mbunifu wa teknolojia hiyo, aliishukuru wizara hiyo kwa kumpa ushirikiano tangu awali alipoanza ubunifu wake hadi kufikia hatua hiyo.

"Nimesajiliwa na ubunifu hutambulika. Napokea ushauri wa maboresho ya kifaa hiki niliyopewa na Waziri na Naibu Waziri ambao wote kwa pamoja wamefurahia sana ubunifu wangu.

Naahidi kuwa nitakifanyia kazi maboresho yote haraka ili kifaa hiki kiingie sokoni," alisema.

**"Nimesajiliwa na ubunifu hutambulika. Napokea ushauri wa maboresho ya kifaa hiki niliyopewa na Waziri na Naibu Waziri ambao wote kwa pamoja wamefurahia sana ubunifu wangu.**

# Mvua yakosesha makazi watu 200

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

ZAIDI ya wakazi 200 wa Jiji la Dodoma wamekosa makazi baada ya nyumba zao kubomoka kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

Wakazi hao hivi sasa wamehifadhiwa na majirani zao wakati wakisubiri serikali kukarabati eneo hilo ambalo linahitaji ujenzi wa mitaro ya kupitisha maji.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, alisema serikali inajipanga kuhakikisha eneo hilo linakuwa salama kutokana na kwamba wamejipanga kujenga mitaro ya kupitisha maji.

Alisema lengo lao ni kuona wakazi wa eneo hilo na maeneo mengine mvua zikinyesha wanakuwa salama.

"Tunaomba wananchi wawe watulivu serikali imeliona hilo na inawahitaji watulie ili kulipatia ufumbuzi," alisema Katambi.

Hata hivyo, aliwaonya wananchi kuacha kujenga holela katika maeneo hatari ambayo maji yanayotiririka.

Alisema lengo la serikali ni kuona kila mmoja anakuwa salama kipindi cha mvua wote wawe wanahifadhi maji ya mvua ambayo huleta madhara.

Katambia alisema jamii inapaswa kuwa makini na ujenzi wa nyumba hususani katika maeneo ya mabonde yanayotiririsha.

Naye mkazi wa Kata ya Nkuhungu eneo la Bochela, Saleh Mussa, alisema wanapata shida kipindi cha mvua kutokana na eneo walilopo kuwa na maji mengi ambayo huongezeka na kusababisha nyumba kubomoka.

Alisema hivi sasa wakazi wengi hawana pa kuishi kutokana na nyumba zao kubomoka na mvua mkubwa zinazoendelea kunyesha.

Alisema wanaiomba serikali kuliangalia hilo ili wananchi wa eneo hilo wapate sehemu za kuishi na kwamba kwa sasa hawana cha kufanya kwa sababu nyumba zao zimebomoka na wamepewa hifadhi na jirani zao ambao wao nyumba zao hazijabomoka.




Wapigadebe wa daladala wakiwanawisha maji na sabuni abiria kwa ajili ya kujilinda na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona, kabla ya kuingia kwenye gari katika stendi kuu ya Sabasaba, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# DC abainisha mikakati kukabili corona

**Na Ibrahim Joseph, KONGWA**

MKUU wa Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma, Deogratius Ndejembi, ameagiza kila nyumba kuhakikisha inachukua tahadhari ya kujikinga na virusi vya corona kwa kuweka maji na sabuni kwa ajili ya kunawa mikono.

Pia amewaagiza watendaji wote kuanzia ngazi ya kitongoji hadi wilaya kuhakikisha wanalisimamia hilo ili kufikia malengo ya serikali ya kupambana na virusi hivyo.

Ndejembi alisema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu tahadhari zinazochukuliwa na wilaya hiyo na inavyojipanga kupambana na virusi vya ugonjwa huo.

Alisema wananchi wote wa Kongwa wanapaswa kuendelea kuchukua tahadhari ya kujikinga na ugonjwa huo kwa kuhakikisha kila nyumba inakuwa na maji ya kunawa mikono au vitakasa mikono.

"Katika hili tutahakikisha tunafuatilia kila nyumba ili kuepuka kuingia kwenye maambukizi ya virusi hivi ambavyo tunaambiwa na wataalamu kuwa bado tiba yake haijapatikana," alisema.

Alibainisha kuwa wataalamu wa afya katika wilaya walipatiwa mafunzo na serikali namna ya kupambana na corona kama wagonjwa watajitokeza katika eneo lao. Hata hivyo, alisema wilaya hiyo imejiandaa kwa kutenga maeneo matatu yaliyoandaliwa maalumu kwa kuwapokea wagonjwa virusi hivyo kama watajitokeza.


Aliyataja maeneo hayo kuwa Hospitali ya Wilaya ya Kongwa, Kituo cha Afya Ipwaga na upande wa eneo la Mkoka ambako wametenga eneo la majengo ya kilichokuwa chuo cha ualimu kilichoko eneo hilo.

Aliongeza kuwa katika maeneo ya mji mdogo wa Kibaigwa na Kongwa mjini wameweka wataalamu wa afya wanaosimamia kwenye masoko, vituo vya mabasi na maeneo ya biashara ili kujikinga na virusi hivyo hatari.

Sambamba na hilo, aliwaomba wananchi kuchukua tahadhari ya kuepuka kuzurura mitaani au kuacha kutembeleana pamoja na kepuka safari zisizo na ulazima ili kujikinga na virusi hivyo.

"Unajua mwananchi anapotoka kwake anakutana na watu wengi au kushika vitu vingi ni hatari kutokana na ushauri wa wataalamu walivyotuambia," alisema.

Mkuu huyo wa wilaya alisema serikali ilifunga vyuo vya elimu, shule za msingi na sekondari pamoja na kuzuia mikusanyiko yote kwa lengo kuhakikisha watu wake wanapumzika nyumbani kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo.



# 'Marufuku mikusanyiko fukwe za bahari'

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MKUU wa Wilaya ya Magharibi 'A' Abeid Juma Ali, amepiga marufuku mikusanyiko katika fukwe za bahari.

Aliwataka wazazi kuwalinda na kusimamia ulinzi wa watoto wao katika kipindi hiki taifa likiwa katika vita dhidi ya maambukizi ya corona.

Akizungumza katika pwani ya Mangroove katika Shehia ya Chuini, wilayani humo, Mkuu huyo wa Wilaya alisema serikali imepiga marufuku mikusanyiko na kuzuia shughuli zote zenye mikusanyiko zikiwamo za elimu ili kuzuia kuenea kwa virusi vya maradhi hayo, hivyo kila mmoja ana wajibu wa kutii maagizo hayo.

Alisema kila mzazi akitekeleza wajibu wake kikamilifu, kuna uwezekano mkubwa wa kuzuia kasi ya maambukizo ya ugonjwa huo ambao hadi sasa Zanzibar imethibitisha kuwapo wagonjwa watano.

"Serikali inapotoa maelekezo mjue kuwa hiyo ni amri na inapaswa kutekelezwa, kusimamiwa na kutii kwa kila mmoja wetu...kuanzia leo sitaki kuona mtu anakuja kuogelea katika eneo hili hadi hali itakapokuwa shwari katika kipindi hiki ni hatari kwenu," alisema Abeid.

Alitoa elimu ya madhara ya maradhi hayo kijamii na kuwapongeza viongozi wa shehia ya Chuini kwa kuendelea kusimamia agizo la serikali na kuwataka kuendelea kufanya hivyo kwa kukutana na makundi mbalimbali ya jamii katika shehia hiyo kupeana elimu.

"Tukumbuke sisi viongozi tunatakiwa kuwa mstari wa mbele kuihamasisha jamii na ikibidi tutumie nguvu za kisheria kwa wanaokaidi maelekezo ya serikali kuhusu vita hii," alisema Abeid.

Naye Sheha wa Shehia ya Chuini, Mohammed Shehe Kheir, alisema wameamua kuchukua hatua hiyo baada ya kubaini makundi makubwa ya watu wakiwamo watoto wanakusanyika katika ufukwe huo kuogelea jambo ambalo ni hatari. Alisema pamoja na hatua hiyo, shehia yake imechukua hatua za kuzifungia kambi za masomo ya ziada zilizokuwa zikiendelea kwa kificho pamoja na kuzuia mazoezi ya michezo mbalimbali kama moja ya hatua za utekelezaji wa maelekezo ya serikali.

"Maradhi haya ni hatari ndiyo maana kwa kushirikiana na viongozi wenzangu tukaamua kumualika mkuu wa wilaya ili tusaidiane kutoa elimu ya tahadhari dhidi ya maradhi ya corona na ninashukuru kuwa wananchi wameonyesha utii," alisema Kheir.

Alisema kuwa katazo hilo litakuwa endelevu na kuwataka wananchi wa shehia hiyo na nyingine wanaojumuika katika eneo hilo kutofanya hivyo kwa sasa ili kuzuia kasi ya maambukizi ya maradhi ya corona sambamba na kuchukua tahadhari wasiambukizwe.



Waziri wa Afya Zanzibar, Hamad Rashid Mohamed (kulia), akiwa na ujumbe wake, katika eneo la nje ya Bandari ya Mkoani mjini Zanzibar jana, baada ya kutembelea ujenzi wa kituo maalum cha kuhifadhi abiria watakaohisiwa kuwa na maambukizi ya virusi vya corona, kabla ya kufikishwa hospitali. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Uingiaji holela visiwani wadhibitiwa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAKUU wa mikoa miwili ya Pemba na kamati za ulinzi na usalama wametakiwa kudhibiti uingiaji wa watu kiholela kutoka nje ya kisiwa hicho ikiwa ni sehemu ya kudhibiti kuingia kwa maambukizi mapya ya corona.

Waziri wa Afya, Hamad Rashid, alisema hayo katika ziara ya mikoa miwili ya Pemba na kutembelea baadhi ya bandari maarufu ambazo hupokea wananchi kwa ajili ya kuingia wageni.

Alisema imebainika kwamba idadi kubwa ya wananchi wanaingia Pemba kutoka katika mikoa jirani ya Tanzania Bara na Mombasa - Kenya baada ya maeneo hayo kuingia hofu ya ugonjwa wa corona.

Baadhi ya bandari ambazo zimebainika kupokea wageni wengi kutoka nje ya nchi ikiwamo Mombasa - Kenya ni Shumba mjini, huko Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba pamoja na Tundauwa.

"Tumewataka wakuu wa mikoa na kamati za ulinzi na usalama kudhibiti uingiaji wa wageni kutoka nje ya nchi pamoja na kuweka ulinzi katika bandari zote ikiwamo rasmi na ambazo sio rasmi, lakini zinatumika na wananchi ikiwamo wavuvi," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Hemed Suleiman, alisema tayari kamati ya ulinzi imeimarisha doria na kufanya ukaguzi wa bandari zote ikiwamo rasmi kujua wageni wanaoingia nchini.

Masheha wametakiwa kufahamu wageni wanaoingia katika maeneo yao na kuhakikisha wanapimwa afya zao kabla ya kujumuika na wananchi.

"Tayari tumeimarisha doria katika ukanda wa mwambao wa pwani wote ikiwamo bandari ambazo sio rasmi, lakini zinatumiwa na wananchi kinyume na sheria," alisema.

Zaidi ya watu 200 wamethibitishwa kuingia Pemba wakitokea Mombasa kupitia bandari na Shumba mjini na Tundauwa huku wengi wakihofia ugonjwa wa corona.

# Uvuvi haramu wapungua hifadhi ya bahari

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

IDARA ya Maendeleo ya Uvuvi ya Serikali ya Zanzibar imesema uvuvi haramu kwa kutumia mabomu umepungua kwa kiasi kikubwa kufuatia doria zinazofanywa mara kwa mara katika maeneo ya ukanda wa hifadhi ya bahari ya Zanzibar.

Mkuu wa doria wa Idara ya Maendeleo ya Uvuvi, Haji Shomari, alisema hayo wakati wa kufanya doria katika ghuba ya hifadhi ya Minai inayounganisha eneo la Mkoa wa Kaskazini hadi Kusini Unguja.

Alisema uvuvi haramu wa kutumia mabomu kwa kiasi kikubwa ulikuwa ukifanywa kwa kuwashirikisha wavuvi kutoka nje ya visiwa vya Zanzibar.

Shomari alisema uvuvi huo ulikuwa chanzo kikubwa cha uharibifu wa matumbawe ambayo baadhi yake yamekufa kwa kushambuliwa na mabomu.

Vile vile, alisema katika kipindi cha miaka miwili 2018-2019 wamefanikiwa kufanya doria 1,532 ambazo hakuna wavuvi waliokamatwa wanaotumia mabomu.

"Tumefanya doria katika maeneo ya hifadhi ya ukanda wa bahari ya Zanzibar kwa muda mrefu sasa na tumebaini kwamba uvuvi wa kutumia mabomu umetoweka...tunashukuru kwa sababu athari zake ni kubwa sana," alisema.

Alitaja aina nyingine za uvuvi haramu ambao umepungua kwa kiasi kikubwa kufuatia kuimarishwa kwa doria ni wa kutumia nyavu za kukokota pamoja na bunduki.

Alisema uvuvi huo umepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na ushirikiano wa kamati za uvuvi za shehia mbalimbali za Unguja na Pemba.

"Tunazipongeza kwa kiasi kikubwa kamati za uvuvi za shehia za hifadhi kwa kazi kubwa ya kupambana na uvuvi haramu unaofanywa na wavuvi kwa lengo la kupata kipato kikubwa," alisema.

**"Tumefanya doria katika maeneo ya hifadhi ya ukanda wa bahari ya Zanzibar kwa muda mrefu sasa na tumebaini kwamba uvuvi wa kutumia mabomu umetoweka...tunashukuru kwa sababu athari zake ni kubwa sana," alisema.**

# Masasi waomba vifaa kujikinga maambukizi ugonjwa wa corona

**Na Hamisi Nasiri, MASASI**

WAKAZI wa vijiji vya Nasindi na Mkolopola wilayani Masasi mkoani Mtwara, wanaomba serikali iwapelekee vifaa vya kutakasa mikono kwenye vijiji vyao ili waweze kuvitumia kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa wa corona.

Wakizungumza na gazeti hili jana kwa vyakati tofauti wilayani humo katika kijiji cha Nasindi, walisema kwenye vijiji vyao hawajawahi kuona vifaa vinavyotangazwa na Wizara ya Afya maarufu kama vitakasa mikono ambavyo vinahimizwa na serikali kwa ajili ya kujikinga na maambukizi ya gonjwa hilo.

Kutokana na hali hiyo, wameiomba serikali kusambaza vifaa hivyo hadi vijijini.

Mkazi mmoja aliyejitambulisha kwa jina moja la Adolfu, wa Kijiji cha Nasindi, alisema licha ya ukosefu wa vifaa vya kutakasa mikono kwenye vijiji vyao, pia elimu ya namna ya kujikinga uganjwa huo wa corona bado hawaipata kwa vitendo, hivyo baadhi ya wananchi hawatambui jinsi ya kujikinga.

Alisema wanaomba serikali ione namna bora ya kuwaangalia wananchi waishio vijijini kuwapatia elimu ya vitendo ya kujikinga na virusi vya corona kuliko kuendelea kutoa elimu hiyo kupitia kwenye vyombo vya habari pekee.

Alisema wapo baadhi ya wananchi ambao hawana utamaduni wa kufuatilia vyombo vya habari, hivyo kukosa elimu hiyo.

Alisema, lakini iwapo serikali ikiwafikishia moja kwa moja vijijini wanakoishi na kupatiwa elimu hiyo kwa vitendo.

Athumani Bakari, mkazi wa Kijiji cha Mkolopola, alisema kwenye vijiji vyao kwa upande wa elimu ya kujikinga na virusi vya corona haijatolewa, lakini hakuna sehemu ambayo kunauzwa vifaa vya kutakasa mikono na vifaa vingine kama barakoa.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Selemani Mzee, hivi karibuni alikutana na wataalamu wa idara wa afya na kuwaagiza kufika maeneo ya vijijini kutoa elimu kwa wananchi ya jinsi ya kujikinga virusi vya corona.

Alisema iwapo elimu hiyo ikitolewa maeneo ya mijini pekee, hilo itakuwa sio lengo la serikali bali lengo wananchi wote kwa ujumla wapatiwe elimu ili kila mmoja awe na ufahamu mzuri wa kujikinga na corona.



Mafundi ujenzi wakiandaa mawe kwa ajili ya kujenga ukingo wa maji ya bahari katika eneo la Kigamboni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# KSC yapiga jeki vita ya corona

**Na Sabato Kasika**

KATIKA kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona, Kampuni ya Sukari ya Kilombero (KSC), imeikabidhi serikali msaada wa lita 30,000 za malighafi za kilevi (Ethanol), ili kutengeneza vitakasa mikono (sanitizers).

Mbali na msaada huo, KSC pia imetoa punguzo la asilimia 22, kwa dawa za kilevi zinazotumika kutengeneza bidhaa hizo, kwa vile changamoto kubwa iliyopo sasa ni upatikanaji wa vitakasa mikono kwa gharama nafuu.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Biashara wa KSC, Fimbo Butallah, msaada huo umetolewa kupitia Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ili kupunguza uhaba wa malighafi za kutengeneza vitakasa mikono kwa wazalishaji wa ndani wa bidhaa hizo.

Mkurugenzi huyo alisema hayo jijini Dar es Salaam jana na kufafanua kuwa hatua hiyo ilifikia baada ya kukutana na Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Innocent Bashungwa.

"Hivi karibuni tulikutana na Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Innocent Bashungwa, katika mkutano maalumu na tulibaini kwamba moja ya changamoto kubwa iliyopo katika kipindi hiki ni upatikanaji wa vitakasa mikono kwa gharama nafuu," alisema Butallah.

Alisema, pia kuna ongezeko la mahitaji ya malighafi yenye kilevi inayotumika kutengeneza bidhaa hizo kwa wazalishaji wa ndani ili waweze kuzalisha bidhaa za kutosha na kuziuza kwa gharama nafuu.

"Kutokana na ongezeko hilo, tumetoa msaada wa lita 30,000 wa malighafi zenye kilevi, ambazo zinazalishwa kutokana na mabaki ya miwa katika mchakato wa kutengeneza bidhaa ya sukari," alisema.

Butallah alisema, wanayo akiba ya lita 100,000 za malighafi zenye kilevi, kati yake lita 30,000 wamezitoa kwa serikali, na lita 60,000 zitauzwa kwa punguzo la asilimia 22 kwa kila lita kwa wazalishaji wa ndani.

**"Kutokana na ongezeko hilo, tumetoa msaada wa lita 30,000 wa malighafi zenye kilevi, ambazo zinazalishwa kutokana na mabaki ya miwa katika mchakato wa kutengeneza bidhaa ya sukari," alisema.**

# Shivyawata yataka taarifa wenye ulemavu ombaomba

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

SHIRIKISHO la vyama vya watu wenye ulemavu Halmashauri ya mji wa Kibaha (SHIVYAWATA), limetoa wito kwa wakazi wa mji huo kutoa ushirikiano wa taarifa za watu wenye ulemavu ambao wanapita kuombaomba.

Akiongea na Nipashe, Katibu wa Shivyawata, Happiness Matagi, alisema, taarifa hizo zitasaidia kukomesha hali ya ombaomba kwa watu hao.

"Mkakati wetu tumeuanza mwaka jana na utakuwa endelevu, hatutaki kuona mtu mwenye ulemavu anapita kuomba omba wakati fursa zipo, kwa sasa kuna mikopo ambayo haina riba tusingependa kuona mtu anapita kuomba msaada mtaani," alisema.

"Tunapenda kuona watu wenye ulemavu wanajitegemea, na kama yupo ambaye hajiwezi tunakutana na msaidizi wake na kumpa elimu, kama mtu anaweza kutembea kutoka mjini hadi hapa Kibaha kuja kuomba anashindwaje kufanya kazi nyingine," alisema Happiness.

Katibu huyo alisema, katika harakati za kuhakikisha mji wa Kibaha hakuna ombaomba wamekuwa wakikutana na changamoto kutoka kwa kundi hilo.

"Wakati mwingine tukiwafuata na kuwaonya kuendelea na tabia ya ombaomba, wengi wao wanakuwa wakali wakisema 'kama wewe umeshapata tuache na sisi tupate' kauli hizi ndio zinazosababisha waendelee kuwapo mitaani," alisema.

Alisema, kwa sasa wamewaomba wananchi kutoa taarifa wanapowaona watu wenye ulemavu wanapita katika maeneo ya minada kwenye stendi kwingine wakiomba lengo kuwaondosha kabisa katika mji huo na wajikite kutumia fursa zilizopo.

Katika hatua nyingine, Happiness ameomba wadau kutoka ndani na nje ya Mkoa wa Pwani kuwasaidia kuwachimbia kisima cha kisasa ili waweze kupata maji ya kutosha katika mradi wao wa tofali.

Alisema, mradi huo ambao chama chao kimepata mkopo kutoka halmashauri kwa sasa unasuasua kutokana na kushindwa kumudu kulipa bili za mamlaka ya maji.

HABARI KIMATAIFA

## Corona yamwokoa kiongozi upinzani, atoka gerezani

**NIAMEY,** Niger

KIONGOZI mkuu wa upinzani nchini Niger, Hama Amadou, ameachiliwa huru pamoja na wafungwa wengine zaidi ya 1,000, kutokana na msamaha wa rais ambaye ameamua kupunguza wafungwa magerezani kama hatua ya kupambana na maambukizi ya virusi vya corona.

Kiongozi huyu aliondolewa katika jela ya Filingué jana, ambapo alikuwa akizuiliwa kwa tuhuma ya kufanya biashara ya watoto.

Amadou aliachiliwa huru pamoja na wafungwa 1,540 kufuatia msamaha wa Rais Mahamadou Issoufou ambaye alitangaza kuwa lengo hasa ni kupunguza idadi ya wafungwa kwenye magereza, wakati huu nchi yake ikipambana na maambukizi zaidi ya virusi vya corona.

Tangazo la kuachiliwa huru kwa kinara huyo wa upinzani nchini Niger lilipokelewa kwa furaha kubwa na wafuasi wake katika mji wa Niamey hapo jana, na kuenezwa kwenye mitandao ya kijamii, huku wanaharakati wa upinzani na hasa wale wa chama chake, Moden Fa Lumana, wakimpongeza rais wa nchi hiyo.

Hamadou alikuwa akiishi uhamishoni nchini Ufaransa, alirudi nchini Niger kwa hiari yake miaka minne iliyopita kutumikia kifungo kilichokuwa kimebaki katika kesi dhidi yake ya kusafirisha watoto nchini Nigeria. **RFI**

## Museveni atangaza marufuku kutoka nje usiku

**KAMPALA,** Uganda

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni ametoa amri ya kutotembea ovyo kote nchini kuanzia saa moja jioni hadi 12 asubuhi, ambayo ilitazamiwa kuanza kutekelezwa kuanzia usiku wa kuamkia jana.

Hiyo ni mojawapo ya hatua ambazo zimechukuliwa katika kuepusha kuenea kwa virusi vya ugonjwa wa virusi vya corona baada ya wagonjwa 33 kugunduliwa. Kipindi hicho kitachukua muda wa siku 14 kuanzia jana.

Nchini Uganda shughuli za kawaida nyakati za mchana zimebanwa baada ya magari yote ya watu binafsi kupigwa marufuku kuendeshwa ila tu kwa dharura na idhini kutoka kwa mkuu wa wilaya. Majengo ya maduka hayatafunguliwa isipokuwa tu shughuli za benki, ukusanyaji kodi na uuzaji wa vyakula katika masoko rasmi.

Akitangaza maagizo hayo siku ya Jumatatu jioni, Rais Museveni aidha aliagiza viwanda kufunga kama hawezi kuwaweka wafanyakazi katika kambi ya muda eneo la kazini kwao.

Katika hatua ya kuwapunguzia mzigo wafanyabiashara katika kipindi hiki, kiongozi huyo wa Uganda aliahidi kushauriana na benki, mashirika ya maji na umeme kutowaandama wanaodaiwa kwa sasa wala kuwakatia maji na umeme. **DW**

# China yafungua viwanda, uzalishaji waendelea

**BEIJING,** China

UZALISHAJI viwandani umeanza tena nchini China wakati maofisa wakilegeza udhibiti wa kupambana na virusi vya ugonjwa wa corona.

Maofisa hao wameruhusu viwanda kufunguliwa na kuanza uzalishaji, uchunguzi rasmi ulionyesha jana. Lakini kundi moja la viwanda limeonya kuwa uchumi hautaweza kurejea katika hali ya kawaida.

**China imeripoti visa vipya 48, na vifo vingine vinne, katika idadi mpya iliyotolewa na tume ya taifa ya afya.**

Chama tawala cha kikomunisti kinajaribu kufufua uchumi wa nchi hiyo ambao ni uchumi wa pili mkubwa duniani baada ya kutangaza ushindi dhidi ya virusi vya ugonjwa huo hata wakati Marekani na nchi nyingine zikiwa zinafunga biashara zao.

Wataalamu wa kiuchumi wa serikali kuu na sekta ya binafsi wametahadharisha kuwa uchumi wa nchi hiyo unakabiliwa na changamoto wakati uzalishaji unajengwa upya.

Walieleza kuwa usambazaji wa bidhaa na maofisa wanajaribu kuzuwia ongezeko la maambukizi wakati wafanyakazi wakianza tena kurejea kazini.

Wakati huohuo, mataifa yaliyoathirika na virusi vya corona yameingia katika wiki nyingine ya udhibiti mkubwa wa kuzuwia watu kutembea nje.

Zaidi ya watu 777,000 wameathirika duniani kote na zaidi ya watu 37,500 wamefariki duniani.

China imeripoti visa vipya 48, na vifo vingine vinne, katika idadi mpya iliyotolewa na tume ya taifa ya afya.

Idadi ya watu walioambukizwa na virusi vya corona nchini Ujerumani imepanda na kufikia watu 61,913, na watu 583 wamefariki kutokana na ugonjwa huo, kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa jana na taasisi ya utafiti wa magonjwa ya kuambukiza ya Robert Koch. **DW**



Hali inavyoonekana katika mojawapo ya mtaa wa Kampala, Uganda baada ya Rais Yoweri Museveni kutangaza watu kutokutoka nje kwa muda wa siku 14. **PICHA: ALLIANCE**

# Rais mstaafu Congo afariki kwa corona

**BRAZZAVILLE,** Congo

RAIS wa zamani wa Congo-Brazzaville, Jacques Joachim Yhombi Opango, ambaye alitawala nchi hiyo kati ya mwaka 1977 na 1979, amefariki dunia akiwa na umri wa miaka 81.

Taarifa kutoka katika familia yake zinaeleza kuwa kifo chake kilitokea juzi nchini Ufaransa kutokana na ugonjwa wa virusi vya corona akiwa na umri wa miaka 81.

Pia ilieleza kuwa hali ya afya ya rais huyo ilikuwa imezorota hivi karibuni, na kumlazimu kuishi mbali na nchi yake, nchini Ufaransa.

Ilieleza kuwa alikuwa akiishi nchini Ufaransa na Congo-Brazzaville tangu kumalizika kwa muda wake wa kuishi nje ya nchi mwaka 2007.

"Baba yangu, Rais wa zamani, Yhombi Opango, alifariki dunia Jumatatu mchana katika Hospitali ya Neuilly-sur-Seine karibu na Paris. Alikuwa mwathirika wa ugonjwa wa corona," alisema Jean-Jacques Yhombi Opango ambaye ni mtoto wake wa kiume.

Taarifa hiyo ilithibitishwa baadaye jioni na televisheni ya serikali ya Congo-Brazzaville, Télé-Congo.

Jacques Joachim Yhombi Opango alizaliwa mwaka 1939 huko Cuvette, Kaskazini mwa Congo-Brazzaville. Yhombi Opango, ambaye alikuwa ofisa wa zamani, alichukuwa madaraka mara tu baada ya mauaji ya kuhuzunisha ya Rais Marien Ngouabi (1968-1977).

Jacques Joachim Yhombi Opango aliongoza Congo-Brazzaville kwa miaka miwili tu kabla ya kutimuliwa madarakani na Waziri wake wa Ulinzi, Rais wa sasa Denis Sassou Nguesso, kutoka mkoa wa Cuvette.

Hata hivyo Rais Jacques Joachim Yhombi Opango alikamatwa na kufungwa kwa kipindi cha miaka 10, kabla ya kuachiliwa huru muda mfupi kabla ya mkutano wa kitaifa wa mwaka 1991 ambao ulifungua ukurasa mpya kwa nchi kwa kuanzishwa mfumo wa vyama vingi. **RFI**

# Aahidi kuvaa gunia kwa siku 40 kuomba corona itoweke

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

KIONGOZI wa Kanisa la Sauti ya Uponyaji lililoko Kihonda mjini hapa, Nabii Joshua Mwantyaka, ameahidi kuvaa gunia kwa siku 40 mfululizo katika ibada zake ili kwa niaba ya Watanzania, amlilie Mungu kutoa toba na maombolezo kwa ajili ya kuuondoa ugonjwa wa corona.

Alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari na kuwataka Watanzania kutumia silaha zote za kisayansi na kiimani, kuchukua tahadhari zinazotolewa na wataalamu wa sekta ya afya kukabiliana na ugonjwa huo.

"Janga kama hili liliwahi kutokea miaka ya nyuma wakati wa enzi za Mfalme Daudi, kuliibuka magonjwa mabaya ya mlipuko na Daudi alivaa gunia na kumlilia Mungu na magonjwa hayo yaliondoka hivyo na mimi nimeamua kufanya hivi ili kuliombea taifa na ugonjwa huu uishe kabisa," alisema.

Licha ya kupongeza hatua ya Rais Dk. John Magufuli kutoa kipaumbele kwenye suala la kiimani kwa kuruhusu ibada kuendelea, alimpongeza kwa kuyaruhusu madhehebu ya dini kuendelea na ibada badala ya kuyazuia kama ilivyo kwa nchi nyingine na kwamba hatua hiyo imeonyesha maono aliyo nayo, kuwa yapo majanga yanayoweza kushughulikiwa kisayansi na wakati huo huo kuhitaji nguvu za kiimani kukabiliana nayo.

Alisema licha ya madhehebu ya dini kutumia tahadhari zote za kiafya zinazoshauriwa ikiwamo kuhakikisha waumini wao wananawa mikono kabla ya kuingia kwenye nyumba za ibada kwa kutumia maji yanayotiririka na sabuni, kuwataka kukaa kwa kuacha nafasi ili wasibanane au kugusana, na tahadhari zingine, bado maombi ni muhimu kama silaha nyingine ya kiimani kukabiliana na janga hilo.

"Hatupaswi kupuuza kwa vile nchi zingine hali imekuwa mbaya, na hatupaswi kuiabudu corona kuwa itatushinda, wakati wanasayansi wanapambana kupata tiba, na wataalamu wa afya wakihimiza namna bora ya kujikinga na sisi tuendelee kupambana kiimani kwa kumuomba Mungu atuepushe na janga hili," alisisitiza Nabii Joshua.

Alishangazwa na baadhi ya wanasiasa kupinga kuwa masuala ya kiimani hayasaidii kukabiliana na corona badala yake akataka Watanzania kutumia silaha zote mbili za kisayansi na kiimani kukabiliana na ugonjwa huo na kumwomba Mungu aondoa tatizo hilo.

Baadhi ya wananchi wa Morogoro, Oliva Ramadhani na Shaban Salum, alisema wameendelea kuchukua tahadhari zote kujikinga na ugonjwa huo ikiwamo kuweka maji na sabuni kwenye sehemu za makazi na biashara na kuwasihi Watanzania kutambua ugonjwa huo haubagui wala kuchagua mtu kwa rangi, jinsia, uwezo, wala itikadi zake hivyo ni lazima kila mmoja ajilinde kwa kutambua hatari za ugonjwa huo.

Mwisho.




Mkazi wa jijini Dar es Salaam, Hussein Kilangilo, akiwa na bango lake kichwani linalohamasisha jamii kuzingatia maelekezo ya serikali ili kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona, katika eneo la Mikocheni, juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Katavi yapata msaada magari 2 kutoa elimu

**Na Neema Hussein,** KATAVI

SHIRIKA la Population Service International (PSI) limetoa msaada wa magari mawili yatakayotumika kutoa elimu ya kujikinga na virusi hivyo maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Magari hayo yametolewa jana na Mratibu wa PSI mkoa wa Katavi, Catherine Bukuku na kukabidhiwa kwa uongozi wa mkoa huo.

Akizungumza baada ya makabidhiano hayo, Bukuku alisema msaada huo ni kwa ajili ya kutoa huduma za masuala ya corona na sio shughuli zingine za kiserikali.

"Tumeamua kutoa magari haya kwa ajili ya kuisapoti serikali kupambana na janga la corona, haya magari yatatumika kwenda kutoa elimu sehemu mbalimbali katika kata na vijiji vya mkoa wa Katavi pia kupeleka watoa huduma," alisema Bukuku.

Mkoa pia umepokea wataalamu kutoka Shirika la Msalaba Mwekundu (Red Cross) kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu kujikinga na corona.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Omary Sukari, alisema kwa kuwa vyombo vingi vya habari katika mkoa huo havifiki maeneo ya vijijini kupitia vipaza sauti vya magari hayo watahakikisha elimu ya corona inafika maeneo yote ya vijijini.

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera, alilishukuru shirika hilo na Red Cross kwa msaada walioutoa katika kuhakikisha mkoa wake unajikinga na virusi vya corona.

**Mkoa pia umepokea wataalamu kutoka Shirika la Msalaba Mwekundu (Red Cross) kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu kujikinga na corona.**

# Wanaopokea wahamiaji mipakani waonywa

**Na Shaban Njia,** NGARA

SERIKALI wilayani Ngara, mkoani Kagera imewataka wananchi kuacha tabia ya kuwapokea na kuwahifadhi wahamiaji kutoka nchi jirani za Rwanda na Burundi ili kujikinga na ugonjwa wa corona ambao kwa sasa umeshaingia nchini.

Ilisema mwananchi atakayebainika kuwa na mhamiaji haramu ndani kinyemela atachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani yeye pamoja na raia wa kigeni atakaye kutwa naye.

Luteni Kanali Michael Mtenjele alitoa kauli hiyo jana, wakati akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu namna walivyojipanga kukabiliana na wahamiaji haramu kutoka nchi za Rwanda na Burundi kupitia mipaka isiyo halali (njia za panya).

Alisema, kwa sasa wanashirikiana na nchi hizo kukabiliana na raia wanaoingia na kutoka kinyemela bila kuwa na kibali na kwa mwananchi atakayebainika kumhifadhi raia wa kigeni kutoka katika moja ya nchi hizo atachukuliwa hatua za kisheria na mgeni wake.

"Tutahakikisha hakuna raia wa kigeni anayeweza kuingia nchini mwetu bila ya kuwa na kibali halali na hatutasita kumchukulia hatua za kisheria raia yeyote atakayebainika kumficha mhamiaji haramu ndani, huku akijua ugonjwa wa corona ni hatari," alisema.

Mmoja kati ya wananchi wa wilaya hiyo ambaye hakutaka jina lake kutajwa gazetini alisema, Wilaya ya Ngara ina mipaka bubu mingi ambayo serikali inatakiwa kuwekeza nguvu na wengine wakiingia nchini kwa kutumia mto Kagera.

Alidai kuwa, upande wake Rwanda wahamiaji haramu hupitia katika njia ya Ntobeye, Nyakiziba na Kasange eneo la Mafiga Matatu ambao huingia nchini na kuja kuajiriwa na raia wa ndani katika shughuli za kilimo.

Pia, alidai upande wa Burundi hupitia katika eneo la Mgoma, Kasange, Mabawe, Mruvyagila Tarafa ya Lulenge, Bugarama, Ruimbogo, Mganza pamoja na Rusahunga na mpaka ambao una maofisa Uhamiaji ni Kabanga na Rusahunga.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ELIMU/ MASOMO

**REGISTRATION OPPORTUNITIES KELAND NURSERY AND PRIMARY SCHOOL** located at salasala announces registration opportunities for Nursery and Primary School students. Call: 0713 327613.

## NYUMBA/VIWANJA

**NYUMBA INAUZWA,** Ninauza nyumba ya vyumba vinne vya kulala, kimoja ni master self contained. Ina vyumba vitano vya nyuma kimoja ni self contained, choo, bafu na jiko. Nyumba iko Ntyuka Dodoma karibu na shule ya sekondari Ntyuka. Nyumba iko kwenye kiwanja cha ukubwa wa SQM 2590. Ni nyumba nzuri sana kwa makazi na kupangisha. Kwa maelezo zaidi piga simu no. 0699-210258


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu:**


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA
KAGERA LILILOPO BUKOBA
RUFAA NA. 103/2019

CHARLES BUCHWA ..........................................MRUFANI
DHIDI YA
1. ALLY ABDU MABARAZA ..........................................................
2. JONAS CHARLES ....................................MRUFANIWA

KWA JONAS CHARLES (POPOTE ULIPO)

Mnaarifiwa/unaarifiwa kuwa maombi Na. 103/2019 yamepangwa kutajwa tarehe 20/04/2020 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, R. Mtei saa 2:00 asubuhi.

Hivyo unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/ mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 30/03/2020

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

BENEDICT WILLIAM KIWANUKA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 763DCE TOYOTA HARRIER yenye injini Na. 1NZ1586487 na Chasisi Na. MCU300002873.

Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa katika kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye.

Ametoa taarifa polisi na kupewa namba KAG/KAY/RB/148455/2020.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**EMANUEL JOSEPH MOSHI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **T 557 BRT** aina ya Boxer iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DAR/UR/RB/277544/2020.**

115685802

## KUPOTELEWA NA KADI ZA PIKIPIKI

**FELIX HENRY MTAVILALO** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki iliyokuwa na namba ya usajili **T391 BTH** na chassis namba **LBRSPJB51H9024989.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.TaarifayaPolisi: **IR/TR/RB/640/2019.**

215685202

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CASCO CONSTRUCTION LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 881 BHU** Mitsubishi Canter rangi ya Blue. Chassis namba **FE537B420050.** Engine namba **4D33D92052.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/MAG/RB/276043/2020.**

215685302


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# CHELSEA YAWEKWA PAZURI KUMSAJILI NEUER




**LONDON,** England

CHELSEA 'imeongezewa nguvu' kwenye harakati zake za kutaka kumsajili Manuel Neuer, baada ya golikipa huyo mzoefu kukataa ofa ya kuongezea mkataba mpya na Bayern Munich.

Frank Lampard anapigania kuleta golikipa mpya na Neuer, ambaye kwa sasa mkataba wake na Bayern unamalizika kipindi cha majira ya joto 2021, ni miongoni mwa chaguo linalofikiriwa zaidi pale Stamford Bridge.

Kama ilivyoripotiwa na gazeti la Bild, Bayern ilimpa ofa ya mkataba mpya utakaomalizika mwaka 2023, lakini kipa huyo anataka mkataba utakaomfikisha mwaka 2025.

Bayern ina hofu ya kumwongezea Neuer mkataba wa muda mrefu kwa sababu tayari wamefikia makubaliano na kumchukua Alexander Nubel kwenye umri wa miaka 23 kutoka klabu ya Schalke msimu ujao.

Akiwa amerudi kutoka kuwa nje ya dimba kwa muda mrefu kutokana na majeruhi msimu uliopita, Neuer amecheza katika mechi muhimu za Bayern msimu huu.

Kipa huyo mwenye umri wa miaka 34 nataka kuendelea kucheza kwa muda mrefu na anaweza kuchagua kuondoka Bayern kama hawatafikia makubaliano ya mkataba mpya.

# Martinez ni mali ya Inter - Wakala

**MILAN,** Italia

WAKALA wa Lautaro Martinez amesisitiza kwamba, mshambuliaji huyo akili yake ikijikita zaidi Inter Milan licha ya kuwaniwa na Real Madrid na Barcelona.

Martinez anachukuliwa mmoja wa wachezaji bora zaidi wa baadaye, huku msimu huu akiwa amefunga mabao 11 katika mechi 22 alizocheza kwenye Serie A.

Wakala Beto Yaque anajiamini kwamba uvumi unaoenea juu ya majaliwa ya mteja wake huyo mwenye umri wa miaka 22 hautaathiri kiwango mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina.

Kama ilivyoripotiwa vyombo vya habari vya Italia, Yaque amesema: "Inasemwa kwamba, Barcelona na Real Madrid wote wanamtaka yeye, lakini kwa upande wake ni kama hakuna kinachoendelea. Wengine wasingelala usiku.

"Hajawahi kunipigia simu na kuniuliza kama uvumi huo ni kweli, yeye akili yake amewekeza kwenye kazi yake ya sasa.

"Tumezungumza na watu wengi, lakini hakuna zaidi ya hilo. Kwa sasa wote wanaonipigia simu hawajasajiliwa na klabu zozote.


"Hakuna lolote rasmi lililofanyika. Kutakiwa sokoni ni jambo ambalo unaweza kuliota, lakini hatarajii chochote: Kitu pekee anachotaka ni kucheza na kufunga mabao.

"Kwa uvumi unaoenea sasa maana yake ni kuwa klabu bora duniani zinamtafuta Lautaro. Tunatumaini kazi yake italipwa kwa namna anavyostahili."

Barcelona inaangalia namba ya kuimarisha safu yake ya ushambuliaji huku wakitafuta mrithi wa muda mrefu wa Luis Suarez.

Mkataba wa sasa Martinez unamalizika kipindi cha majira ya joto mwaka 2023, lakini ni wazi kwamba ni yeye kuendelea kucheza pale Inter kwa muda mrefu.






# *Ceballos anataka kuondoka Arsenal*

**LONDON,** England

DANI Ceballos yupo tayari kuondoka Real Madrid kutafuta sehemu ya kucheza na angependa zaidi kurudi katika timu yake ya zamani ya Real Betis dhidi ya Arsenal.

Kiungo huyo ameonyesha kiwango cha kuvutia kwa muda wake aliocheza hapo kwa washikabundi na kocha, Mikel Arteta ameripotiwa kutaka kumsajili kwa mkataba wa kudumu.

Lakini gazeti la Estadio Deportivo limedai kwamba, mchezaji mwenyewe anataka kurudi Betis kuliko kuendelea kucheza hapo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 anajua kwamba anahitaji kupata timu ya kucheza mara kwa mara katika kikosi cha kwanza, ili apate nafasi ya kuitwa timu ya taifa ya Hispania kwa ajili ya michuano ya Euro 2021.

Ceballos alitumia misimu mitatu akiwa na Betis kati ya mwaka 2014 na 2017 kabla ya kuhamia pale Bernabeu.

HABARI MICHEZO

# Tite: Brazil inaweza kung'ara bila Neymar

**SAO PAULO,** Brazil

KOCHA wa Brazil, Tite amedai kwamba, nyota wa Paris Saint-Germain, Neymar si mtu 'muhimu' kwenye mafanikio ya timu ya taifa ya nchini hiyo.

Lakini pengo lake ni ngumu kuzibika kutoka na ukweli kwamba ana vitu ambavyo wachezaji wengine hawana.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 tayari amecheza mechi zaidi ya 100 za kimataifa, akisaidia kubeba kombe la shirikisho na medali ya dhahabu kwenye michezo ya Olimpiki.

Lakini pamoja na kwamba, mchezaji huyo anaonekana kuwa muhimu, Tite anaamini Brazil inaweza kufanya vizuri bila nyota huyo wa klabu ya PSG.

"Neymar ana umuhimu kubwa, kwa sababu analeta mambo yasiyotabirika kwenye mchezo," amesema kocha huyo wa timu ya taifa ya e Brazil akiliambia Jarida la France Football.

"Kwa sababu anauwezo binafsi ambao wengine hawana. Lakini Neymar ninayemzungumzia hapa ni yule ambaye yupo fiti kiakili na kimwili."

Nyota huyo wa PSG tayari anashika nafasi ya tatu katika orodha ya wafungaji wa wakati wote kwenye kikosi cha Brazil, nyuma ya Pele na Ronaldo, akiwa na mabao 61.







# GREALISH AOMBA RADHI BAADA YA AJALI

**LONDON,** England

JACK Grealish ameomba radhi na kupigwa faini na klabu yake ya Aston Villa baada ya kuvunja sheria ya kutotoka nje kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 alibainisha kwamba aliondoka nyumbani kwake wikendi iliyopita na kukutana na rafiki yake licha ya maelekezo kutakiwa kubaki nyumbani kutokana na hofu ya kuenea kwa virusi vya ugonjwa huo.

"Habari zenu, nataka kutuma ujumbe huu wa video kuomba radhi kwa kile kilichotokea mwishoni mwa wiki," amesema Grealish katika video hiyo aliyoituma kwenye mitandao ya kijamii.

"Najua kwamba ni wakati mgumu kwa kila mmoja kwa wakati tulionao, kufungiwa majumbani na nilipigiwa simu na rafiki yangu akinitaka tuonane na kwa upumbavu wangu nilikubali kwenda.

"Sitaki mtu yoyote afanye kosa kama langu, nataka kuendelea kubakia nyumbani na kufuata maagizo na maelekezo ya kile tunachotakiwa kukifanya.

"Najua ukweli kwamba, wengine wanaweza kufanya hivyo, lakini jambo la muhimu ni kubakia nyumbani na kufuata maelekezo.

"Natumaini kila mmoja anaweza kukubali radhi yangu na nafikiri baada ya hapo nina matumaini kwa siku chache zijazo tutaendelea kufurahia mchezo tunaoupenda."

# *Inter kumrudisha Sanchez United*

**MILAN,** Italia

INTER Milan imeripotiwa kwamba inapanga kusitisha mpango wa kuongeza muda wa kucheza kwa mkopo wa Alexis Sanchez klabuni hapo, baada ya kuwa na msimu usio na mafanikio tangu atue nchini Italia mchezaji huyo wa Manchester United.

Nyota huyo wa kimataifa wa Chile mwenye umri wa miaka 31 ameanza katika mechi mbili tu za Serie A kutokana na kukabiliwa na majeruhi ya mara kwa mara na sasa anaonekana kuwa njiani kurudi kule Old Trafford.

Fowadi huyo wa zamani wa Arsenal bado ana miaka miwili imebakia kwenye mkataba wake ambao unamfanya alipwe pauni 500,000 kwa wiki, lakini hajawahi kuwa kwenye kiwango cha kuvutia tangu alivyoondoka pale kwenye dimba la Emirates.

Sanchez ni maarufu kwenye vyumba vya kubadilishia nguo vya Inter, lakini matumaini yake ya kufanya mambo makubwa yalioshindikana kutokana na kukabiliwa na majeruhi ya kifundo cha mguu tangu Oktoba mwaka jana.

Fowadi huyo licha ya sasa kupona majeruhi, lakini ameshindwa kupata nafasi ya kucheza na sasa siku zake zinahesabika pale katika dimba la San Siro, kwa mujibu wa gazeti la Telegraph.

Antonio Conte ameamua kwamba, hamhitaji tena, na hivyo kutakiwa kurejea kule United wakati wa kipindi cha majira ya joto.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



## MESSI ATANGAZA BARCA KUKATWA MISHAHARA 70%

Ni kwa wachezaji wote kipindi hiki cha corona, pia watachangia kulipa wafanyakazi...

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA ni moja kati ya klabu nyingi za Ulaya zilizokubali kupunguziwa mishahara yao wakati huu wa janga la dunia la virusi vya corona (COVID-19).

**Wachezaji wa Barcelona wamekubali kukatwa asilimia 70 wakati huu dunia ikipambana na janga la virusi vya corona na kufanya mchango wa ziada ili kuhakikisha wafanyakazi mbali na wachezaji wanapata mishahara yao kamili.**

Nahodha Lionel Messi alisema hatua hiyo ilichelewa kwa sababu wachezaji walikuwa "wanatafuta fomula sahihi ya kuisaidia klabu".

Wachezaji wa Juventus na kocha wao, Maurizio Sarri nao walikubali kupunguza mishahara yao kwa kipindi cha miezi minne kipindi hiki cha janga la corona.

Watu waliofariki dunia Hispania kutokana na janga la corona hadi jana walifikia 7,340, idadi ambayo inaifanya kuwa nchi iliyopoteza watu wengi zaidi duniani baada ya Italia.

Miamba ya Ujerumani, Bayern Munich na Borussia Dortmund, pia imekubali kukatwa mishahara yao kutokana na janga hilo.

Katika taarifa yake, nahodha huyo wa Barca, Messi alisema: "Kabla ya kwenda mbali zaidi, tunataka kuliweka hili wazi mara zote tulikuwa tayari kupunguza mishahara yetu kwa sababu tunatambua sahihi kwamba tupo katika hali ya kipekee. Sisi, kama wachezaji, mara zote tupo hapa kuisaidia klabu wakati watakapotuomba.

"Haikuacha kutushangaza kuwa kutoka ndani ya klabu kulikuwa na wale ambao walijaribu kutuweka chini ya glasi ya kukuza na kujaribu kuongeza shinikizo kufanya kitu ambacho sisi kila wakati tunajua tutafanya.

"Kama hatukuzungumza hadi sasa, ni kwa sababu kipaumbele kilikuwa kutafuta suluhisho kuisaidia klabu na kuona nani muathirika zaidi wakati wa hali hii.

"Kwa sehemu yetu, wakati umefika kwamba, makato yatakuwa asilimia 70 kwa mishahara yetu wakati wa tahadhari hiyo. Pia tutaisaidia klabu ili wafanyakazi wake walipwe kwa asilimia 100 ya mishahara yao."

Bodi ya Wakurugenzi ya Barcelona, wanachama wa timu ya wataalamu wao na wachezaji wengi wa timu ya mpira wa kikapu pia wamekubali kupunguza mishahara yao.

## ZISIKUPITE

### UNITED KUMGEUKIA MADDISON

MANCHESTER United inaweza kugeuzia akili yao kwa kiungo wa Leicester City na England, James Maddison, 23, baada ya kumuwinda kwa muda mrefu na nahodha wa Aston Villa, Jack Grealish, 24, pia amejumuishwa katika tukio lingine nje ya uwanja. ***(Daily Star)***

### LIVER YAMPOTEZEA COUTINHO

LIVERPOOL haivutiwi kumsajili kwa mara nyingine kiungo Mbrazil Philippe Coutinho, 27, ambaye anacheza kwa mkopo Bayern Munich akitokea Barcelona. ***(Mirror)***

### GOMES AIVUTIA REAL, BARCA

REAL Madrid inamfuatilia kwa karibu kiungo wa Sao Paulo, anayeelezwa kuwa 'Kaka mpya', Igor Gomes, 21, wakati pia Barcelona, Sevilla na Ajax nazo zikivutiwa na nyota huyo wa Brazil wa U-20. ***(AS)***

### WILLIAN KUIAMSHA ARSENAL

KIUNGO wa Chelsea na Brazil, Willian, 31, yupo tayari kuendelea kuicheza Ligi Kuu England kama ataondoka Stamford Bridge, hatua ambayo inaiweka sawa Arsenal na Tottenham. ***(ESPN Brazil - in Portuguese)***

### NEUER AIFUNGULIA CHELSEA

Chelsea imeongezewa nafasi ya kumsajili Manuel Neuer, kufuatia kipa huyo mzoefu kuikataa ofa ya kuongeza mkataba mpya hapo Bayern Munich. ***(Daily Mail)***

### SPURS, ARSENAL KWA LOVREN

ARSENAL, Tottenham na West Ham zipo tayari kumsajili beki wa Liverpool, Dejan Lovren, 30, wakati huu Mcroatia huyo akionekana kutopewa nafasi hapo Anfield. ***(Teamtalk)***

### CEBALLOS AITAKA REAL BETIS

DANI Ceballos, 23, anaichezea Arsenal kwa mkopo angependa zaidi kurejea Real Betis kuliko kubaki hapo Uwanja wa Emirates, kama klabu yake mama Real Madrid haitahitaji kumrejesha Mhispania huyo. ***(Estadio Deportivo via Express)***

### MILANGO KUTIWA KUFULI EPL

LIGI Kuu England inafanyia kazi kuanza tena msimu milango ikiwa imefungwa katika wiki ya kwanza ya Mei wakati ratiba ikiwa imepangwa kumalizika Jumapili ya Julai 12, mwaka huu. ***(Daily Mail)***

### INTER KUACHANA NA SANCHEZ

INTER Milan imeripotiwa kujiandaa kutupilia mbali nafasi ya kuongeza mkataba wa mkopo wa Alexis Sanchez kufuatia nyota huyo wa Manchester United kutokuwa na msimu mzuri hapo Italia. ***(Daily Mail)***

### YAJIAMINI KWA GABRIEL

EVERTON inaamini itaipiku Arsenal na Chelsea katika mbio za kuinasa saini ya beki wa kati wa Lille, Mbrazil Gabriel Magalhaes wakati dirisha la usajili litakapofunguliwa. ***(Daily Telegraph)***

### KUTABASAMU DORTMUND

ERLING Haaland hataficha tabasamu lake wakati yeye na wachezaji wenzake wa Borussia Dortmund wakirejea uwanja wa mazoezi Jumatatu. ***(Daily Telegraph)***

HABARI MICHEZO

## Uhamiaji yapania kupanda Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KATIBU Msaidizi wa timu ya Uhamiaji iliyopo Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja, Mwinyi Khalidi amesema msimu huu wamepania kupanda daraja ili kucheza Ligi Kuu msimu ujayo, lakini hilo likitegemea kurejea tena kwa ligi hiyo baada ya kusimama.

Akizungumza na gazeti hili jana, alisema kwa muda mrefu wamecheza Ligi Daraja la Kwanza, hivyo msimu huu kiu yako kubwa ni kuona wanatoka katika ligi hiyo na kucheza Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao.

Alisema timu hiyo msimu huu imeanza vizuri licha ya ugumu uliopo katika ligi hiyo ambayo inaupinzani wa hali ya juu kutokana na timu zilizoshuka daraja kutamani kurudi Ligi Kuu, huku kiu hiyo pia ikizikumba timu zilizopo Ligi Daraja la Kwanza.

"Timu yetu inafanya vizuri, tulianza vizuri msimu huu, japo michezo ya katikati hatukuwa na matokeo mazuri, lakini baadaye tulinyanyuka na hii inatokana na hali ya mchezo wenyewe, matumaini yetu ya kupanda daraja bado hayajafutika na hiyo ndio mipango yetu ya kwanza pale tu tulipoanza msimu," alisema.

Hadi ligi hiyo inasimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona duniani, Uhamiaji ipo nafasi ya tatu ikiwa na alama 30 katika msimamo huo wa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja yenye timu 13, ambapo jumla ya timu nne zitashuka daraja msimu huu.

## Kabadi kujipanga mashindano dunia

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Chama cha Mchezo wa Kabadi Tanzania, unajiandaa kufanya mashindano ya Dunia yatakayofanyika Aprili 30, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa chama hicho, Abdallah Nyoni, alisema awali mashindano hayo yalipangwa kufanyika mwezi uliopita, lakini yalisogezwa mbele kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Nyoni alisema ugonjwa huo umewaathiri kutokana na gharama ambazo walikuwa tayari wamezitumia, kwa ajiili ya mashindano.

"Tayari tulikuwa tumelipa gharama za kambi Arusha pamoja na nyaraka za kusafiria kwaa baadhi ya wachezaji," alisema.

Alisema endapo serikali itaruhusu michezo kuanza kufanyika kufuatia kuisimamisha kwa kipindi cha mwezi mmoja kilichoanza tangu Machi 15, mwaka huu, wataanza rasmi mazoezi kwa kujiweka sawa kwa mashindano hayo.

# MWAMNYETO ATAKA MIL. 90/- MEZANI KUNG'OKA COASTAL

**Na Saada Akida**

LICHA ya Simba kudaiwa imeshamalizana na beki wa Coastal Union ya Tanga, Bakari Mwamnyeto, mchezaji huyo ametaka dau la milioni 90 mezani kwa timu inayohitaji huduma yake kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Akizungumza na Nipashe jana, Mwamnyeto alisema yupo tayari kuondoka Coastal na kujiunga na timu yoyote ambayo itakubali kutoa dau hilo.**

Alisema mbali na dau hilo la usajili pia anahitaji mshahara wa milioni tano kila mwezi ili kwenda kufanya kazi kwa timu inayomhitaji kwa msimu ujao.

"Hizi taarifa za kwamba nimechukuwa milioni 80 si za kweli, nina mkataba na Coastal, nipo tayari kuondoka endapo timu inayohitaji huduma yangu basi wakitoa dau hilo la milioni 90 niko tayari kujiunga na kuitumikia timu hiyo," alisema Mwamnyeto ambaye amekuwa katika kiwango cha hali ya juu msimu huu.

Alisema kikubwa ni maelewano kama timu husika itakuwa kutoa kuanzia dau hilo na mshahara aliotaja unaweza kumng'oa Coastal Union.

Mbali na kuhusishwa na Simba, lakini pia kuna taarifa kwamba nyota huyo aliyekuwa ameitwa katika kikosi cha Taifa Stars kilichokuwa kinajiandaa na fainali za Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), kabla ya kambi hiyo kuvunjwa kutokana na michuano hiyo kuahirishwa kufuatia mlipuko wa virusi vya corona (covid-19) , inadaiwa ameshalamba milioni 80 kutoka Simba, jambo ambalo amelikana.

Wakati Mwamnyeto akiweka wazi dau analohitaji, Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili ya timu hiyo, Hemed Ally 'Aurora', alisema wapo tayari kumuachia beki huyo kwenda timu yoyote ambayo itafika mezani kwao na kukubaliana.

"Waje mezani, kikubwa ni maelewano pande zote tatu, timu inayomhitaji na inayommiliki, lakini pia mchezaji husika," alisema Aurora.

MILIKI...



Mchezaji wa Mipango FC, Mohamed Ally (kulia) akimiliki mpira huku mpinzani wake wa timu ya Kulutini FC, Erick George, akijipanga kumkabili katika mchezo wa kirafiki uliopigwa mwishoni mwa wiki katika Uwanja wa Kulutini, Kivule jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Kakolanya: Sijutii benchi Simba*



**Na Saada Akida**

KIPA wa Simba, Benno Kakolanya amesema hatajutia maamuzi yake ya kuichezea timu hiyo kutokana tu na sababu ya kukaa benchi.

Kakolanya (pichani) ameyasema hayo wakati akijibu maswali ya mashabiki wa Simba kupitia kurasa za Twitter, Facebook na Instagram za klabu hiyo juzi.

Alisema hana kinyongo kuona mwenzake, Aishi Manula akidaka mechi nyingi kwa sababu wote wapo kwa maslahi ya timu kufanya vizuri.

"Anapopata mwenzangu nafasi ya kucheza (Aishi Manula) ni sawa sawa nimecheza mimi, ni sawa sawa amecheza Ally Salim kwa hiyo inakuwa ni sababu ya timu, si nafasi ya mtu mmoja mmoja," alisema.

Kakolanya alisema kukaa benchi na kupata nafasi ya kucheza mechi chache hakutamfanya kujutia maamuzi yake ya kuitumikia klabu yake hiyo ya Simba.

Alisema wachezaji wanaokuwapo ndani ni kwa ajili ya maslahi ya timu hiyo kuhakikisha wanapambana kufikia malengo yanayotarajiwa na Wanamsimbazi.

Kakolanya yupo katika msimu wake wa kwanza ndani ya Simba tangu asajiliwe kutoka kwa mahasimu wao wa jadi, Yanga Julai mwaka jana.

Wakati msimu unaelekea ukingoni, kipa huyo amedaka mechi 23 tu za mashindano yote zikiwamo za kirafiki zilizocheza Simba na kuruhusu jumla ya mabao 15.

# Michezo

Jumatano Aprili 1, 2020

Nipashe




Messi atangaza Barca kukatwa mishahara UKURASA 30

ATARUDI!...




Mshambuliaji wa zamani wa Yanga, Heritier Makambo (kwa sasa Horoya AC ya Guinea), anawindwa kwa mara nyingine na miamba hiyo ya mtaa wa Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam, ambayo imepania kumrejesha msimu ujao. **PICHA: MAKTABA**

## Yanga: Makambo lazima kieleweke

**Na Saada Akida**

WAKATI mashabiki na wanachama wa Yanga wakiwa na kiu ya kuona mshambuliaji wao kipenzi, Mkongomani Heritier Makambo akirejeshwa klabuni hapo, uongozi wa klabu hiyo umesema katika usajili ujao lolote linaweza kutokea na wapo katika mchakato wa kumrejesha straika huyo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mhamasishaji wa Yanga, Antonio Nugaz alisema wapo katika mikakati mikubwa ya kumrejesha mshambuliaji huyo pamoja na wachezaji wengi ambao wamependekezwa na Kocha Mkuu, Mbelgiji Luc Eymael.

Alisema Kamati ya Utendaji ya Yanga na ile ya usajili kwa kupitia nguvu kubwa ya wadhamini wao, GSM na SportPesa hakuna linaloshindikana na kwamba suala la dola laki tatu kwa klabu hiyo si tatizo linapokuja suala la kumpata mchezaji anayehitajika na benchi la ufundi.

"Kurejea kwa Makambo lolote linaweza kutokea kwani tayari mchakato unaendelea kwa mchezaji huyo na wengine watakuwa kuijenga Yanga na kurejea heshima yake, dola laki tatu si tatizo kwa Yanga," alisema Nugaz.

Alisema mipango ya kamati hiyo ya utendaji ni kufanya usajili ili timu msimu ujao iwe ya ushindani mkubwa na kuwapa raha mashabiki na wanachama wa klabu hiyo.

Mbali na Makambo, tayari uongozi wa Yanga umepanga kukaa meza mmoja na Azam FC kwa ajili ya mazungumzo kumnasa kiungo Salum Abobakar 'Sure Boy'.

Makombo aliondoka Yanga msimu uliopita baada ya kuuzwa na kusaini mkataba wa miaka mitatu katika timu ya Horoya FC ya Guinea, hata hivyo hajaweza kuwika akiwa na klabu hiyo.

# Kagere, Kahata waitesa Simba

### ●●● Wahofia mabao kupungua kikosini baada ya nyota hao kuwekewa ngumu kurejea, sasa...

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU Ligi Kuu Tanzania Bara ikiendelea kusubiri majaliwa ya serikali kuruhusu kurejea baada ya kufunga shughuli zote za michezo kwa kipindi cha mwezi mmoja kuanzia Machi 17, mwaka huu kutokana na kuepuka kasi ya maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19) vinavyoitesa dunia, Simba inateseka na uwezekano wa kuwapata baadhi ya nyota wake wa kimataifa waliorejea makwao, imeelezwa.

**Wachezaji nyota wawili wa Simba, Mshambuliaji Meddie Kagere na kiungo 'mahiri mpishi wa mabao', Fancisis Kahata, wameshindwa kurejea Tanzania kufuatia zuio lililowekwa nchini mwao la kutoka ama kuingia kutokana na janga la virusi vya corona.**

Simba inamtegemea zaidi Kagere katika safu yake ya ushambuliaji huku Kahata akiwa nguzo muhimu kwa timu hiyo kutokana na ubora wake wa kufunga na kutoa pasi za mwisho.

Hadi Ligi Kuu inasimama Simba ndiyo iliyopo kileleni ikiwa na pointi 71, ambazo ni 17 zaidi ya Azam FC inayoifuata katika nafasi ya pili, huku Kagere akiongoza katika orodha ya wafungaji bora akiwa na mabao 19 akifuatiwa na mshambuliaji wa Namungo FC, Reliants Lusajo aliyecheka na nyavu mara 11 hadi sasa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Meneja wa timu ya Simba, Patrick Rweyemamu, alisema licha ya kutokujua tarehe rasmi ya kuanza tena kwa ligi hiyo, wamepata pigo kutokana na wachezaji hao kukutana na zuio hilo linalowafanya kushindwa kurejea nchini kuungana na wenzao.

"Ni kweli Kagere na Kahata ni wachezaji muhimu kikosini, lakini hatuna namna ya kuwapata kutokana na mipaka ya nchini zao kufungwa, hatujui lini itafunguliwa na wao kurejea.

"Hata hivyo, itakapofunguliwa na wao kurejea bado watalazimika kukaa karantini kwa siku 14 kabla ya kuungana na wenzao," alisema Rweyemamu ambaye kitaaluma ni kocha.

Alisema kwa sasa ni suala la kumwomba Mungu ili kasi ya maambukizi ya virusi hivyo ipungue na kumalizika kabisa na michezo kurejea kwa kuwa hadi sasa bado haijajulikana ni lini ligi hiyo itarejea tena hata baada ya zuio la mwezi mmoja uliowekwa na serekali kupita.

Jana Simba ilitarajia kufanya kikao cha ndani kati ya uongozi wa klabu hiyo, wachezaji pamoja na benchi la ufundi, lakini Kagere na Kahata wakiwa miongoni mwa nyota ambao bado hawajarejea nchini.

Kagere yupo kwao nchini Rwanda ilhali Kahata akiwa kwao Kenya walipokwenda kwa mapumziko ya wiki mbili kabla ya mipaka nchi zao kufungwa.

Kwa mujibu wa Rais wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Wallace Karia, mchezaji yeyote aliyeko nje ya nchi akirejea nchini, itabidi kukaa karantini kwa muda wa wiki mbili na kisha kupimwa kama ana maambukizi ya virusi vya corona ama la kabla ya kuruhusiwa kuitumikia timu yake katika ligi hiyo.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >